**8 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 8 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023.

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023)*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa mwaka 2023 (*The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa mwaka 2023 *(The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)*.

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023.

**SPIKA:** Ahsante sana, naona mwingine na yeye amekuja Mheshimiwa Khadija Taya kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka 2023 (*The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Taya, tunakushukuru sana.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 558

### Hitaji la nyumba za walimu – Kibiti

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga nyumba za walimu Shule za Msingi katika Kata za Salale, Kiongoroni, Mbuchi na Maparoni Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa niaba ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa nyumba za walimu hususan katika maeneo ya visiwani na imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi bilioni 55.57 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 809 zenye uwezo wa kuchukua kaya 1,916.

Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Kata za Maparoni na Kiongoroni ambazo zipo visiwani, Serikali imepeleka shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili

za walimu *(2 in 1)* katika Shule za Msingi Maparoni na Jaja na taratibu za ujenzi wa nyumba hiyo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu hususan katika maeneo ya pembezoni ikiwemo katika Visiwa vya Kata za Salale, Kiongoroni, Mbuchi na Maparoni Kibiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika,pamoja na jibu zuri la Serikali lenye kuleta matumaini lakini kwa kuwa hii Tarafa ya Mbwera ipo visiwani na changamoto kubwa ya upungufu wa nyumba za walimu zaidi ya 35, hasa katika maeneo ya Twasalie, Kiongoroni, Mbuchi na Saninga. Je, Serikali inatupa matumaini gani kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025?

Swali la pili kwa kuwa Tarafa hii ya Mbwera siku za nyuma huko ilijengewa sekondari moja tu kwa ajili ya Kata zote tano lakini kwa sasa Mheshimiwa Mbunge Twaha Mpembenwe na wananchi wa Tarafa hizi hasa Kata ya Mbuchi na Msala wamejenga sekondari imefikia ngazi ya lenta. Je, Serikali ina mpango gani wa kuchangia jitihada hizi za Mheshimiwa Mbunge na Madiwani na wananchi wa maeneo haya ili kukamilisha hizi sekondari? ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba upatikanaji wa bajeti ndiyo kigezo kikubwa kinachoweza kusaidia shule hizo kujengwa.

Hivyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa Kata hizo za pembezoni hatutowaacha isipokuwa Serikali yao inaendelea kutafuta fedha na itaendelea kuweka fedha ili kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo anashirikiana na Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Mpembenwe kwa jinsi anavyofuatilia maendeleo ya wananchi wetu. Nataka nimhakikishie kwamba pamoja na kujengwa kwa shule ambapo kumekwama katika Kata hizo za Mbuchi na kule alikosema nataka nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kutenga bajeti katika mwaka ujao wa bajeti kama ilivyofanya katika mwaka huu kwa kutenga bilioni 55.75 ili kuendelea kusaidiana na wananchi kuweza kufikia malengo makubwa ya kuwapelekea elimu wananchi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu Mbunge wa Tunduru Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 559

**Watumishi wanaoripoti na kuondoka – Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuchukua hatua kwa Watumishi wanaoripoti na kuondoka bila kufanya kazi Wilayani Tunduru?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatoa waraka wa kusimamia masuala ya uhamisho wa watumishi kutoka mwajiri mmoja kwenda mwingine ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo

Waraka huo pamoja na mambo mengine, unaelekeza Mtumishi wa Umma kukaa kwenye kituo chake cha kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu kabla ya kuomba kibali cha kuhama kwenda katika kituo kingine cha kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia utaratibu huu ili kuhakikisha kuwa watumishi wanaopangiwa vituo vya kazi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru wanafanya kazi katika vituo vyao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa kutokana na Waraka huo wa Serikali sina uhakika sana kama unazingatiwa kwa Wilaya ya Tunduru, kutokana na mwaka jana tulipata Walimu wa Shule za Msingi 56 na waliohama ni 57. Je, Serikali ina mpango gani wa kutufidia wale waliohama?

Swali la pili, je, Serikali haioni haja ya kutoa Waraka maalum kwa ajili ya Tunduru pekee kwa kuwa wale wote wanaohama labda inawezekana kutokana na mazingira waliotokea na wanayokwenda kuyakuta hawakubaliani nayo.

Je, Serikali haioni haja ya kutuletea ama kuajiri waajiriwa ambao wanaotokana na maeneo yale ili waendelee kubaki pale na kupunguza kero hiyo ya kuomba kuhama? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu kilio cha wananchi wa Tunduru kilishafikishwa katika Ofisi zetu mbili zote ikiwemo Ofisi ya Rais, Utumishi ili kuweza kuyashughulikia na hizo taratibu kufuatwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali, kwa maana ya kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi hilo jambo tumeshalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi na Mheshimiwa Mbunge tutakapokuwa tayari tutakujulisha ili upate kujua hatua ambayo zimefikiwa katika jambo la kufidia hili *gap* lililopo katika upande wa walimu wako.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili nataka kumhakikishia Mbunge kwamba siyo taratibu za Serikali kutengeneza Waraka kwa ajili ya Halmashauri moja au Wilaya Moja. Waraka ni kwa ajili ya Tanzania nzima ili kuweza kukabiliana na changamoto iliyopo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imechukua kilio hicho na inakwenda kukifanyia kazi na itakapokuwa tayari tutakuja kumjulisha yeye pamoja na Bunge lako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru juu ya eneo linalohusu watumishi kuwa wako kwenye harakati za kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine muda mwingi kuliko hata kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge unajua kinachotokea, jambo hili linapaswa kupatiwa majibu ya uhakika kwa sababu ni kweli kabisa kwamba watumishi wengi wanapangiwa mahala na wanakwenda kule kwa mipango ya harakati za kuanza kuondoka toka siku waliyofika. Ni ukweli kwamba huwezi ukazuia *mobility* ya watumishi wa umma kwa sababu wao ni binadamu kuna changamoto na mambo mbalimbali yanayowasibu pia.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya watumishi ambao wao ni wanandoa wanachangamoto kubwa unamkuta mume yupo Kigoma, mke yuko Mbeya familia hii inapata changamoto ya

kutokuwa Pamoja, pia watumishi hawa hawatafanya kazi kwa ufanisi kwa sababu muda mwingi wanafikiria juu ya mwenza wake yuko mbali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili wacha tulichukue tusijibu kwa haraka tukae na mamlaka za ajira na hasa TAMISEMI ili tuweze kutengeneza mfumo mzuri, tuangalie pengine inawezekana huko Tunduma ambako wanahama walipelekwa ambao hawapendi Tunduma lakini wako wengi wanaopenda kwenda Tunduma kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, tutajaribu kutengeneza utaratibu tuone tunaweza tukafanyeje bila kuvunja umoja na mshikamano wa Taifa letu kwa sababu pia kuwapangia watu kutoka sehemu aliyotoka huko huko itakuwa ni jambo, lakini wapo wanaoweza kuwa wanapenda kwa kiasi fulani, tunaweza tukafanya maamuzi hayo kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 560

**Hitaji la vyombo vya usafiri kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwapatia vyombo vya usafiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kufuatilia Mikopo inayotolewa na Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha kwa kuwawezesha usafiri na kutenga pesa kati ya 500,000 mpaka 5,000,000 kwa ajili ya ufatiliaji kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa kanuni ya ufatiliaji wa mikopo ya makundi haya yakiwemo ya wanawake, vijana na walemavu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwezi Februari, 2023, Serikali iligawa pikipiki 916 kwa Watendaji wa Kata, pikipiki 85 kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, pikipiki 5, 889 kwa Maafisa Ugani wa Kilimo na pikipiki 1,200 kwa Maafisa Ugani wa Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusisitiza kwamba utumiaji wa vyombo hivyo kwa pamoja ndiyo utatuletea tija katika kufikia maendeleo ya kufuatilia vikundi vyetu na misaada inayoendelea kupelekwa katika zile asilimia 10. Nashukuru.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni pikipiki 85 zilizotoka kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii zimetoka kwa Mikoa 21 na Mkoa wangu wa Tabora zimetoka pikipiki nne. Pikipiki mbili zimeenda Wilaya ya Urambo kwa Kata ya Kazaroho na Uyumbu na zingine zimeenda Kaliua. Sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha inatenga pikipiki nyingi za kutosha kwa ajili ya kuwezesha Afisa Maendeleo, kwa ajili ya kazi hizi za kufatilia mikopo?

Swali la pili, Kanuni ya utoaji mikopo Februari 2021 iliwaagiza Wakurugenzi kutenga pesa 500,000 hadi milioni 5,000, 000 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mikopo lakini siyo kila Halmashauri ina uwezo wa

kuwa na pesa za kutosha. Swali langu kwa Serikali, haioni kama na Serikali yenyewe ni chanzo cha mikopo hii chefuchefu ambayo tunashindwa kukusanya na kufuatilia vikundi hai na ambavyo siyo hai.

Je, ina mpango gani kuhakikisha sekta hii ya Maafisa Maendeleo ya Jamii wanapata vitendea kazi vya kutosha? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jacqueline Kainja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la utengaji wa pikipiki hizi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utengaji au upatikanaji wa pikipiki hizi kigezo cha kwanza ni upatikanaji wa bajeti. Kwa hiyo, kama Serikali tutaendelea kutenga bajeti ili tuweze kuwafikia wananchi wote ikiwezekana Kata zote au Wilaya zote za Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwamba Halmashauri nyingine hazina uwezo wa kutenga pesa kwa ajili ya kupeleka Maafisa wetu kwenda kuangalia au kufuatilia vikundi hivyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa haya pia ni maelekezo ya Serikali kwamba Wakurugenzi wote katika Halmashauri zote wahakikishe kwamba wanaendelea kutenga fedha kama ambavyo imeelekezwa na wale ambao watashindwa maelekezo yetu ni kwamba wawasiliane na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuona ni jinsi gani tunatatua tatizo hilo.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 561

**Manispaa ya Morogoro kuwa Jiji**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro itakuwa Jiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uanzishaji au upandishaji hadhi wa Halmashauri upo kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijapokea kusudio la kupandisha hadhi Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuwa Halmashauri ya Jiji. Hivyo kwa sasa Serikali imeweka utaratibu katika kuimarisha miundombinu ya huduma za jamii kwa maendeleo yaliyopo kabla ya kuanzisha mamlaka mpya za utawala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kufuatana na swali la msingi, nilikuwa natanguliza tu, maombi yatakuja, tayari tumeshaongelea, kwa hiyo, yatakuja. Yakija naomba mtufikire.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza. Manispaa yetu ya Morogoro ina kata 29 lakini ina tarafa moja. Kata zake ni kubwa sana: Je, Serikali haioni kuwa inaweza angalau ikatupatia tarafa ya pili kusudi kuwe na tarafa mbili kwa sababu kata ni nyingi sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa sababu mkazo wa Serikali sasa hivi ni kuimarisha miundombinu pamoja na huduma za jamii; miundombinu ya Manispaa ya Morogoro bado siyo mizuri hasa kwa upande wa Barabara: Je, ni lini Serikali itaweza kuwapa fedha na kuwaongezea kusudi barabara zetu za Manispaa ya Morogoro ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongezwa tarafa ya pili. Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge na pia kuishauri Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kufanya vikao kwa ajili ya maombi hayo kama ambavyo amesema juu ya maombi ya kuwa Halmashauri ya Jiji. Utaratibu uko wazi. Kikao cha kwanza ni cha Bodi ya Ushauri ya Wilaya *(DCC),* baada ya hapo maamuzi yenu yanapelekwa katika kikao cha Mkoa, yaani Bodi ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* na baada ya hapo tunakwenda kumwasilishia Mheshimiwa Waziri ili sasa maamuzi ya kugawa Halmashauri yenu au Manispaa yenu ili mweze kupata tarafa ya pili na taratibu nyingine kwa ajili ya kuwa jiji ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, hilo ni jibu kwa swali la kwanza. Swali la pili, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia *TARURA* imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaimarisha miundombinu katika majiji yetu, Manispaa zetu na Halmashauri zetu zote zilizopo ndani ya nchi yetu. Hivyo nataka nimhakikishie tena Mheshimiwa Mbunge kupitia

Halmashauri yake, watengeneze bajeti yao, watengeneze vipaumbele vyao, watuletee Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tutakwenda kufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdulla Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 562

**Huduma za vyoo mashuleni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje Wanafunzi wenye mahitaji maalum katika huduma za vyoo kwenye shule za msingi na sekondari nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiboresha ramani za ujenzi kwa shule za msingi na sekondari ili kukidhi mahitaji ya makundi maalum ya wanafunzi. Kwa sasa Serikali imeelekeza kwamba kila panapojengwa matundu ya vyoo lazima kuhakikisha kwamba mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu nayo yanaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, Maelekezo yalishatolewa kwa viongozi wa ngazi mbalimbali ikiwemo Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa ujenzi wa shule mpya, ujenzi wa matundu ya vyoo uzingatie ramani ilyotolewa tarehe 20

Februari, 2023, ambayo ndani yake mahitaji ya watu maalum yameangaliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa baadhi ya watumiaji wenye mahitaji maalum baadhi huwa wanasota kwenda kupata huduma: Je, Serikali inaweza kuhakikisha kwamba vyuo na mashule vilivyojengwa hivi karibuni vimewekewa visaidizi maalum kwa watumiaji hawa kufika vyooni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Asha Abdullah Juma, almaarufu Bi. Mshua, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika taratibu za Serikali, katika kila Halmashauri wako watu wanaitwa Wakaguzi wa Ubora wa Shule zetu. Maelekezo yetu Serikali ni kwamba wakaguzi wote wa ubora wa shule, wapite katika kila shule iliyopo ndani ya Halmashauri zetu kuhakikisha kama hili hitaji au changamoto iliyoelezwa na Mheshimiwa Bi. Asha (Mshua), inafanyiwa kazi, kuhakikisha kwamba walemavu wote au wenye mahitaji maalum wote mahitaji yao yameangaliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 563

**Kujenga Kituo cha Utalii Kihesa – Kilolo**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, lini Kituo cha Utalii Kihesa Kilolo chini ya Mradi wa *REGROW* kitaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha taratibu zote za usanifu na makadirio ya ujenzi ikiwemo michoro ya usanifu *(Detailed Design),* kabrasha la zabuni *(Tender Document),* makadirio ya gharama za ujenzi na michoro *(BOQ)*. Kwa sasa tunasubiri kibali cha Benki ya Dunia ili taratibu za manunuzi zianze. Tunatarajia ifikapo Julai, 2023 tuwe tumempata Mkandarasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa hatua tuliyofikia. Pia namshukuru Naibu Waziri kwa juhudi kubwa aliyoifanya mpaka mahali tulipofika. Naamini hatakata tamaa, tumalizie kabisa.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu mawili ya nyongeza: La kwanza, kwa kuwa sasa Iringa inakwenda kuwa lango la utalii kusini. Ni namna gani Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunaingiza tamaduni, mazingiira ya Iringa, watu wa Iringa, vivutio vya Iringa ili viwe sehemu ya kutoa taarifa au picha halisi kwa watalii watakaokuja kusini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba viongozi wakiwepo Waheshimiwa Madiwani wanapewa semina kuhakikisha kwamba wanaupokea utalii kusini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niwataarifu tu wananchi wa Iringa hususan mikoa yote iliyoko kusini mwa Tanzania, kwamba malengo ya Serikali ni kuhakikisha tunatanua wigo kwa masuala mazima ya utalii. Ujenzi wa kituo hiki unaendana sambamba na kutanua wigo wa masuala mazima ya utalii. Kwa hiyo, tuna Hifadhi ya Ruaha katika maeneo yale ya jirani, lakini tutahakikisha tunaunganisha *package* zote za masuala ya utalii ikiwemo masuala ya utamaduni, masuala ya kihistoria, tunaunganisha na utalii wa wanyamapori. Haya yote yatakuwa yanaunganishwa kwenye *package* moja ambayo tutaisaidia sasa sekta hii iweze kukua katika maeneo mazima yaliyoko kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala lingine hili la viongozi wa kisiasa hususan Waheshimiwa Madiwani, kwa kuwa tunaanzisha kituo mahususi hiki, lazima tutatoa elimu kwa wananchi na viongozi ili nao watusaidie kutoa *promotion* katika maeneo hayo na pia waweze kutembelea vivutio hivi, kwa sababu tunaamini kiongozi anapofika katika eneo hilo, tayari anawahabarisha hata wengine ambao hawajawahi kufika katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako. Kuna Mheshimiwa amesimama, samahani. Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika kuendeleza utalii ukanda wa kusini…

**SPIKA:** Weka kisemeo chako vizuri.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza utalii ukanda wa kusini, Kata ya Kisaki kuna eneo linaloitwa Kisaki Majimoto ambapo kuna chemchemi inayochemsha maji kiasi hata cha kuweza kulifanya yai likaiva, je, Wizara ina mpango gani wa kutambua eneo hilo na kuliingiza katika kivutio cha utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa Wizara ni kuhakikisha maeneo yote ambayo yana vivutio vya kihistoria ikiwemo Majimoto; tuna maeneo mengi ambayo yana majimoto na eneo ambalo anatoka Mheshimiwa Mbunge, lakini tuna maeneo mengine mengi ambayo yana vivutio ambavyo bado hatujaviibua. Tunataka kila Mkoa, kila wilaya angalau mtalii yoyote anayefika katika eneo hilo, basi aweze kuona kivutio kilichopo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati tulionao ni mkubwa, tunachotafuta sasa hivi ni fedha ya kutosha ili mambo yasonge mbele.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 564

**Ajali za barabarani katika eneo la Mikumi – Ruaha Mbuyuni**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza: -

Je, ajali ngapi za barabarani zimetokea kati ya Mikumi na Ruaha Mbuyuni kwa Mwaka 2010 hadi 2022?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi 2022 ajali za barabarani zilizosababishwa na vyombo vya moto katika eneo la Mikumi hadi Ruaha Mbuyuni, barabara ya Morogoro kwenda Iringa ni 128. Mchanganuo wa ajali hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ajali zilizohusisha mabasi ya abiria ni 30, malori 42 na magari madogo 56, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Juzi kulikuwa na ajali ambayo imepoteza maisha ya watu watano na majeruhi hali zao ni mbaya; jana kulikuwa na ajali ambayo imejeruhi majeruhi wanane ambao hali zao ni mbaya; na hizi namba ambazo tunapewa na Serikali 128 ni namba za ajali ambazo ni kubwa mno, zina madhara makubwa:-

Mheshimiwa Spika, Swali langu kwa Serikali:-

(a) Serikali haioni wakati umefika sasa kwa sababu ajali hizi zina athari kubwa na pana kwa jamii yote, kutangaza eneo hili kama ni janga?

(b) Serikali haioni wakati umefika sasa Wizara ya mambo ya ndani kukaa pamoja na TAMISEMI na Wizara ya Afya kuangalia Kituo cha Afya Mikumi na Hospitali ya Mtakatifu Kizito kama maeneo ya kimkakati ya uokozi wa majeruhi ambao unatokana na ajali hizi, badala ya kukichukulia kama wanavyokichukulia sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ajali hutokea na kadiri alivyosema, katika kipindi cha miaka hii 12 zimetokea ajali 128. Kwa takwimu zetu, ajali hizi zimekuwa zikishuka kadiri Serikali inavyoimarisha usimamizi wa

sheria. Kwa mfano, mwaka 2010 tulikuwa na ajali 16 na majeruhi wakawa saba, vifo vinane; 2011 tulikuwa na ajali 14, vifo vitano na majeruhi 10, lakini kadiri miaka ilivyoongezeka ajali hizo zilipungua. Kwa mfano, mwaka 2021 ajali tano, vifo vitatu na majeruhi watatu; na mwaka 2022 ni ajali tano, vifo vitatu na majeruhi wawili.

Mheshimiwa Spika, kiukweli hata kama atakufa mtu mmoja, kwetu tusingependa kumpoteza kwa jambo ambalo lingeweza kuzuilika. Kwa hiyo, pamoja na dhamira yake kwamba litangazwe janga, sijaona kama kiwango hiki kinatufikisha mahali pa kutangaza kama hili ni janga.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tutaendelea kuimarisha doria kama inavyofanyika kwa wenzetu wa Iringa, Askari hufuatilia magari haya, na kwa kweli kule ajali zimepungua sana. Kwa hiyo, kupitia Bunge lako Tukufu, tumwelekeze *RPC* Morogoro aanzishe utaratibu kama uliofanywa na mwenzie wa Iringa kuona kwamba magari yanafuatiliwa kwenye maeneo ambayo ni *prone,* yenye mwelekeo mkubwa wa ajali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukaa pamoja kwa Wizara husika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia kupitia ushirikiano wetu kwenye vikao vyetu vya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, wadau wote aliowataja ni Wajumbe ili kuona namna ya kuimarisha huduma za uokozi katika Kituo cha Afya Mikumi na Hospitali ya Kizito iliyopo pale Mikumi. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika harakati za kuimarisha doria, Kituo cha Polisi cha Ruaha Mbuyuni hakina gari: Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia kituo hicho gari ili kuimarisha doria katika eneo hilo lililotajwa ili kupunguza ajali pia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli siyo vituo vyote vya Polisi vina magari. Tulichokifanya ni kuimarisha uwezo wa Makamanda wa Mikoa na wasaidizi wao kuwa na magari, lakini awamu inayofuata ni kuimarisha ngazi za Wilaya. Mheshimiwa Nyamoga Wilaya yako itapata gari kama haikuwa na gari la uhakika na tutakapoimarisha kwenye ngazi ya Wilaya tutaenda kwenye vituo vikubwa kama vya Ruaha Mbuyuni ili tuviimarishe. Kwa hatua za dharura tunaweza tukawapatia pikipiki za kuweza kuwawezesha wao kufanya ufatiliaji, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pale Mbezi eneo la Magari Saba kwenye barabara ya Njia Nane, nilipoteza wananchi wangu wengi sana kwa kugongwa na magari kila mara: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kushirikiana na Wizara ya ujenzi kuona sababu ya kujenga kivuko cha juu ili kuokoa maisha ya wananchi hao?

**SPIKA:** Sasa hapo sijaelewa kama hilo swali ni la kwako wewe au ni la…

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni la Wizara ya Ujenzi. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, nadhani ni swali la Wizara ya Ujenzi na siyo la Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, tutaangalia kama leo wanalo swali, watakujibu. Kama hawana, basi ulilete kama swali la msingi.

Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Bunge lako lilitunga sheria ya kutoza faini ya boda boda shilingi 10,000 kwa kosa ambalo mwendesha boda boda amefanya. Siku hizi kumetokea matatizo, boda boda sasa hawatozwi faini ya shilingi 10,000, badala yake wanapelekwa Mahakamani kutozwa faini ya shilingi 30,000. Nini tamko la Serikali kuhusu jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hii faini anayoisema ya Shilingi 10,000/= ni ya papo kwa hapo, lakini wakati mwingine Polisi wanatathmini ukaidi na uzoefu wa hawa vijana kufanya makosa makubwa ya barabarani na hivyo huwapeleka Mahakamani ili Mahakama ambacho ndiyo chombo cha mwisho katika utoaji wa haki watoe hukumu kulingana na uzito au uzembe unaosababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, kama amepelekwa Mahakamani na Mahakama imeamua vile, nadhani Mheshimiwa Mbunge tukubaliane. La muhimu ni kuwahimiza vijana wetu waepuke kufanya makosa wanayoweza kuyaepuka ambayo mengi yanasababisha ulemavu na vifo miongoni mwao, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana wa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalumu, sasa aulize swali lake.

Na. 565

**Uhitaji wa kupitia mitaala ya Vyuo Vikuu**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapitia Mtaala wa Vyuo Vikuu ili kufungamanisha elimu sambamba na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Mkenda, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 na Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu. Katika ngazi ya Vyuo Vikuu, kikanuni, mitaala huandaliwa na Vyuo Vikuu vyenyewe kisha kuidhinishwa na Seneti na kuwasilishwa Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya uhakiki na ithibati. Hata hivyo, tayari Wizara yangu imeshatoa maelekezo kwa Vyuo Vikuu kuhuisha na kufanya maboresho ya mitaala yote ili iendane na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ambayo kwa sasa inalenga kutoa Elimu itakayompa kijana wa Kitanzania elimu na ujuzi kwa mujibu wa mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi kupitia mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* vimepata mafunzo mbalimbali ya kuandaa programu zinazoendana na vipaumbele vya nchi na mahitaji ya soko la ajira. Aidha, Vyuo vimeunda Kamati za Ushauri wa Insia *(Industrial Advisory Committees)* zenye Wajumbe kutoka Sekta za Waajiri kwa ajili ya kuzishauri Taasisi za Elimu ya Juu kutoa programu zinazoendana na soko la ajira. Kupitia utaratibu huu, zaidi ya programu 300 zitaanzishwa au kuhuishwa ili kuendana na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa sambamba na mahitaji ya sasa ya kijamii, kiuchumi na soko la ajira, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri mno ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa sababu mradi wa *HEET* ume-*fund* vyuo vya umma pekee ambavyo viko 15 kati ya 47 vilivyopo nchini: Ni upi mkakati wa Serikali kuona namna wataweza kuviwezesha vyuo vya *private* ambavyo kimsingi ni vingi kwa idadi hii ili na vyenyewe viweze kufanya mapitio ya mtaala ili viendane na dira na mwelekeo wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna *terms of reference* zipi ambazo Serikali wameshavipatia vyuo vya *private* ambavyo

waliamua kuanza wenyewe kufanya mapitio, ili sasa kuona namna gani bora tunaweza tukafungamanisha dira na mwelekeo wa Serikali kwenye elimu ambayo inatolewa katika mtaala wa vyuo vikuu nchini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza pamoja na kwamba, fedha nyingi zaidi za Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation* zimepelekwa katika vyuo vya umma, bado fedha zimetengwa vilevile kwa ajili ya sekta ya vyuo binafsi kwa mfano, kutoa *scholarship,* lakini na mafunzo ambayo yanaendeshwa kwa ajili ya kubadilisha mitaala yanachanganya vyuo vyote bila kujali kama ni binafsi ama vya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TOR;* vyuo vyote, kama nilivyosema katika kujibu swali la msingi, vinatengeneza mitaala yao kwanza kwa kupitia kwenye seneti zao, baada ya kukamilisha ndio zinapelekwa kwenye *Commission* ya Elimu ya Juu kwa ajili ya kupata ithibati. Chuo kinapata kibali cha kuwa chuo kikuu kwa sababu, tunaamini seneti yao ina uwezo mkubwa wa kuidhinisha mitaala. Sasa sisi maelekezo yetu ni kwamba, sasa hivi tuanze kuongeza elimu ya mali na kuzingatia vipaumbele vya nchi, hilo tumeshazungumza na ma-*vice chancellors* wote wa vyuo vyote na wakati wa kupitisha kwenye ithibati kuna fursa ya sisi kuangalia ni kiasi gani wameji-*align* na muelekeo huo wa kitaifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia fursa hii kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kujenga vyuo vya *VETA* sehemu mbalimbali. Je, Serikali ina mkakati gani kufungamanisha mitaala ya vyuo vya *VETA* na sehemu

vilikojengwa? Kwa mfano Kagera tumepata Chuo cha *VETA,* tunaishukuru Serikali, kufungamanisha mtaala wa *VETA* na uchumi wa Mkoa wa Kagera kama kusindika kahawa, uvuvi na maeneo mengine kama madini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Vyuo vya *VETA* vinawaandaa watu kwa ajili ya ajira na kuweza kumudu mazingira ambayo wapo. Na mkakati wa Serikali ni kwamba, pamoja na zile kozi mbalimbali za *VETA* ambazo kwa kweli zina-*cut across* kwa mfano kusoma *wiring, electrical wiring* au *mechanics,* n.k., lakini kila Chuo cha *VETA* kinashauriwa kufanya kazi na maeneo yale pale, ili kuchagua baadhi ya masomo ambayo yanakidhi matakwa ya eneo lile ambalo wanafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, najua kwa mfano, chuo ambacho kinajengwa pale Mkuranga kutakuwa na mazungumzo na wanaojenga viwanda katika eneo lile kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, mafunzo yanayofanyika pale yanaendana na mahitaji. Kwa hiyo, kadhalika hata cha Kagera na sehemu nyingine tutaendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza swali kwamba, zamani tulikuwa na vyuo kama Sokoine kinahusika na kilimo, *IFM* kilikuwa kinahusika na fedha, Mzumbe inahusika na sheria na utawala, ardhi kinahusika na ardhi, lakini siku hizi kumekuwa na kozi mbalimbali zinazoingia ambazo zinatofautiana na asili ya vyuo hivi. Ni upi mkakati wa Serikali kuona vyuo hivi vinabaki kwenye asili yake, ili tuendelee kuzalisha wataalamu bora zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Sanga kwamba, kuna wakati vyuo vilipoanzishwa vilikuwa vina-*specialize* katika maeneo mbalimbali na vingine kwa kweli, vilikuwa ni taasisi ya elimu ya juu, lakini sio vyuo vikuu kwa tafsiri ambayo tulikuwanayo kwa mfano Mzumbe kilikuwa kinatoa *Advanced Diploma* badala ya kutoa *Degree.* Baada ya mageuzi ambayo yalitokea hapo kabla vyote vilipewa vibali vya kuwa vyuo vikuu na hivyo walikuwa wanaweza wakaanzisha *programs* mbalimbali na wakipata kibali walikuwa wanaendelea kwa hiyo, maana yake hata vyuo kama Sokoine vimeongeza baadhi ya *programs* nje hata ya eneo ambalo mwanzoni walikuwa wamelizingatia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hivyo tuna-*insist* na tutaendelea kufanya jitihada kuhakikisha kwamba, kila chuo kikuu kinajaribu kuwa na eneo ambalo wame-*specialize,* ili kuwa na *competence* kubwa zaidi. Kwa hiyo, kama Sokoine tutatarajia kwamba, waongeze nguvu sana kwenye kilimo, kuna chuo kama Nelson Mandela ambacho kime-*specialize* kwenye sayansi na teknolojia tungependa wa-*focus* zaidi kwenye sayansi na teknolojia na kadhalika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri; huko nyuma imezoeleka mara panapotokea mabadiliko ya mtaala, hizi *competence base* kwenye madarasa, Serikali inachukua walimu wa Serikali kwenda kuwapa mafunzo kwa ajili ya mabadiliko ya teknolojia, lakini shule za *private* wanachajiwa na wanalipia. Je, katika huu mtaala mpya unaoendelea sasa Serikali iko tayari kuanza kuunganisha walimu wa *private* na Serikali ili wawe wanakwenda pamoja kwa sababu, watoto wote ni wa kitanzani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kila mitaala inapobadilika Serikali hutenga bajeti kwa ajili ya kuwafundisha walimu kujiandaa kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala mipya. Ni kweli kwamba, wakati mwingine fedha ambazo zimekuwa zikitengwa zilikuwa zinakidhi tu kuweza kuwaandaa walimu wa sekta ya umma kwa ajili hiyo na sekta binafsi wanapohudhuria wakati mwingine walikuwa wanachangia au wanajigharamia wenyewe, lakini huduma nyingine wanapewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaongeza jitihada za kuhakikisha kwamba, mabadiliko ya mitaala ambayo yanakuja tutajitahidi kukusanya walimu wote bila kujali wanatoka sekta binafsi au sekta ya umma. Lakini kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu tunaweza tukawalipia hata wale wa sekta binafsi. Kama hairuhusu tutawaalika wahudhurie katika semina na mafunzo haya bila kuchajiwa chochote kwa sababu, wale wanaoandaa mafunzo haya na kumbi na gharama za chakula na kila kitu ni ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kusaidia vilevile shule binafsi kuandaa walimu wao. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 566

**Kukamilika kwa Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Ikweha, Mufindi Kaskazini**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Kata ya Ikweha uliopo Jimbo la Mufindi Kaskazini utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji Ikweha ni miongoni mwa skimu zilizoko katika Wilaya ya Mufindi yenye ukubwa wa hekta 500. Skimu hii ina mchango mkubwa katika kuboresha Maisha ya wananchi katika Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha za kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kupata gharama za kukamilisha ujenzi wa bwawa na miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya Ikweha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa muda wa kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, huu mradi umechukua muda mrefu sana kwenye utekelezaji wake, na Serikali tayari ilikuwa imeshaweka zaidi ya shilingi milioni 800 katika mradi huu. Wananchi wa Mufindi Kaskazini wameusubiri kwa muda mrefu sana. Je, Serikali sasa katika bajeti hii iko tayari kufanya huo upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, utekelezaji wa maagizo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi *Comrade* Chongolo alipotembelea Mradi wa Umwagiliaji wa Ruaha Mbuyuni katika Wilaya ya Kilolo kwa sababu ulikuwa una changamoto kubwa sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza; ni kweli zmetumika shilingi milioni 800 katika hatua ya awali ambayo kazi yake kubwa ilikuwa ni ujenzi wa banio, njia ndefu ya kilometa 3.5 pamoja na vivuko, lakini katika Mwaka wa Fedha unaokuja tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili kupata chanzo cha uhakika cha maji katika skimu hii, ili iweze kufanya shughuli za umwagiliaji mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, jambo hili pia, tulikaa na Mbunge wa jimbo, Mheshimiwa Kigahe, tulizungumza kwa pamoja namna ya kuweza kuboresha skimu hii na hasa katika kuhakikisha kwamba, tunajenga bwawa hilo kwa ajili ya chanzo cha maji cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, la pili la kuhusu Ruaha Mbuyuni; tulipokea maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na tayari mimi na Mheshimiwa Aweso tulishatuna timu ya wataalamu kwa ajili ya kwenda kuangalia, kufanya marejeo ya usanifu wa eneo lile na hasa kurudisha Mto Lukosi katika njia yake ya asili, ili iweze kusaidia maji yale yaende katika mashamba ya wananchi na yasilete athari. Na hivi sasa kazi inaendelea, naamini baada ya muda mfupi ujao tutapata gharama halisi na utekelezaji utaanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga Mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Mwanyahina katika Jimbo la Meatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alishawasilisha jambo hilo ofisini kwetu na tumekubaliana kwamba, nitawaelekeza wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwenda kuangalia lile bwawa lililoko pale kama litakuwa ni chanzo kizuri cha maji kwa ajili ya umwagiliaji. Na baada ya hapo

tutawatengea fedha kwenye bajeti inayokuja ili waanze kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kalenga lina skimu ambazo ni chakavu sana. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, skimu hizo zinafufuliwa na zinakuwa zinahudumia wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha miradi yote ya umwagiliaji inafanya kazi. Ninataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kuipitia miradi yote, tutakwenda pia katika Jimbo la Kalenga kuangalia na pia, wataalam wetu watafanya kazi tutahakikisha kwamba, miradi hiyo inafanya kazi na wakulima waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia vyanzo vya uhakika vya maji kama maziwa na mito kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Machi, 2023 mbele ya Mheshimiwa Rais tulisaini mikataba 22 kwa ajili ya kuyapitia mabonde yote ya kimkakati nchi nzima na hasa yale yenye mito na maziwa. Nataka nimuondoe hofu Mheshimiwa

Mbunge ya kwamba, tumezingatia hoja ya Wabunge humu ndani na tutalitumia Ziwa Victoria, Mto Malagarasi, Mto Ruhuhu, Mto Songwe, kule Litumbandyosi, pamoja na Kilombero, Mto Ngono, Mto Rufiji, hii yote tutaitumia kuhakikisha kwamba, tunafanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kasinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kufufua skimu ya umwagiliaji iliyoko Kijiji cha Makangaga, Kata ya Kiranjeranje, Jimbo la Kilwa Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale awali ni dhamiravya Serikali kuhakikisha skimu zote za umwagiliaji zinafanya kazi. Nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuangalia kama katika jedwali letu skimu hiyo haipo katika mwaka huu wa fedha, basi tutaitengea fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inafanya kazi na wakulima wanatumia skimu hiyo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Malinyi lina maji mengi sana yanayopotea bure. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Malinyi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo lote la Malinyi linaingia katika mradi huu mkubwa ambao tunaendelea nao wa Bonde la Kilombero na Ifakara Idete. Kwa hiyo, ndani yake humo tutapata nafasi ya kujenga skimu nyingi za umwagiliaji na wabanchi wa Malinyi watanufaika kupitia mradi huu mkubwa unakuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana:-

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Takwa, Kata ya Kinyomshindo, Jimbo la Chemba, kuna skimu ambayo imetelekezwa sasahivi. Siku za nyuma imepata fedha kutoka Serikalini. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuifufua skimu ile ya umwagiliaji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitahakikisha nashirikiana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wataalam wangu kwa sababu, ipo karibu hapa twende tukaiangalie muda wowote tutakaopata nafasi katikati hapa, ili tuweze kutoa maamuzi sahihi ya utekelezaji wa skimu hii, lakini lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha kwamba, skimu zote zinafanya kazi, ndio dhamira kuu. Kwa hiyo, kama hiyo ndio dhamira kuu maana yake hiyo skimu aliyoitaja ipo ndani ya mpango wa Serikali, baada ya kukaa na wataalamu wetu kuona namna ya kuweza kutekeleza mradi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana:-

Mheshimiwa Spika, katika jimbo ambalo mimi ndio mwakilishi wao, Halmashauri ya Itigi, kuna skimu moja tu. Je, Serikali sasa iko

tayari kuyatumia Mabonde ya Ipalalyo na Bonde la Mnazi kwa ajili ya kutengeneza skimu nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.
**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tupo tayari na tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kufanya hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele. Tutaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni.

Kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika, na mimi leo nina wageni 62; kwanza ni wachimbaji wa madini kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili kutoka Benki ya CRDB Tawi la *Palm Beach Premier* Dar es Salaam. Na huyu ni Ndugu Pendo Kitula, sijui yuko sehemu gani? Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Anthony Moshi, hawa wameambatana na Stephen Biseko, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia walimu pamoja na marafiki wangu ambao tulisomanao Shule ya Sekondari Loleza miaka 29 iliyopita, Loleza jamani iko Jijini Mbeya, lakini wao wanatoka nchi nzima walikotawanyika, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Hawa wameongozana na aliyekuwa Mwalimu Mkuu wakati huo, Mwalimu Sangicha Mosha, karibu sana, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Lakini pia, yupo Mwalimu Wendy Lulapangilo Machibya, huyu alikuwa ni mwalimu wa *Needlework,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia, Mwalimu Ernest Mwawela, huyu alikuwa Mwalimu wa Kifaransa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Seleman Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kutoka Burundi na hawa ni Profesa Sanctus Niragira ambaye ni Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo, karibu sana. *(Makofi)*

Ameongozana na Ndugu Tusanga Mukanga Sylvain, ambaye ni *Executive Director – LTA,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Beatrice Nyakora Marwa, ambaye ni *Regional Fisheries Director – LTA,* karibu sana. *(Makofi)*

Huyu naona ni wa hapa hapa huyu, kwa kitenge alichovaa, haya ahsante. *(Makofi)*

Ndugu Maria Rose Hatungimana ambaye ni *translator; Translator Officer to The Minister.* Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Sobomana Guillaume ambaye ni *Private Assistant to The Minister,* karibu sana. *(Makofi)*

Hawa wameambatana na watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Ndugu Abdallah Mitawi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Muungano, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Thomas Bwana, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Deogratius Paul ambaye ni Afisa Kiungo wa Mkataba wa Bonde la Ziwa Tanganyika, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia, wagebi wawili wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambaye ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Uwekezaji ambaye ni Dkt. Tausi Kida, karibu sana. *(Makofi)*

Lakini pia, yupo Ndugu Obedi Sayore, ambaye ni Kamishna wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wako pia Bungeni hii asubuhi.

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mary Masanja...

Waheshimiwa Wabunge, mnazungumza na mimi nimesimama. Tusikilizane.

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mary Masanja; Waheshimiwa Wabunge, mnazungumza na mimi nimesimama, tusikilizane.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Mary Masanja ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, na hawa ni wanafunzi wa Chuo cha *CBE* ambao wamehusika kuhamasisha utalii wa ndani kwa upigaji kura vivutio kwenye mashindano ya dunia, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Malleko ambao ni wadau kutoka *Dar 24 Media,* karibuni sana. *(Makofi*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Regina Qwaray kutoka Babati Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Mchafu ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mhambwe Mkoa wa Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo kutoka Arumeru, karibuni sana. *(Makofi*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joseph Tadayo kutoka Jijini Dar es Salaa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa David Kihenzile kutoka Taasisi ya *Response and Preparedness and Disasters Tanzania, (RAPID Tanzania)* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi na tisa wa Mheshimiwa Boniphance Getere kutoka Kanisa la *Calvary Assemblies of God* Ufunuo wa Yesu kutoka Mbwanga Kata ya Mnadani Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni Jukwaa la Uwezeshaji Kiuchumi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Ally Makoa ambao ni viongozi wa dini wakiongozwa na Sheikh Bashiru Mgeta na Paroko Michael Chipondo kutoka Kondoa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Issa Mtemvu ambao ni wanafunzi 25 na walimu wa tano kutoka Shule ya Msingi Beta ya Kibamba Jijini Dar es Salaam.

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Innocent Kalogeris ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Morogoro Kusini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Tumaini Magesa ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 110 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi Loam kutoka Jijini Arusha, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni tulionao Bungeni siku ya leo. Kuna jambo moja ambalo linahitaji kutolewa ufafanuzi.

Waheshiumiwa Wabunge, katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge unao endelea Serikali iliwasilisha orodha ya shughuli za nyongeza kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Bunge. Miongoni mwa shughuli zilizo wasilishwa ni Azimio la Bunge kuhusu pendekezo la kuridhiwa Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii katika uendelezaji wa maeneo ya Bandari nchini.

Baada ya kupokea shughuli hiyo na kwa mujibu wa matakwa ya kanuni zetu niliekeza Azimio hilo lifanyiwe kazi na Kamati mbili kwa pamoja, yaani Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, ambazo kwa mujibu wa Kanuni zilitakiwa kufanya uchambuzi pamoja na kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusu azimio hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia maelekezo hayo na matakwa ya Kanuni ya 108(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tarehe 5 Juni, 2023 Kamati iliwaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu Azimio hilo ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kikao mahsusi cha kupokea maoni kilichopangwa kufanyika katika ofisi ya Bunge tarehe 6 Juni, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, mara tu baada ya taarifa ya kuwaalika wadau kutolewa kumekuwepo na taarifa za upotoshaji kuhusiana na taarifa hiyo na Azimio husika. Hivyo nimeona nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi wa masuala yaliyojitokeza kama ifuatavyo: -

Mosi, pamoja na mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya wadau yaani *public hearing* uliofanyika siku ya jumanne tarehe 6 Juni, 2023 hapa Dodoma ambapo Kamati iliweza kupokea maoni ya wadau waliofika. Kamati ya pamoja bado inaendelea kupokea maoni ya wadau ambao hawakuweza kufika. Maoni ya wadau yanapokelewa kwa njia ya posta na barua pepe kupitia anuani zilizo ainishwa kwenye taarifa ya kuwaalika wadau kutoa maoni.

Pili, taarifa zilizotolewa na baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya jamii ikiwemo magazeti ya *The Guardian* na Nipashe ya tarehe 7 Juni, 2023 zikidai kwamba Azimio hilo limesharidhiwa na Bunge si za kweli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Azimio husika kwa sasa bado lipo katika ngazi ya Kamati ya pamoja kwa mujibu wa Kanuni, na mara baada ya Kamati kumaliza kazi yake Azimio hilo limepangwa kuingia Bungeni tarehe 10 Juni, 2023 kwa ajili ya mjadala na kupitishwa na Bunge.

Tatu, kwa mara nyingine tena tunatoa wito kwa waandishi wa habari na wana-mitandao kuzingatia maadili kwa kuhakikisha kwamba wanajiridhisha na kutuma taarifa sahihi kutoka kwa mamlaka zinazo husika kabla ya kutoa taarifa ili kuepusha taharuki na usumbufu kwa umma. Kitendo kilichofanywa na vyombo vya habari husika kwa maana ya Nipashe na *The Guardian* ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 34(1)(a) cha Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge ambacho kwa ujumla wake kinaeleza kwamba ni kosa kisheria kuchapisha habari za uongo au zinazolenga kwa namna yoyote ile kupotosha kwa makusudi jambo lolote linalo husu uendeshaji wa shughuli za Bunge na Kamati zake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kusema kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninarudia, nimalizie kwa kusema kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

litaendelea kuunga mkono Juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza uchumi na maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Bunge kupitia Kamati zake lipo tayari wakati wowote kupokea, kujadili na kutoa maoni yale ambayo wananchi wameyaleta kwetu yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nimeona nitoe ufafanuzi huo maana naona vyombo vya habari vinajiongeza kwenye orodha ya vyombo vya habari ambavyo havifanyi haki kwa Bunge. Hatupendi upotoshaji na tulishawaambia milango iko wazi kama ni lazima gazeti litoke piga simu kwa kiongozi akujibu, usiandike taarifa ya uongo. Na ninafikiri kwa sababu nimekuwa nikitoa tu maonyo hapa bila kuchukua hatua pengine sasa hili litakuwa ni onyo la mwisho kwa vyombo vya habari.

Chombo cha habari kitakachofanya upotoshaji tutashughulika nacho kwa mujibu wa taratibu zetu, kanuni zetu na sheria zetu ili tufike mahali ambapo kama ambavyo tumewafungulia milango kuuliza taarifa zozote mnazozitaka na sasa hivi Bunge liko wazi popote unaliona, sioni sababu ya chombo cha habari chochote kusema Bunge limepitisha Azimio wakati Bunge linakaa hapa na linaonekana kwa wananchi wote na wao hawajaiona hiyo taarifa halafu vyombo vya habari vinavyoheshimika vinaanza kuandika habari za upotoshaji haikubaliki; mnaleta taharuki kwa wananchi wakati sisi tunawategemea ninyi mwe wa kwanza kutoa taarifa sahihi kwa wananchi.

Kwa hiyo, nitoe wito na huo, na niseme kwa kweli hili litakuwa ni onyo la mwisho kwa vyombo vya habari vinavyofanya upotoshaji kwa taarifa zinazo husu Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023

*(Kusomwa Kwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene aje awasilishe hoja yake kuhusu muswada.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria wa Tume ya Mipango wa mwaka 2023 ambao uko mbele ya Bunge lako tukufu; napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuuboresha muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023 unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Mipango. Lengo la kutungwa kwa sheria hii ni kuanzisha Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais itakayokuwa na

jukumu la kubuni, kupanga, kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ili kuwa na mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Taifa, kuwa na utaratibu wa kupanga pamoja mipango ya kisekta hususan sekta zenye majukumu yanayotegemeana na kuwa na mfumo wa kisheria na chombo mahsusi cha kusimamia uandaaji, utekelezaji wa mipango ya maendeleo, utafiti na kuishauri Serikali kuhusu vipaumbele vya maendeleo ya Taifa. Majukumu haya kwa sasa yanatekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita; Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa, utaratibu wa kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza masharti kuhusu uanzishwaji wa Tume ya Mipango, muundo, mamlaka na majukumu ya Tume ya Mipango. Kwa mujibu wa sehemu hii, Tume ya Mipango itaongozwa na Rais kama Mwenyekiti na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais, akiwemo Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango ya maendeleo na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha. Aidha, inapendekezwa kuwepo na nafasi ya Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume watakaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Tume hii itakuwa chini ya Ofisi ya Rais, lengo la muundo unaopendekezwa ni kuhakikisha kuwa Tume inakuwa na uwezo wa kuratibu na kusimamia masuala yote ya mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kusimamia masuala ya ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi, sehemu hii inapendekeza kuipa Tume mamlaka ya kutoa miongozo, maelekezo na nyaraka mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu inahusu masuala ya utawala ambayo yanajumuisha uteuzi wa Katibu Mtendaji, Naibu Makatibu Watendaji na upatikanaji wa watumishi wengine wa Tume. Kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii, Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji watateuliwa na Rais kupitia mchakato wa ushindani. Hali kadhalika, watumishi wengine wa Tume pia watapatikana kwa utaratibu wa ushindani kwa kuzingatia vigezo vya weledi na uzoefu. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tume inapata watendaji na watumishi wenye ujuzi, weledi na waliobobea katika masuala ya mipango ya uchumi na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza masharti ya fedha ambayo yanajumuisha vyanzo vya fedha za Tume, utaratibu wa uwajibikaji wa matumizi ya fedha za Tume, uandaaji na ukaguzi wa hesabu za Tume ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa taarifa za utendaji wa Tume Bungeni.

Aidha, kama ambavyo muswada umeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kuwa vyanzo vikuu vya fedha za uendeshaji wa Tume vitokane na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kupitia bajeti ya kila mwaka na fedha za ruzuku. Vilevile kama ilivyo kwa taasisi nyingine za umma zinazoendeshwa kwa bajeti ya Serikali, hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada huu inaainisha masharti ya jumla ambayo ni mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kubainisha makosa na adhabu. Aidha, inapendekezwa Tume iwe na mamlaka ya kuitisha taarifa yoyote kutoka kwa mtu au taasisi yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 ili kuwianisha majukumu ya Tume yaliyoainishwa katika Sheria hiyo na yale yatakayoanishwa kwenye Sheria ya Tume ya Mipango, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134 kwa lengo la kuwajumuisha Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kwenye Kamati mbalimbali

zilizoanzishwa chini ya sheria hiyo; Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266 ili kuwawezesha Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kuapa mbele ya Rais.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023 na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA MIPANGO WA MWAKA 2023 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023 ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023 unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Mipango. Lengo la kutungwa kwa Sheria hii ni kuanzisha Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais itakayokuwa na jukumu la kubuni, kupanga, kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ili kuwa na mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Taifa, kuwa na utaratibu wa kupanga pamoja mipango ya kisekta, hususan, sekta zenye majukumu yanayotegemeana na kuwa na mfumo wa kisheria na chombo mahsusi cha kusimamia uandaaji, utekelezaji wa mipango ya maendeleo, utafiti na kuishauri Serikali kuhusu vipaumbele vya maendeleo ya Taifa. Majukumu haya kwa sasa yanatekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita.
Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa kutungwa, utaratibu wa kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza masharti kuhusu uanzishwaji wa Tume ya Mipango, muundo, mamlaka na majukumu ya Tume ya Mipango. Kwa mujibu wa Sehemu hii, Tume ya Mipango itaongozwa na Rais kama Mwenyekiti na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais, akiwemo Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango ya maendeleo na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Aidha, inapendekezwa kuwepo na nafasi ya Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume watakaoteuliwa na Rais. Tume hii itakuwa chini ya Ofisi ya Rais. Lengo la muundo unaopendekezwa ni kuhakikisha kuwa Tume inakuwa na uwezo wa kuratibu na kusimamia masuala yote ya mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kusimamia masuala ya ufuatiliaji na tathmini. Ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi, Sehemu hii inapendekeza kuipa Tume mamlaka ya kutoa miongozo, maelekezo na nyaraka mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu inahusu masuala ya utawala ambayo yanajumuisha uteuzi wa Katibu Mtendaji, Naibu Makatibu Watendaji na upatikanaji wa watumishi wengine wa Tume. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji watateuliwa na Rais kupitia mchakato wa ushindani. Hali kadhalika, watumishi wengine wa Tume pia watapatikana kwa utaratibu wa ushindani kwa kuzingatia vigezo vya weledi na uzoefu. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tume inapata watendaji na watumishi wenye ujuzi, weledi na waliobobea katika masuala ya mipango ya uchumi na maendeleo kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza masharti ya fedha ambayo yanajumuisha vyanzo vya fedha za Tume, utaratibu wa uwajibikaji wa matumizi ya fedha za Tume, uandaaji na ukaguzi wa hesabu za Tume ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa taarifa za utendaji wa Tume Bungeni. Aidha, kama ambavyo Muswada umeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kuwa vyanzo vikuu vya fedha za uendeshaji wa Tume vitokane na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kupitia bajeti ya kila mwaka na fedha za ruzuku. Vilevile, kama ilivyo kwa taasisi nyingine za umma zinazoendeshwa kwa bajeti ya Serikali, hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada huu inaainisha masharti ya jumla ambayo ni mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kubainisha makosa na adhabu. Aidha, inapendekezwa Tume iwe na mamlaka ya kuitisha taarifa yoyote kutoka kwa mtu au taasisi yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 ili kuwianisha majukumu ya Tume yaliyoainishwa katika Sheria hiyo na yale yatakayoainishwa kwenye Sheria ya Tume ya Mipango, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134 kwa lengo la kuwajumuisha Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kwenye Kamati mbalimbali zilizoanzishwa chini ya Sheria hiyo, Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266 ili

kuwawezesha Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kuapa mbele ya Rais.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023 na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA.

George B. Simbachawene (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,**
**(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)**
...07.../.06 /2023

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria aje awasilishe maoni ya Kamati. kWa niaba yake Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hajaanza kusoma niwaombe sana na kwa sababu tunaelekea kwenye kutunga Sheria tatu muhimu sana. Wale ambao wana mjadala wa muhimu kabisa unao husu hoja zinazoendelea kwenye Kamati na mambo kama hayo ya kushauriana wanaruhusiwa kwenda kushauriana hapo nje kuliko kushauriana mkiwa humu ndani Wabunge wengine hawasikii kile kinachosemwa hapa; na muhimu wote tukisikie tukielewe ili tunapoingia kutunga Sheria tujue tunatunga kuhusu jambo gani.

Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za

Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa niaba ya Mwenyekiti wangu Dkt. Joseph Mhagama kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Kikao cha Ishirini na Nane cha Mkutano wa Kumi na Moja, tarehe 18 Mei, 2023 kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 96(1). Aidha, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14), ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ili ufanyiwe uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 25 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika mkutano wa maoni *(public hearing)* uliofanyika tarehe 27 Mei, 2023 ili kutimiza Masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za kudumu za Bunge. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea maoni kutoka Chuo cha Mipango, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Wadau wengine mbalimbali. Kamati inawashukuru kwa dhati wadau hao kwa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yameisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria wa Tume ya Mipango wa mwaka 2023 ulifanyiwa uchambuzi na Kamati kwa kuhakiki na kufanya upembuzi wa maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Kamati pia ilifanya rejea ya muundo wa Tume za Mipango katika nchi mbalimbali ikiwemo Zanzibar, Ghana, Indonesia, Afrika ya Kusini na India ambako Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ni Rais wa Nchi. Lengo lilikuwa ni kupata ufahamu kuhusu miundo mbalimbali ya Tume za Mipango, ufanisi wake na changamoto kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kushauriana na Serikali ilifanya tathmini ya changamoto zilizojitokeza tangu kufutwa kwa Tume ya Mipango mwaka 2018 iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango Sura ya 314 na jukumu hilo kuhamishiwa Wizara ya Fedha na Mipango. Kamati ilibaini kuwa kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa upangaji, usimamizi na ufuatiliaji thabiti wa mipango ya nchi. Changamoto hii inatokana na Wizara ya fedha kushughulika kwa kiasi kikubwa na masuala ya fedha na kutoa nafasi finyu upande unaohusu mipango ya ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Tume hii pia kutasaidia kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayotekelezwa katika kipindi cha Dira ya Taifa ya Maendeleo inayomalizika mwaka 2025 na kuandaa mipango mipya itakayojumuishwa katika Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 – 2050. Kwa sababu hizi, Kamati imejiridhisha kuwa Muswada huu umeletwa wakati muafaka na ikiwa utaridhiwa na Bunge lako Tukufu utawezesha Serikali kuunda chombo mahsusi kitakachoshughulika na masuala ya mipango na kutatua changamoto zilizojitokeza wakati jukumu hili linatekelezwa na Wizara yenye dhamana na fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii, Kamati inaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi thabiti na maono makubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuuleta Muswada huu wakati muafaka ili kuiwezesha nchi kuwa na mipango endelevu itakayochochea kukua kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Muswada huu yamejikita katika kuanzisha Tume ya Mipango kama idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais. Tume hii itaundwa na Wajumbe saba chini ya Uenyekiti wa Rais. Jukumu la msingi la Tume litakuwa kusimamia uchumi, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Muswada unakusudia kuipa Tume mamlaka ya juu nchini katika masuala ya mipango ya maendeleo. Pamoja na mamlaka mengine Tume itakuwa na mamlaka yafuatayo:-

(a) Kubaini na kuidhinisha maeneo ya vipaumbele vya maendeleo ya Taifa na kutoa maelekezo ya kujumuishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa na sekta;

(b) Kutoa maelekezo na miongozo kwa taasisi zote za umma kuhusu masuala ya mipango na uchumi na maendeleo;

(c) Kuitisha takwimu zinazohusiana na masuala ya Mipango ya Maendeleo na usimamizi wake; na

(d) Kutoa maelekezo na miongozo muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora na wenye ufanisi wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia unakusudia kufanya marekebisho katika sheria nyingine ili kuondoa mgongano baina ya masharti ya sheria zinazorekebishwa na Sheria mpya ya Tume inayopendekezwa kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kuhusu Ibara za Muswada: Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inaanzia Ibara ya 1 hadi Ibara ya 3. Kwa ujumla Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada katika Ibara hizo. Ibara ya 1 ya Muswada inataja jina la Sheria inayopendekezwa kuwa ni Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Muswada, Kamati iliridhika na Jina la Sheria inayopendekezwa kwa kuwa linaakisi maudhui ya sheria inayopendekezwa. Aidha, Ibara ya 2 ya Muswada inaeleza mawanda ya matumizi ya sheria inayopendekezwa kuwa mipaka ya matumizi yake ni Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 imetoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada na kwa kiasi kikubwa ilikubaliana na mapendekezo ya Muswada isipokuwa kwa tafsiri

ya neno moja tu ambalo ni Mipango Mikakati. Kamati ilipata shaka na tafsiri ya maneno hayo kwa kuwa hayajatumika katika Muswada, na kupendekeza maneno Mpango Mkakati ndio yatafsiriwe kwa kuwa ndio yaliyotumika katika Muswada. Pendekezo hilo lilikubaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu Tume ya Mipango. Ibara ya 4, 5, 6 na 7 ya Sehemu hii zinaweka masharti ya uanzishwaji wa Tume, Muundo wa Tume, Majukumu ya Tume na Mamlaka ya Tume mtawalia ambayo maudhui yake yameelezwa hapo awali katika kipengele cha maudhui ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa sehemu hii, Kamati ilibaini kuwa Ibara ya 5(1)(c) ya Muswada haijaweka bayana masharti ya uteuzi wa mjumbe kutoka sekta binafsi katika uteuzi wa wajumbe wengine wanne wa Tume ili kuendana na sera ya nchi kuwa na ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Baada ya majadiliano na Serikali, ilionekana Ibara hii ibaki kama ilivyopendekezwa kwa kuwa uteuzi wa wajumbe umewekewa sifa za kitaalam na uzoefu katika Ibara ya 5(3) ya Muswada. Aidha, Tume pia imepewa mamlaka ya kumwalika mtu yeyote kushiriki vikao vya Tume na kutoa utaalam wake kadri Tume itakavyoona inafaa. Kamati inashauri katika kutekeleza Ibara hii, uteuzi wa mjumbe kutoka sekta binafsi uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu Ibara ya 6(1) ya Muswada umebaini kuwa maneno "katika mfumo husika" yanayosomeka mwishoni mwa Ibara hiyo yana utata ukilinganisha na maudhui ya Ibara hiyo na kupendekeza maneno hayo yaondolewe. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 imeeleza majukumu ya Tume. Kwa kurejea historia ya Tume na majukumu yake inayokusudia kuyatekeleza, Kamati ilipendekeza sheria inayopendekezwa iweke ulinzi wa mipango ya maendeleo itakayoandaliwa na Tume ili iweze kubadilishwa tu pale kunapotokea ulazima kwa lengo la kuiboresha. Kutokana na mapendekezo hayo, Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8, 9 na 10 za Muswada maudhui yake yanahusu mwenendo wa Tume kwa ujumla. Kamati ilifanya uchambuzi wa Ibara hizo na kwa kiasi kikubwa inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa maneno ya pembeni (*marginal notes*) ya Ibara ya 8 yanayosomeka "Mwenendo wa Tume" na kuweka maneno fasaha yanayoakisi maudhui ya Ibara hiyo. Mapendekezo hayo yalikubaliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipendekeza Ibara itaje idadi ya chini ya vikao vya Tume kwa mwaka kuwa angalau vinne kama ilivyo kwenye sheria mbalimbali zenye Bodi au Tume. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Serikali, ilikubalika Ibara ibaki kama ilivyopendekezwa katika Muswada ili kuwezesha Tume kuwa na vikao kulingana na mahitaji ya wakati husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka Masharti ya Utawala na inaanzia Ibara ya 11 mpaka Ibara ya 15. Maudhui ya Ibara hizi yanaeleza kuwa Tume ya Mipango itakuwa ni taasisi ya Umma inayofanya kazi zake kwa misingi ya Kiserikali chini ya utendaji wa kila siku wa Mtendaji Mkuu wa Tume. Mtendaji Mkuu atasaidiwa na Naibu Watendaji Wakuu na Sekretarieti. Mtendaji Mkuu na Sekretarieti yake watapatikana kwa njia ya ushindani kwa utaratibu ulioainishwa katika Ibara za 11, 12, 13 na 14(2) za Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Ibara ya 12 ya Muswada, Kamati ilibaini kuwa Ibara haijaeleza idadi na sifa za Naibu Makatibu Watendaji wa Tume wanaokusudiwa kuteuliwa. Kamati ilipendekeza Ibara iboreshwe kwa kuweka idadi ya Naibu Makatibu Watendaji pamoja na kuainisha sifa zao kwa lengo la kuweka uwazi katika mchakato wa uteuzi na kupata watendaji wenye sifa stahiki. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na hoja pia katika Ibara ya 15 ya Muswada inayokusudia kuweka Masharti ya Tume kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kuanzisha jukwaa la mashauriano. Kamati ilipendekeza kuondoa wajibu wa Tume kushauriana na Waziri wa Fedha katika kuanzisha

jukwaa la mashauriano ili kumpatia Waziri wa Fedha nafasi ya kutosha katika masuala ya fedha. Aidha, Kamati ina maoni kuwa maudhui ya masharti haya yamezingatiwa katika Ibara ya 5(1) ya Muswada kwa kuwa Waziri wa Fedha ni mojawapo wa Wajumbe wa Tume ya Mipango. Baada ya majadiliano na Serikali ilikubalika Ibara iboreshwe ili kuakisi na kuleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, inakusudia kuweka masharti yanayohusu masuala fedha na inaanzia Ibara ya 16 hadi Ibara ya 21. Kwa kiasi kikubwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya masharti ya ibara hizi. Hata hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa vyanzo vya fedha katika Ibara ya 16(1)(b) na (c) inayoeleza kuwa mojawapo ya vyanzo vya fedha vya Tume ni misaada, michango, zawadi na mapato mengine yatakayotokana na utekelezaji wa majukumu ya Tume chini ya Sheria hii. Kamati ilipendekeza vyanzo hivi viondolewe kwa hofu kuwa Tume itaanza kujikita katika kutafuta misaada, michango na fedha za taasisi badala ya kujikita katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya kuandaa, kusimamia na kufuatilia mipango ya maendeleo. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipendekeza kuboreshwa kwa ya Ibara ya 21 kwa kuondoa maneno ya pembeni; "na mikataba ya utendaji" yanayopatikana baada ya maneno; "Taarifa za mwaka" kwa kuwa maneno hayo hayaakisi katika maudhui ya Ibara hiyo. Serikali ilikubaliana na pendekezo hilo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inaweka Masharti ya Jumla kuhusu Muswada na inaanzia Ibara ya 22 hadi Ibara ya 26. Ibara hizi zinakusudia kuweka masharti kuhusu mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni, Kuweka kiapo rasmi kwa Wajumbe wa Tume na Watendaji Wakuu wa Tume, Mamlaka ya Tume kupata taarifa, wajibu wa Tume kushirikiana na mamlaka nyingine na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti ya sheria inayopendekezwa mtawalia. Kwa ujumla Kamati ilikubaliana na mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita inaanzia Ibara ya 27 hadi Ibara ya 34 na inaweka Masharti ya Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali ili kuweka ufanisi wa utekelezaji wa Sheria hizo na Sheria ya Tume ya Mipango inayopendekezwa. Ufafanuzi wa Sheria zinazorekebishwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

(b) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134.

(c) Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati; Tume imepewa mamlaka ya kuwa chombo cha juu cha kiserikali katika kushauri kuhusu masuala yote ya mipango ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu kwa Wizara na Taasisi zote za Umma kuhusu mamlaka ya Tume katika kuandaa, kusimamia na kutoa miongozo ya mipango ya maendeleo. Hii itasaidia kufungamanisha mipango inayoandaliwa na taasisi hizo na ile inayoandaliwa na Tume ili kuwianisha mipango ya kisekta katika mamlaka hizo na mipango ya Tume. Aidha, elimu kwa umma itawezesha wadau wote kushiriki katika kuiwezesha Tume kwa kuipatia taarifa zitakazowezesha uandaaji na ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maboresho ya sera; uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo unategemea sera zenye uhai na uhalisia. Kumalizika kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa Mwaka 2025 kunaashiria kubadilishwa kwa sera mbalimbali ili ziendane na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 - 2050. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri sera mbalimbali zichambuliwe na kuangaliwa upya ili ziendane na Mipango na Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa kwa niaba ya Mwenyekiti, niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao wametajwa na naomba majina yao yasomeke katika *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa

kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Ridhiwani J. Kikwete, Naibu Waziri wa Wizara hiyo; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, – Ikulu, Ndugu Moses M. Kusiluka; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndugu Onorius Njole; pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati. Tutakumbuka mapendekezo mengi ya Kamati yalikubaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndugu Frank Nkya, Ndugu Praisegod Lukio, Ndugu Ganjatuni Kilemile, Ndugu Ludovick Ringia, Ndugu Rabeca Balisidya, Ndugu Nesta Kawamala, Ndugu Evelyene Shibandiko wakisaidiwa na Ndugu Theresia Jacob. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msimamo wa Kamati kuhusu hoja; baada ya kusema hayo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2023 pamoja na Marekebisho yake kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**8 JUNI, 2023**

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA MIPANGO WA MWAKA 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu **Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023.**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Kikao cha Ishirini na Nane cha Mkutano wa Kumi na Moja, tarehe 18 Mei, 2023 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 96 (1)**. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 136 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ili ufanyiwe uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Muswada huu ni utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 25 Mei, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa maoni *(Public Hearing)* uliofanyika tarehe 27 Mei, 2023 ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano

huo, Kamati ilipokea maoni kutoka Chuo cha Mipango, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (***LHRC***) na Wadau wengine mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawashukuru kwa dhati wadau hao kwa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yameisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu. Baada ya maoni ya wadau, tarehe 31 Mei, 2023 Kamati ilifanya majumuisho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Ibara za Muswada kwa lengo la kupata ufafanuzi katika Ibara hizo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria wa Tume ya Mipango wa Mwaka 2023 ulifanyiwa uchambuzi na Kamati kwa kuhakiki na kufanya upembuzi wa maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Kamati pia ilifanya rejea ya muundo wa Tume za Mipango katika nchi mbalimbali ikiwemo Zanzibar, Ghana, Indonesia, Afrika ya Kusini na India ambako Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ni Rais wa nchi. Lengo lilikuwa ni kupata ufahamu kuhusu miundo mbalimbali ya Tume za Mipango, ufanisi wake na changamoto kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa kushauriana na Serikali ilifanya tathmini ya changamoto zilizojitokeza tangu kufutwa kwa Tume ya Mipango mwaka 2018 iliyokuwa ikiundwa kwa mujibu wa **Sheria ya Tume ya Mipango Sura ya 314** na jukumu hilo kuhamishiwa wizara ya fedha na mipango. Kamati ilibaini kuwa kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa upangaji, usimamizi na ufuatiliaji thabiti wa mipango ya nchi. Changamoto hii inatokana na Wizara ya fedha kushughulika kwa kiasi kikubwa na masuala ya fedha na kutoa nafasi finyu upande unaohusu mipango ya yaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya rejea katika Ilani ya Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi (**CCM**) ya Mwaka 2020-2025 kuhusu mipango ya maendeleo na kubaini kwamba, Ilani hiyo inatoa maagizo kwa Serikali ya kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka 25. **Kipengele Na. 8** cha Masharti ya Utangulizi ya Ilani kinaeleza kuwa; nanukuu

"***CCM inatambua kwamba utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo utafikia kikomo chake katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii (yaani 2025). Hivyo, Chama kitazisimamia Serikali zake kuandaa Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2050, na kuanza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 - 2050***".

**Mheshimiwa Spika,** kuundwa kwa Tume hii pia kutasaidia kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayotekelezwa katika kipindi cha Dira ya Taifa ya Maendeleo inayomalizika mwaka 2025 na kuandaa mipango mipya itakayojumuishwa katika Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025-2050. Kwa sababu hizi, Kamati imejiridhisha kuwa Muswada huu umeletwa wakati muafaka na ikiwa utaridhiwa na Bunge lako utawezesha Serikali kuunda chombo mahsusi kitakachoshughulika na masuala ya mipango na kutatua changamoto zilizojitokeza wakati jukumu hili linatekelezwa na wizara yenye dhamana na fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sababu hii, Kamati inaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi thabiti na maono makubwa ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuuleta Muswada huu wakati muafaka ili kuiwezesha nchi kuwa na mipango endelevu itakayochochea kukua kwa maendeleo ya taifa.

### 2.2 Upembuzi wa Maudhui

**Mheshimiwa Spika,** Maudhui ya Muswada huu yamejikita katika kuanzisha Tume ya Mipango kama idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais. Tume hii itaundwa na wajumbe saba (7) chini ya Uenyekiti wa Rais. Jukumu la msingi la Tume litakuwa kusimamia uchumi, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya

maendeleo ya taifa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza wajibu huu, Tume itatekeleza kazi mbalimbali mahsusi ikiwemo: -

(a) Kutathmini hali ya rasilimali za taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya rasilimali hizo;

(b) Kuandaa dira ya maendeleo ya taifa na mpango wa maendeleo wa muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi na kusimamia utekelezaji wake;

(c) Kupendekeza maeneo ya miradi endelevu ya kielelezo na mikakati ya utekelezaji wake;

(d) Kutathmini sera mbalimbali zilizopo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya taifa na kupendekeza sera mpya pale inapoonekana inafaa; na

(e) Kufuatilia utekelezaji wa maeneo muhimu ya vipaumbele vya taifa katika sekta mbalimbali za uchumi na kuchukua hatua stahiki za kutatua changamoto zozote zitakazobainika katika sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza majukumu haya, Muswada unakusudia kuipa Tume mamlaka ya juu nchini katika masuala ya mipango ya maendeleo. Pamoja na mamlaka mengine, Tume itakuwa na mamlaka yafuatayo:-

(a) Kubaini na kuidhinisha maeneo ya vipaumbele vya maendeleo ya taifa na kutoa maelekezo ya kujumishwa katika mipango ya maendeleo ya taifa na sekta;

(b) Kutoa maelekezo na miongozo kwa taasisi zote za umma kuhusu masuala ya mipango na uchumi na maendeleo;

(c) Kuitisha takwimu zinazohusiana na masuala ya mipango ya maendeleo na usimamizi wake; na

(d) Kutoa maelekezo na miongozo muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora na wenye ufanisi wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada pia unakusudia kufanya marekebisho katika sheria nyingine ili kuondoa mgongano baina ya masharti ya Sheria zinazorekebishwa na Sheria mpya ya Tume inayopendekezwa kuanzishwa.

**2.3 Uchambuzi Kuhusu Ibara za Muswada**

**2.3.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inaanzia **Ibara ya 1** hadi **Ibara ya 3**. Kwa ujumla Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada katika Ibara hizo.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 1** ya Muswada inataja jina la Sheria inayopendekezwa kuwa ni **Sheria ya Tume ya Mipango ya Mwaka 2023**, na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atatangaza kupitia notisi kwenye Gazeti la Serikali. Jina hili fupi la Muswada linatolewa ufafanuzi wa ziada na Jina Refu (***long title***) linaloeleza kuwa "***Sheria ya kuanzisha Tume ya Mipango, kubainisha wajumbe wake na kuanisha majukumu na mamlaka yake; na kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo***".

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Muswada, kamati iliridhika na Jina la Sheria inayopendekezwa kwa kuwa lina akisi maudhui ya sheria inayopendekezwa. Aidha, **Ibara ya 2** ya Muswada inaeleza mawanda ya matumizi ya sheria inayopendekezwa kuwa mipaka ya matumizi yake ni Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3** imetoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada na kwa kiasi kikubwa ilikubaliana na mapendekezo ya Muswada isipokuwa kwa tafsiri ya neno moja tu ambalo ni **Mipango mkakati**. Kamati ilipata shaka na tafsiri ya maneno hayo kwa kuwa hayajatumika katika Muswada, na kupendekeza maneno **mpango mkakati** ndio

yatafsiriwe kwa kuwa ndio yaliyotumika katika Muswada. Pendekezo hilo lilikubaliwa na Serikali.

**2.3.2 Sehemu ya Pili ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya Muswada inaweka Masharti kuhusu Tume ya Mipango. **Ibara ya 4, 5, 6 na 7** ya Sehemu hii zinaweka Masharti ya uanzishwaji wa Tume, Muundo wa Tume, Majukumu ya Tume na Mamlaka ya Tume mtawalia ambayo maudhui yake yameelezwa hapo awali katika kipengele cha maudhui ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa sehemu hii, Kamati ilibaini kuwa **Ibara ya 5(1)(c) ya Muswada** haijaweka bayana masharti ya uteuzi wa mjumbe kutoka sekta binafsi katika uteuzi wa wajumbe wengine wanne wa Tume ili kuendana na sera ya nchi kuwa na ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Baada ya majadiliano na Serikali, ilionekana Ibara ibaki kama ilivyo pendekezwa kwa kuwa uteuzi wa wajumbe umewekewa sifa za kitaalam na uzoefu katika Ibara ya **5(3) ya Muswada**. Aidha, Kamati pia imepewa mamlaka ya kumualika mtu yeyote kushiriki vikao vya Tume na kutoa utaalamu wake kadri Tume itakavyoona inafaa. Kamati inashauri katika kutekeleza Ibara hii, uteuzi wa mjumbe kutoka sekta binafsi uzingatiwe.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu **Ibara ya 6(1)** ya Muswada umebaini kuwa maneno "**katika mfumo husika"** yanayosomeka mwishoni mwa Ibara hiyo yana utata ukilinganisha na maudhui ya Ibara hiyo na kupendekeza maneno hayo yaondolewe. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6** imeeleza majukumu ya Tume. Kwa kurejea historia ya Tume na majukumu yake inayokusudia kuyatekeleza, kamati ilipendekeza sheria inayopendekezwa iweke ulinzi wa mipango ya maendeleo itakayoandaliwa na Tume ili iweze kubadilishwa tu pale kunapotokea ulazima kwa lengo la kuiboresha. Kutokana na mapendekezo hayo, Serikali imekubaliana na Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8, 9 na 10 za Muswada** maudhui yake yanahusu mwenendo wa Tume kwa ujumla. Kamati ilifanya uchambuzi wa Ibara hizo na kwa kiasi kikubwa inakubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa maneno ya pembeni (***marginal notes***) ya **Ibara ya 8** yanayomeka "***Mwenendo wa Tume***" na kuweka maneno fasaha yanayoakisi maudhui ya Ibara hiyo. Mapendekezo hayo yalikubaliwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pia kamati ilipendekeza Ibara itaje idadi ya chini ya vikao vya Tume kwa mwaka kuwa angalau vinne kama ilivyo kwenye Sheria mbalimbali zenye Bodi au Tume. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Serikali, ilikubalika Ibara ibaki kama ilivyopendekezwa katika muswada ili kuwezesha Tume kuwa na vikao kulingana na mahitaji ya wakati husika.

**2.3.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka Masharti ya Utawala na inaanzia **Ibara ya 11** hadi **Ibara ya 15**. Maudhui ya Ibara hizi yanaeleza kuwa Tume ya Mipango itakuwa ni taasisi ya Umma inayofanya kazi zake kwa misingi ya Kiserikali chini ya utendaji wa kila siku wa Mtendaji Mkuu wa Tume. Mtendaji Mkuu atasaidiwa na Naibu Watendaji Wakuu na Sekretarieti. Mtendaji Mkuu na secretarieti yake watapatikana kwa njia ya ushindani kwa utaratibu ulioanishwa katika Ibara ya **11, 12, 13 na 14 (2)** ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchambua **Ibara ya 12 ya Muswada** Kamati ilibaini kuwa Ibara haijaeleza idadi na sifa za Naibu Makatibu Watendaji wa Tume wanaokusudiwa kuteuliwa. Kamati ilipendekeza Ibara iboreshwe kwa kuweka idadi ya Naibu Makatibu Watendaji pamoja na kuaninisha sifa zao kwa lengo la kuweka uwazi katika mchakato wa uteuzi na kupata watendaji wenye sifa stahiki. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na hoja pia katika **Ibara ya 15 ya Muswada** inayokusudia kuweka Masharti ya Tume kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha

kuanzisha jukwaa la mashauriano. Kamati ilipendekeza kuondoa wajibu wa Tume "***kushauriana na Waziri wa fedha"*** katika kuanzisha jukwaa la mashauriano ili kumpatia Waziri wa fedha nafasi ya kutosha katika masuala ya fedha. Aidha, Kamati ina maoni kuwa maudhui ya masharti haya yamezingatiwa katika **Ibara ya 5 (1)** ya Muswada kwa kuwa Waziri wa fedha ni mojawapo wa wajumbe wa Tume ya Mipango. Baada ya majadiliano na Serikali ilikubalika Ibara iboreshwe ili kuakisi na kuleta maana iliyokusudiwa.

**2.3.4 Sehemu ya Nne ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kuweka Masharti yanayohusu masuala Fedha na inaanzia **Ibara ya 16** hadi **Ibara ya 21**. Kwa kiasi kikubwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya masharti ya Ibara hizi. Hata hivyo, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa vyanzo vya fedha katika **Ibara ya 16 (1) (b) na (c)** inayoeleza kuwa mojawapo ya vyanzo vya fedha vya Tume ni "***misaada, michango, zawadi na mapato mengine yatakayotokana na utekelezaji wa majukumu ya Tume chini ya Sheria hii***". Kamati ilipendekeza vyanzo hivi viondolewe kwa hofu kuwa Tume itaanza kujikita katika kutafuta misaada, michango na fedha za taasisi badala ya kujikita katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya kuandaa, kusimamia na kufuatilia mipango ya maendeleo. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipendekeza kuboreshwa kwa ya **Ibara ya 21** kwa kuondoa maneno ya pembeni "***na mikataba ya utendaji***" yanayopatikana baada ya maneno "***Taarifa za mwaka***" kwa kuwa maneno hayo hayaakisi katika maudhui ya Ibara hiyo. Serikali ilikubaliana na pendekezo hilo kwa kuondoa maneno hayo.

**2.3.5 Sehemu ya Tano ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inaweka Masharti ya Jumla kuhusu Muswada na inaanzia **Ibara ya 22** hadi **Ibara ya 26**. Ibara hizi zinakusudia kuweka masharti kuhusu Mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni, Kuweka kiapo rasmi kwa wajumbe wa

Tumen a watendaji wakuu wa Tume, Mamlaka ya Tume kupata taarifa, Wajibu wa Tume kushirikiana na mamlaka nyingine na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti ya Sheria inayopendekezwa mtawalia. Kwa ujumla Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Ibara zote za sehemu hii.

### 2.3.6 Sehemu ya Sita ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaanzia **Ibara ya 27** hadi **Ibara ya 34** na inaweka Masharti ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ili kuweka ufanisi wa utekelezaji wa Sheria hizo na sheria ya Tume ya Mipango inayopendekezwa. Ufafanuzi wa Sheria zinazorekebishwa ni kama ifuatavyo:-

**(a) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439**. Maudhui ya Marekebisho ya Sheria hii yanakusudia kurekebisha Kifungu cha 11(a) cha Sheria ya Bajeti kwa kumuondolea Waziri mamlaka ya kuandaa Mipango ya maendeleo na kupewa jukumu la kuratibu uandaaji wa Mipango kwa kuwa jukumu la kuandaa mipango linakusudiwa kutekelezwa na Tume.

**(b) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134**. Maudhui ya Marekebisho yanakusudia kumuondolea aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji kuwa mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Mikopo, Dhama na Misaada, badala yake Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Mipango na Katibu Mtendaji wa Tume kuwa wajumbe wa Kamati hiyo.

**(c) Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266**. Maudhui ya Marekebisho haya yanakusudia kuwajumuisha Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume ya Mipango kuapa mbele ya Rais baada ya kuteuliwa kushikilia madaraka.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 Elimu kwa Taasisi za Serikali na Umma

**Mheshimiwa Spika,** Tume imepewa mamlaka ya kuwa chombo cha juu cha kiserikali katika kushauri kuhusu masuala yote ya mipango ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu kwa Wizara na taasisi zote za umma kuhusu mamlaka ya Tume katika kuandaa, kusimamia na kutoa miongozo ya mipango ya maendeleo. Hii itasaidia kufungamanisha Mipango inayoandaliwa na taasisi hizo na ile inayoandaliwa na Tume ili kuwianisha mipango ya kisekta katika mamlaka hizo na mipango ya Tume. Aidha, elimu kwa umma itawezesha wadau wote kushiriki katika kuiwezesha Tume kwa kuipatia taarifa zitakazowezesha uandaaji na ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo.

### 3.2 Maboresho ya Sera mbalimbali

**Mheshimiwa Spika,** uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo unategemea sera zenye uhai na uhalisia. Kumalizika kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa Mwaka 2025 kunaashiria kubadilishwa kwa sera mbalimbali ili ziendane na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025-2050. Kwa sababu hiyo, kamati inashauri sera mbalimbali zichambuliwe na kuangaliwa upya ili ziendane na mipango na Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya

Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama, Mb. | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. | Makamu |
| 3. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani J. Kikwete (Mb, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Ikulu, Ndg. Moses M. Kusiluka, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio, Ndg. Ganjatuni Kilemile, Ndg. Ludovick Ringia, Ndg. Rabeca Balisidya, Ndg. Nesta Kawamala, Ndg. Evelyene Shibandiko wakisaidiwa na Ndg. Theresia Jacob.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023** pamoja Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria**
08 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa taarifa hiyo. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite tena Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**8 JUNI, 2023**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI.**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa kwa mwaka 2023 (*The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendments) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Kwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, aje awasilishe Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa tena kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa ya Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence Security Service (Amendment) Act 2023)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Kamati ya kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Frolent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii wamefanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuuboresha. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na kuwasilisha Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka, 2023 *(The*

*Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Act, 2023)* kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika sheria hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa na masharti kuhusu namna ambavyo vifungu mbalimbali vya sheria hii vimefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada huu inapendekeza marekebisho katika vifungu mbalimbali vya sheria ili kuifanya Idara katika kutekeleza majukumu yake kuwajibika moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na mabadiliko ya muundo wa sasa ambapo Idara hiyo inawajibika moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais. Mapendekezo haya yamezingatia pia asili na utaratibu wa utendaji kazi wa idara za usalama duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mabadiliko haya ya jumla ya kuiweka Idara chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Mheshimiwa Rais, inapendekezwa kurekebisha vifungu vya 8, 11, 15, 18 na 19(3) ili kuoanisha masharti ya vifungu hivyo na mfumo wa uwajibikaji wa Idara unaopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kifungu cha 4 cha Sheria kifanyiwe marekebisho ili kuipa Idara hadhi ya Chombo cha Ulinzi na Usalama chini ya Mheshimwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kutambua jukumu ambalo Idara imekuwa ikitekeleza kama mojawapo ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini. Inapendekezwa sheria ifanyiwe marekebisho katika Kifungu cha (5) kwa lengo la kuyapa nguvu ya kisheria majukumu ya msingi na muhimu ya usalama ambayo kwa sasa yanatekelezwa na Idara lakini hayatambuliwi na Sheria. Majukumu hayo ni pamoja na ulinzi binafsi wa Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa, ulinzi wa vituo muhimu, mamlaka ya upekuzi wa kiusalama wa viongozi na udhibiti wa matishio ya kiusalama dhidi ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa Kifungu cha (6) cha Sheria kifanyiwe marekebisho ili kuweka sifa za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na kuainisha masharti kuhusu nafasi hiyo baada ya utumishi. Lengo la marekebisho haya ni kupata mtendaji mwenye uwezo, sifa, weledi na kulinda maslahi ya kiusalama kwa watu ambao wamewahi kutumikia nafasi ya Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuboresha utendaji kazi wa Idara, inapendekezwa kuongeza vifungu vipya vya 6(A) na 6(B) katika Sheria ili kuweka masharti kuhusu nafasi za Naibu Wakurugenzi Wakuu kwa Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na nafasi ya Wakurugenzi wengine katika Idara watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais. Vilevile, inapendekezwa kuainisha masharti kuhusu sifa za uteuzi katika nafasi hizo tajwa.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha saba cha Sheria ili kuainisha masharti kuhusu vigezo vya ajira kwa watumishi wa Idara. Marekebisho haya pia yanaweka sharti la matumizi ya silaha wakati wa kutekeleza wa majukumu ya watumishi wa Idara kwa lengo la kutambua matumizi ya silaha na kuweka utaratibu wa nidhamu ya umiliki na matumizi ya silaha hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii pia inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 10 cha Sheria hii ili kumtambua Mkurugenzi Mkuu kama Mshauri Mkuu wa Rais na Serikali katika masuala ya Usalama wa Taifa. Lengo ni kutambua wajibu wa Idara katika usimamizi na udhibiti wa Usalama wa Taifa. Aidha, kwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Idara, Sheria inarekebishwa kwa kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya nidhamu kwa watumishi walio chini yake. Hali kadhalika, Kifungu cha 13 kinarekebishwa ili kuainisha utaratibu wa kuapishwa kwa Mkurugenzi Mkuu, Naibu Wakurugenzi Wakuu, Wakurugenzi na Maafisa wa Idara.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya udhibiti wa utambulisho wa Maafisa na watu wengine wanaoshirikiana na Idara. Lengo la marekebisho haya ni kuwalinda Maafisa na watu hao kutokana na utendaji wao wa kazi za kiusalama. Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza kinga dhidi ya mashtaka kwa Maafisa wa Idara wanapotekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, tofauti na ilivyo sasa ambapo kinga inahusu tu mashauri ya madai dhidi ya Maafisa hao. Lengo la marekebisho haya ni kuweka kinga dhidi ya makosa yanayoweza kutendeka wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 16(3), 17(3), 20(2) na 23 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali kutegemeana na uzito wa kosa.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa viwango hivyo vya adhabu vinaendana na mazingira ya sasa. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 24, 25 na 26 vitakavyoainisha masharti mbalimbali, ikiwemo udhibiti wa Maafisa kutoa taarifa za kiusalama pindi wanapostaafu au kumaliza vipindi vya ajira, kuzuia uingiaji katika maeneo ya Idara bila idhini na masharti kuhusu vitendo vya uvunjifu wa sheria nje ya mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Sheria linalopendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiapo cha utii pamoja na kurekebisha kiapo cha utumishi na kutunza siri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge la Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka, 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Act, 2023)* na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

8 JUNI, 2023

# HOTUBA YA MHESHIMIWA GEORGE B. SIMBACHAWENE, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA IDARA YA USALAMA WA TAIFA WA MWAKA 2023 (THE TANZANIA INTELLIGENCE AND SECURITY SERVICE (AMENDMENT) ACT, 2023) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

**Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka, 2023 (The Tanzania Intelligence and Security Service *(Amendment)* Act, 2023).

**Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuuboresha. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na kuwasilisha Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka, 2023 (The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Act, 2023) kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria hiyo kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa na masharti kuhusu namna ambavyo vifungu mbalimbali vya Sheria hii vimefanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada huu inapendekeza marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria ili kuifanya Idara katika kutekeleza majukumu yake kuwajibika moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na mabadiliko ya muundo wa sasa ambapo Idara hiyo inawajibika moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais. Mapendekezo haya yamezingatia pia asili na utaratibu wa utendaji kazi wa idara za usalama duniani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mabadiliko haya ya jumla ya kuiweka Idara chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Mheshimiwa Rais, inapendekezwa kurekebisha vifungu vya 8, 11, 15, 18 na 19(3) ili kuoanisha masharti ya vifungu hivyo na mfumo wa uwajibikaji wa Idara unaopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika,** inapendekezwa kifungu cha 4 cha Sheria kifanyiwe marekebisho ili kuipa Idara hadhi ya Chombo cha Ulinzi na Usalama chini ya Mheshimwa Rais. Lengo la marekebisho hayo ni kutambua jukumu ambalo Idara imekuwa ikitekeleza kama mojawapo ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama Nchini. Inapendekezwa sheria ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 5 kwa lengo la kuyapa nguvu ya kisheria majukumu ya msingi na muhimu ya usalama ambayo kwa sasa yanatekelezwa na Idara lakini hayatambuliwi na Sheria. Majukumu hayo ni pamoja na ulinzi binafsi wa Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa, ulinzi wa Vituo Muhimu, mamlaka ya upekuzi wa kiusalama wa viongozi na udhibiti wa matishio ya kiusalama dhidi ya Jamhuri ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** inapendekezwa kifungu cha 6 cha Sheria kifanyiwe marekebisho ili kuweka sifa za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na kuainisha masharti kuhusu nafasi hiyo baada ya utumishi. Lengo la marekebisho haya ni kupata mtendaji mwenye uwezo sifa, weledi na kulinda maslahi ya kiusalama kwa watu ambao wamewahi kutumikia nafasi ya Mkurugenzi Mkuu.

Aidha, katika kuboresha utendaji kazi wa Idara, inapendekezwa kuongeza vifungu vipya vya 6A na 6B katika Sheria ili kuweka masharti kuhusu nafasi za Naibu Wakurugenzi Wakuu kwa Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na nafasi ya Wakurugenzi wengine katika Idara watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Vilevile, inapendekezwa kuainisha masharti kuhusu sifa za uteuzi katika nafasi hizo tajwa.

**Mheshimiwa Spika,** inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 7 cha Sheria ili kuainisha masharti kuhusu vigezo vya ajira kwa watumishi wa Idara. Marekebisho haya pia yanaweka sharti la matumizi ya silaha wakati wa utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa Idara kwa lengo la kutambua matumizi ya silaha na kuweka utaratibu wa nidhamu ya umiliki na matumizi ya silaha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii pia inapendekeza kurekebisha kifungu cha 10 cha Sheria ili kumtambua Mkurugenzi Mkuu kama Mshauri Mkuu wa Rais na Serikali katika masuala ya Usalama wa Taifa. Lengo ni kutambua wajibu wa Idara katika usimamizi na udhibiti wa Usalama wa Taifa. Aidha, kwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Idara, Sheria inarekebishwa kwa kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya nidhamu kwa watumishi walio chini yake. Hali kadhalika, kifungu cha 13 kinarekebishwa ili kuainisha utaratibu wa kuapishwa kwa Mkurugenzi Mkuu, Naibu Wakurugenzi Wakuu, Wakurugenzi na Maafisa wa Idara.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 16 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya udhibiti wa utambulisho wa Maafisa na watu wengine wanaoshirikiana na Idara. Lengo la marekebisho haya ni kuwalinda maafisa na watu hao kutokana na utendaji wao wa kazi za kiusalama. Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza kinga dhidi ya mashtaka kwa Maafisa wa Idara wanapotekeleza majukumu yako kwa mujibu wa sheria tofauti na ilivyo sasa ambapo kinga inahusu tu mashauri ya madai dhidi ya Maafisa hao. Lengo la marekebisho haya ni kuweka kinga dhidi ya makosa yanayoweza kutendeka wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa uaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 16(3), 17(3), 20(2) na 23 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali kutegemeana na uzito wa kosa. Lengo

la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa viwango hivyo vya

adhabu vinaendana na mazingira ya sasa. Aidha, Sehemu hii inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 24, 25 na 26 vitakavyoainisha masharti mbalimbali, ikiwemo udhibiti wa Maafisa kutoa taarifa za kiusalama pindi wanapostaafu au kumaliza vipindi vya ajira, kuzuia uingiaji katika maeneo ya Idara bila idhini na masharti kuhusu vitendo vya uvunjifu wa Sheria nje ya mipaka ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Sheria linapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiapo cha utii pamoja na kurekebisha kiapo cha utumishi na kutunza siri.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka, 2023 (The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Act, 2023) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA

George Boniface Simbachawene (Mb)
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
07/06/2023

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, Sura ya 406 *(The Tanzania Intelligence and Security Services (Amendment Bill, 2023))*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huo ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Kikako cha 28, Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati iliuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali Tarehe 25 Mei, 2023 ili kupata maelezo ya Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu maudhui ya Muswada huo. Baada ya maelezo, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 29 Mei, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 31 Mei, 2023 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uchambuzi wa Muswada, Kamati ilichambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, Sura ya 406 ukiwa umegawanyika katika Sehemu Kuu mbili (2). Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayoeleza jina la Sheria. Vilevile, inaweka masharti kwamba Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa Sura ya 406.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifungu vinavyofanyiwa marekebisho pamoja na maudhui yake ni kama ambavyo imeelezwa kwenye wasilisho la Serikali lililofanyika hivi punde. Kamati itajielekeza kwenye matokeo ya uchambuzi maoni na usahuri. Kwa hiyo naomba urejee ukurasa wa 14.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yalivyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 2 Kamati ilipendekeza kufutwa kwa neno "*Tanzania*" na kutumika kwa neno "*United Republic*" ili kuweka usawa (*uniformity*) wa matumizi ya msamiati

huo kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimwa Spika, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kufuta neno Tanzania na kutumia Msamiati "*United Republic*" pale kote neno Tanzania litatumika kwa kumaanisha Nchi.

Mheshimwa Spika, Katika Ibara ya 3(c) Kamati ilipendekeza kuongeza neno "*or necessary service*" mara baada ya neno "*establishment*" kwenye tafsiri ya Msamiati "*vital installation*". Hii ni kwa nia ya kulinda vifaa au miundombinu mbalimbali inayotumika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Idara.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kuongeza maneno yaliyopendekezwa katika tafsiri ya Msamiati "*vital installation*".

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 5(e) inayohusu utoaji wa ulinzi kwa viongozi, Kamati ilipendekeza mpangilio wa orodha ya viongozi waliowekwa katika Kifungu hicho kifuate itifaki sahihi (*order of priority*) kwenye mpangilio wa Viongozi na Kuwaongeza Wanasheria Wakuu wa Tanzania na Tanzania Zanzibar.

Aidha, Kamati ilishauri kufuta neno "*in*" kwenye Ibara ya 5(e)(xiv) na kuandika neno "*upon*" ili kuweka ulazima kwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara kufanya mawasiliano na Rais kabla ya kuongeza mtu mwingine kwenye hadhi ya kupewa ulinzi wa Idara.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya mabadiliko ya mpangilio wa Viongozi Pamoja na kuwaweka Mwanasheria Mkuu wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Zanzibar, Pamoja na kuweka neno "*upon*" na kuondoa neno "*in*".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7(d) inakusudia kufanya marekebisho kwa kuweka masharti yanayozuia Mkurugenzi Mkuu wa Idara kuajiriwa au kuteuliwa katika nafasi yeyote ya utumishi Serikalini baada ya kuitumikia nafasi hiyo. Kamati ilishauri kuwa

Katazo hilo liondolewe kwani linakinzana na Masharti ya Ibara ya 9 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kufuta Ibara ya 7(d) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Katika Ibara ya 8(3) inayohusu sifa za kumteua Naibu Mkurugenzi Mkuu. Kamati ilipendekeza kuweka sifa ya mtu ambae atateuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu Bara awe na asili ya kutoka Tanzania Bara kama ilivyo kwa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 11(e) inayohusu Mkurugenzi Mkuu kuwa mamlaka ya mwisho ya nidhamu na maamuzi yake kuwa ya mwisho. Kamati ilipendekeza kuwa Ibara hiyo ieleze kuwa kutakuwa na mchakato wa kisheria "*due process*" na kufuta maneno "*final and conclusive*" yanayoonekana katika Ibara hiyo na badala yake ibaki tu kuwa Mkurugenzi Mkuu atakuwa mamlaka ya nidhamu kwa Watumishi wa Idara kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 12 cha Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kama Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Katika Ibara ya 18 ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ilikusudia kuongeza Ibara ndogo ya (3) na siyo kuifuta kwa kuwa haipo kwenye Sheria Mama, Hivyo Kamati ilipendekeza kufuta maneno "*deleting subsection (3) and substituting for it*" na badala yake kuandika maneno "*adding immediately after subsection (2)*" ili kuleta maana iliyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kuhusu mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 22(b) Kamati ilipendekeza marekebisho ya kiuandishi kwa kufuta neno "*carving*" na kuandika neno "*carrying*" ilikuleta maana iliyokusudiwa. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kufanya marekebisho kama ililivyopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu za kudumu za Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ndugu Moses M. Kusiluka Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Ikulu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndugu Onorius Njole, pamoja na Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Vilevile nimshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge ikiwemo Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninaishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ambayo imehusika na uratibu wa shughuli zote za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii wakiwemo Ndugu Frank Rumisha Nkya, Ndugu Praisegod Lukio, Ndugu Ganjatuni Kilemile, Ndugu Elizabeth Malogo, Ndugu Idda Kombe, Ndugu Daniel Salamba, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Theresia Jacob.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA IDARA YA USALAMA WA TAIFA, SURA YA 406 [*THE TANZANIA INTELLIGENCE AND SECURITY SERVICE (AMENDMENT) BILL, 2023]* - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 **Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, Sura ya 406 *(The Tanzania Intelligence and Security Services (Amendment) Bill, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huo ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Kikako cha 28, Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la 12.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba,

Kamati iliuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 1.2 **Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 25 Mei, 2023 ili kupata maelezo ya Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu maudhui ya Muswada huo. Baada ya maelezo , Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing*) tarehe 29 Mei, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 31 Mei, 2023 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 **Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, Sura ya 406 *(The Tanzania Intelligence and Security Services (Amendment) Bill, 2023)* ukiwa umegawanyika katika Sehemu Kuu mbili (2). Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayoeleza jina la Sheria. Vilevile, inaweka masharti kwamba Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa Sura ya 406.

### 2.2 **Vifungu vinavyofanyiwa Marekebisho na Maudhui Yake**

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2** inakusudia kufanya marekebisho kwa kuondoa neno "Waziri" kila linapoonekana katika Sheria kwa lengo la kuondoa dhamana ya Usalama wa Taifa kutoka kwa Waziri na kuweka jukumu hilo kwa Rais.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3** inakusudia kufanya marekebisho kwa kufuta baadhi ya misamiati katika kifungu cha Sheria kinachotoa tafsiri ya misamiati na kuongeza misamiati mipya ambayo haikuwepo kwenye Sheria inayokusudiwa kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4** inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 4 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 3 ili kuipa Idara hadhi ya Chombo cha Ulinzi na Usalama na kuiweka chini ya usimamizi wa Rais. Aidha, kifungu kinakusudia kufuta maneno "***regional na district offices"*** na badala yake kuweka maneno "***directorates, regional and district offices or any other office."*** Lengo ni kuanzisha Kurugenzi ndani ya Idara.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 5 (1) cha Sheria kwa;-

(i) kufuta aya (a) inayohusu jukumu la Idara katika kukusanya taarifa za kiusalama na kukiandika upya;

(ii) kuongeza aya mpya za (e), (f), (g), (h) na (i) kwa lengo la kuboresha kwa kuongeza majukumu ya Idara yanayotekelezwa kwa sasa ikiwa ni pamoja na ulinzi binafsi wa Viongozi wa ngazi za juu wa Kitaifa na Kimataifa, ulinzi wa wagombea wa Urais wa Nchi, ulinzi wa vituo muhimu, mamlaka ya upekuzi wa kiusalama wa Viongozi na udhibiti wa matishio ya kiusalama dhidi ya Jamhuri ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6** inakusudia kufanya marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 5A kuweka masharti yanayomtaka Waziri anaye husika na masuala ya Usalama wa Taifa kutekeleza masuala ya Kisera na Kibajeti ya Idara.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 6 cha Sheria kwa lengo la kuweka masharti yanayozuia Mkurugenzi Mkuu wa Idara kuajiriwa au kuteuliwa katika nafasi yeyote ya utumishi Serikalini baada ya kuitumikia nafasi hiyo. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza Kifungu kidogo kipya cha (2) kinachohusu sifa za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu;

(b) Kuvipanga upya vifungu vidogo vya (2) hadi (5);

(c) Kuongeza Kifungu kidogo cha (6) kinachohusu Naibu Wakurugenzi;

(d) Kuzipanga upya vifungu vidogo vya (6) na (7).

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 6 kwa:-

(a) Kuongeza Kifungu kipya cha 6A kinachotoa masharti kuhusu nafasi za Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Bara na wa Zanzibar;

(b) Kuongeza Kifungu cha 6B kinachotoa masharti kuhusu nafasi ya Wakurugenzi wengine katika Idara watakaoteuliwa na Rais kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu wa Idara; na

(c) Kuweka masharti kuhusu sifa za uteuzi katika nafasi hizo tajwa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 7 cha Sheria kwa;-

(a) Kufuta maneno "***and members"*** yanayoonekana katika aya (a) ya Kifungu kidogo cha 7(1);

(b) Katika Kifungu kidogo cha 7(2) kwa kufuta maneno "***or of the Revolutionary Government of Zanzibar";***

(c) Kuifuta na kuandika upya aya ndogo ya 7(2)(a) inayohusu kuajiri za mkataba na za kudumu kwa maafisa wa Idara;

(d) Kuongeza Kifungu kidogo cha (3) kinachohusu kukidhi masharti ya ajira kwa maafisa wa Idara;

(e) Kuvipanga upya vifungu vidogo vya (3) na 4);

(f) Kuongeza Vifungu vipya vya (6) na (7) vyenye lengo la kuweka sharti la matumizi ya silaha na kuweka utaratibu wa nidhamu ya umiliki na matumizi ya silaha hizo.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 cha Sheria kinachohusu katazo la matumizi ya Sheria ya Utumishi wa Umma kwa Maafisa wa Idara kwa kuongeza maneno ***"unless the context requires otherwise"*** katika Kifungu cha 9 (1) na kufuta na vifungu vidogo vya 5 na 6. Lengo ni kuweka masharti ya kutumika kwa Sheria ya Utumishi wa Umma kwa Maafisa wa Idara pale mazingira yatakaopo lazimu.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11** inakusudia;-

(a) Kufanya marekebisho katika Kifungu cha 10 cha Sheria kinachuhusu majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa Idara kwa kufuta maneno ***"the directions of the Minister***" yanayoonekena katika Kifungu kidogo cha (1);

(b) Kuongeza Kifungu kidogo cha (2) kinacho eleza kuwa Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye mshauri Mkuu wa masuala ya ulinzi na usalama kwa Rais;

(c) Kukipanga upya Kifungu kidogo cha (2);

(d) Kufuta maneno ***and unless the Minister directs otherwise in writing;*** na

(e) Kuongeza Kifungu kidogo cha 10 (4) kwa lengo la kumtambua Mkurugenzi Mkuu wa Idara kuwa ndiye mwenye mamlaka ya nidhamu kwa maafisa na waajiriwa walio katika Idara na kuwa maamuzi yake ndiyo yatakuwa ya mwisho utakao hitimisha shauri la nidhamu.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12** inakusudia kufanya marekebisho kwa kuongeza Kifungu kipya ili kuweka masharti yatakayomwezesha Katibu Mkuu Kiongozi kuratibu na kuwa kiungo baina ya Rais na Idara katika utekelezaji wa masuala ya Kisera na Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika, Ibara 13** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu 11 cha Sheria kinachohusu wajibu wa Waziri katika kutoa maelekezo kwa kufuta maneno "***and a copy of any such direction..."*** na kwa kukifuta Kifungu kidogo cha (3).

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 13 cha Sheria kwa kukifuta na kukiandika upya Kifungu cha 13, kinachoweka utaratibu wa kuapishwa kwa Mkurugenzi Mkuu, Naibu Wakurugenzi Wakuu, Wakurugenzi na Maafisa, na kwamba kiapo hicho kitawafunga watumishi tajwa hata baada ya Utumishi wao kukoma.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14 cha Sheria kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (5) kinachohusu wajibu wa Idara kukusanya taarifa zinazohusu ulinzi wa maeneo maalum ambayo kama yakiharibiwa au kuhujumiwa yataathiri uchumi, ulinzi na usalama wa nchi na kushauri Serikali na Mamlaka zinazohusika.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 15 cha Sheria kwa kufuta aya (c) na kuiandika upya, kufuta Kifungu kidogo cha (4) na kukiandika upya. Lengo la mabadiliko hayo ni kuiwesha Idara kushirikiana na Idara, Taasisi au vyombo vingine vya Usalama Kimataifa. Ushirikiano huo utafanyika kwa idhini ya Rais.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 16 cha Sheria kinachohusu kuzuia kuchapisha na kutangaza taarifa kwa kufuta Kifungu kidogo cha 16(1) na kukiandika upya, pamoja na kufuta maneno "***Minister"*** katika Kifungu kidogo cha (2) na badala yake kuweka neno "***Director General".***

Aidha, Ibara inakusudia kufuata maneno ***"not exceeding five hundred shillings"*** yanayoonekana katika Kifungu kidogo cha (3) na badala yake kuweka maneno "***of not less than twenty million shillings or to imprisonment for a term not less than 15 years or to both."*** Lengo ni kuongeza adhabu ili kuzuia ufichuaji wa utambulisho wa watu wanaofanya kazi katika Idara au watu wengine wanaoshirikiana na Idara na kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya udhibiti wa watu hao ikiwa ni kuwalinda Maafisa na watu hao kutokana na utendaji wao wa kazi za kiusalama.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 17 (3) kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kukiandika upya. Kifungu hiki kimenakiliwa kimakosa kwa sababu katika Sheria inayokusidiwa kurekebishwa hakuna Kifungu cha 17 (3).

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19** inakusudia kufanya marekebisho ya kimuundo katika Kifungu cha 18 (1) ili kusomeka kama Kifungu cha 18. Aidha, kufuta maneno aya 18(b) na kuyaandika upya, pamoja na kufuta Kifungu kidogo cha 2. Kifungu hiki kinahusu ushirikiano unaoweza kufanywa baina ya Idara kuingia kwenye makubaliano na idara nyingine, taasisi za Serikali au Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20** inakusudia kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 19 kwa kufuta Kifungu kidogo cha 1 na

kukiandika upya. Pia katika Kifungu kidogo cha 3 kwa kufuta maneno "***Attorney General***" na badala yake kuweka maneno "***Attorney General, Director of Public Prosecution or Solicitor General as the Case may be"*** ili kuweka kinga dhidi ya Maafisa wa Idara katika makosa yanayoweza kutendeka wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa uaminifu.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu 20(2) cha Sheria kwa kufuta maneno "***five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years"*** na kuyaandika upya kama "***fifteen million shillings or to imprisonment for a term of not less than fifteen years"*** kwa lengo la kuongeza viwango vya adhabu kwa kosa la kutoa taarifa inayohusiana na kazi iliyofanywa chini ya
Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 22 cha Sheria kinachohusu utungwaji wa Kanuni kwa kufuta maneno ya utangulizi na kuyaandika upya ili yasomeke ***"President may upon a recommendation of the Director General, make regulations providing for,"***

Aidha, kuongeza aya mpya (b) na zipanga upya aya (b), (c), (d) na (e). Kufanya marekebisho katika Kifungu cha 22(2) kwa kufuta maneno ***"members"*** na badala yake kuandika maneno ***"Officers."*** Lengo ni kuwatambua maafisa wa Idara kama Maafisa tofauti na ilivyokuwa awali kwenye Sheria walitambulika kama *Members.*

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 23 cha Sheria kwa kufuta maneno "***not exceeding three hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding twelve months"*** na badala yake kuyaandika upya kama ***"of not less* than *ten million shillings or to imprisonment for a term of not less than ten years"*** lengo ni kuhakikisha viwango hivyo vya adhabu vinaendana na mazingira ya sasa.

Vile vile kufuta na kuandika upya aya (b), na kufuta maneno **"a fine not exceeding *five hundred shillings or imprisonment for a***

***term not exceeding thirthy six months without remission or to both the fine and imprisonmnet”*** yanayoonekana mwishoni mwa sentensi na kuyaandika upya ili yasomeke ***“imprisonment for a term of not less than fifteen years”***

Aidha, Ibara pia inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu kidogo cha (3) cha Sheria kwa kufuta maneno ***“a fine not exceeding three hundred thousand shillings or imprinsomnet for a term not exceeding six months or to both the fine and imprisonment”*** na kuyaandika upya yasomeke ***“for term of not less than fifteen years”*** lengo ni kuhakikisha viwango hivyo vya adhabu vinaendana na mazingira ya sasa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24** inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 24 cha Sheria kwa kuongeza Vifungu vipya vya 24, 25, 26, na 27.

**Mheshimiwa Spika,** Vifungu 24 na 25 zinakusudia kuweka masharti mbalimbali ikiwemo kuwakataza wa maafisa kutoa taarifa pindi wanapostaafu au kumaliza vipindi vya ajira na kuzuia uingiaji katika maeneo ya Idara bila idhini.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 26 kinakusudia kuweka sharti kuhusu vitendo vya uvunjifu wa Sheria nje ya mipaka ya Tanzania kuwa vitahesabika kama kosa kwa mujibu wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 27 kinakusudia kuweka masharti kwa makosa ambayo hayajatajwa adhabu yake katika Sheria hii, itakuwa ni faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungu miaka 5.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25** inakusudia kufanya marekebisho kwa kufuta jedwali na kuliandika upya kwa lengo la kuongeza kiapo cha utii, kurekebisha kiapo cha utumishi na kiapo cha kutunza siri kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa taarifa na ufanishi katika utekelezaji wa majukumu ya Idara.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 **Maelezo ya Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuatazo;

i) **Mheshimiwa Spika,** katika Ibara ya 2 Kamati ilipendekeza kufutwa kwa neno "*Tanzania*" na kutumika kwa neno "*United Republic*" ili kuweka usawa (*uniformity*) wa matumizi wa msamiati huo kama ilivyo katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano.

**Mheshimwa Spika**, Serikali imekubaliana na maoni ya Kamati kwa kufuta neno Tanzania na kutumia Msamiati "*United Republic*" pale kote neno Tanzania litatumika kwa kumaanisha Nchi.

ii) **Mheshimwa Spika**, Katika Ibara ya 3(c) Kamati ilipendekeza kuongeza neno "*or necessary service*" mara baada ya neno "*establishment*" kwenye tafsiri ya Msamiati "*vital installation*". Hii ni kwa nia ya kulinda vifaa au miundombinu mbalimbali inayotumika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Idara.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kwa kuongeza maneno yaliyopendekezwa katika tafsiri ya Msamiati "*vital installation*".

iii) **Mheshimiwa Spika,** Katika Ibara ya 5(e) kinachohusu utoaji wa ulinzi kwa viongozi, Kamati ilipendekeza mpangilio wa orodha ya viongozi waliowekwa katika Kifungu hicho kifuate itifaki sahihi (*order of priority*) kwenye mpangilio wa Viongozi na Kuwaongeza Wanasheria Wakuu wa Tanzania na Tanzania Zanzibar.

Aidha, Kamati ilishauri kufuta neno "*in*" kwenye Ibara ya 5(e)(xiv) na kuandika neno "*upon*" ili kuweka ulazima kwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara kufanya mawasiliano na Rais kabla ya kuongeza mtu mwingine kwenye hadhi ya kupewa ulinzi wa Idara.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya mabadiliko ya mpangilio wa Viongozi Pamoja na kuwaweka Mwanasheria Mkuu wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Zanzibar, Pamoja na kuweka neno "*upon*" na kuondoa neno "*in*".

i) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 7(d) inakusudia kufanya marekebisho kwa kuweka masharti yanayozuia Mkurugenzi Mkuu wa Idara kuajiriwa au kuteuliwa katika nafasi yeyote ya utumishi Serikalini baada ya kuitumikia nafasi hiyo. Kamati ilishauri kuwa Katazo hilo liondolewe kwani linakinzana na Masharti ya Ibara ya 9 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kufuta Ibara ya 7(d) ya Muswada.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 8(3) inayohusu sifa za kumteua Naibu Mkurugenzi Mkuu, Kamati ilipendekeza kuweka sifa ya mtu ambae atateuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu bara awe na asili ya kutoka Tanzania bara kama ilivyo kwa Tanzania Zanzibar. Mheshimiwa Spika, Serikali imekubaliana na mapendekezo yaliotolewa na Kamati.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 11(e) inayohusu Mkurugenzi Mkuu kuwa mamlaka ya mwisho ya nidhamu na maamuzi yake kuwa ya mwisho, Kamati ilipendekeza kuwa Ibara hiyo ieleze kuwa kutakuwa na mchakato wa kisheria "due process" na kufuta maneno "final and conclusive" yanayoonekana katika ibara hiyo na badala yake ibaki tu kuwa Mkurugenzi Mkuu atakuwa mamlaka ya nidhamu kwa Watumishi wa Idara kwa kuzingatia Masharti ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kama Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

iv) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 18 ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ilikusudia kuongeza Ibara ndogo ya (3) na sio kuifuta kwa kuwa haipo kwenye Sheria Mama, Hivyo Kamati ilipendekeza kufuta maneno "*deleting subsection (3) and substituting for it*" na badala yake kuandika maneno "*adding immediately after subsection (2)"* ili kuleta maana iliyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati kuhusu mapendekezo hayo.

v) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 22(b) Kamati ilipendekeza marekebisho ya kiuwaandishi kwa kufuta neno “carving” na kuandika neno “carrying” ilikuleta maana iliyokusudiwa. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kufanya marekebisho kama ililivyopendekezwa na Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

**4.1** Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb - **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesra Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ndg. Moses M. Kusiluka Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Ikulu, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Vilevile nimshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndg. Micheal Chikokoto, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge ikiwemo Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, niishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ambayo imehusika na uratibu wa shughuli zote za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii wakiwemo Ndg. Frank Rumisha Nkya, Ndg. Praisegod Lukio, Ndg. Ganjatuni Kilemile, Ndg. Elizabeth Malogo, Ndg. Idda Kombe, Ndg. Daniel Salamba, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Theresia Jacobs.

4.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
08 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwenyekiti.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 *(The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Kwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, aje awasilishe hoja yake kuhusu Mabadiliko hayo ya Sheria Mbalimbali. Mheshimiwa Waziri Dkt. Damas Ndumbaro.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kabla ya kutoa Maelezo ya kuhusu Muswada huu, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai na afya njema kwa kuniwezesha kusimama kwa mara nyingine tena mbele ya Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria ya Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kwa ushirikiano na ushauri walioupata wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria ya Mwaka 2023 *(The Laws Revision Miscellaneous Amendment Bill, 2023)* unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane

zilizoainishwa katika sehemu ya pili hadi sehemu ya tisa ya Muswada. Marekebisho yanayopendekezwa yanatokana na zoezi la urekebu wa sheria inayoendelea kutekelezwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambalo kwa sasa lipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, urekebu wa sheria ni zoezi linalohusisha uhuishaji na uchapishaji wa kitabu cha sheria *(Statute Book)*. Zoezi hili pamoja na mambo mengine linahusisha na kujumuisha marekebisho yote yaliyofanywa katika sheria mbalimbali pamoja na kufuta vifungu vya sheria vilivyofutwa katika marekebisho ili kurahisisha rejea ya matumizi ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, zoezi la urekebu kwa sheria kuu hufanywa kwa mujibu wa sheria ya urekebu wa sheria sura ya nne. Kwa mujibu wa sheria hiyo, zoezi la urekebu linawahusisha Waziri mwenye dhamana na sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwandishi Mkuu wa Sheria. Sheria inamtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumwelekeza Mwandishi Mkuu wa Sheria kufanya urekebu wa sheria kuu kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Urekebu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mwandishi Mkuu wa Sheria baada ya kupokea maelekezo hayo anapaswa na kutoa toleo la urekebu. Wakati wa kuandaa toleo hilo, sheria inamruhusu Mwandishi Mkuu wa Sheria kuboresha na kurekebisha makosa madogo madogo katika sheria ambayo hayatabadili maudhui ya sheria. Endapo marekebisho yanabadili maudhui ya sheria, yatahitajika marekebisho hayo kuwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya sheria ili yaweze kupitishwa na Bunge na kuwa sehemu ya sheria za nchi. Hivyo, kupitishwa kwa marekebisho yanayopendekezwa kutawezesha kuwa sehemu ya sheria husika na kujumuishwa kwenye toleo la urekebu lenye juzuu 14 liliokusudiwa kutolewa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane zifutazo:-

(1) Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi Sura ya 119 yaani *(The Corporate Sole Establishment Act Cap. 119);*

(2) Sheria ya Usimamizi na Tozo ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147 *(The Excise Management and Tariffs Act Cap. 147);*

(3) Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 *(The Income Tax Act Cap. 332);*

(4) Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya kwanza *(The Interpretation of Laws Act Cap. 1);*

(5) Sheria ya Urekebu wa Sheria Sura ya 4 *(The Laws Revision Act Cap. 4);*

(6) Sheria ya Hifadhi ya Jamii Sura ya *135 (The Social Security Act Cap. 135);*

(7) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399 *(The Tanzania Revenue Authority Act Cap. 399);* na

(8) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263 *(The Workers Compensation Act Cap. 263)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi na yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho, zimerekebishwa katika sehemu husika ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 5 kifungu kidogo cha (2) cha sheria ya uanzishwaji wa mashirika binafsi sura ya 119. Kifungu hiki kimeyataka mashirika yote yaliyoanzishwa chini ya sheria hii kukopa kutoka Serikalini na benki zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali ambazo kwa sasa hazimilikiwi na Serikali. Hivyo, inapendekezwa kurekebisha kifungu hiki ili kuyawezesha mashirika hayo kukopa siyo tu Serikalini, bali hata katika taasisi za fedha nyingine kwa kuzingatia masharti ya sheria ya mikopo, dhamana na misaada ya Serikali sura ya 134 kama ilivyo kwa mashirika mengine ya umma.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Tozo ya

Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147 ambapo sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla na katika kifungu cha pili ili kuondoa matumizi ya neno "*excise*" na badala yake kutumia neno "*authority*". Lengo ya marekebisho haya ni kuhuisha sheria hii kwa kuweka utaratibu unaotumika sasa ambapo masuala ya utozaji wa ushuru wa bidhaa yanafanywa na kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 100 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha fedha zilizopatikana kutokana na mamlaka kushinda katika mashauri mbalimbali yanayohusiana na ushuru wa bidhaa kujumuisha katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa sasa sheria inaelekeza fedha hizo ziwekwe kwenye mfuko wa ushuru wa bidhaa ambao haupo. Lengo la marekebisho hayo ni kujumuisha katika sheria, utaratibu sahihi wa ukusanyaji wa mapato na ambao ndiyo unaotumika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu cha 107 kinafutwa ili kuondoa masharti ya uteuzi wa Maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendesha mashauri yanayohusiana na ushuru wa bidhaa nchini chini ya sheria hii na badala yake masuala hayo kusimamiwa na Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Sura ya 430. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya sheria hii na masharti ya Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuhusu masuala ya uteuzi wa waendesha mashtaka kwani kwa sasa Maafisa wa Mamlaka huteuliwa kuendesha mashauri ya kikodi kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 ambapo Kifungu cha 65E kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa kujumuisha mirabaha *(royalty)* ya shughuli za madini katika orodha makato yasioruhusiwa *(non-allowable deductions)*. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya kifungu hiki na masharti ya Kifungu cha 65E kifungu kidogo cha (1) kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria Na. 7 ya Mwaka 2017 ambapo *royalty* ilifutwa katika orodha ya makato yanayokubalika *(allowable deductions)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria sura ya kwanza ambapo Kifungu kipya cha 49A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka mipaka ya utekelezaji wa mamlaka ya kurekebisha majedwali ya sheria hususan katika uteuzi wa muundo wa Wajumbe. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba masuala ya muundo, uteuzi na muda wa Wajumbe wa chombo cha usimamizi cha taaisisi ambacho ni masuala ya msingi katika sheria yanaamuliwa na Bunge, na vile vile kuziba mianya ya matumizi mabaya ya mamlaka katika masuala hayo yanayoweza kusababishwa na uwepo wa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Urekebu wa Sheria Sura ya Nne ambapo Kifungu cha Saba kinarekebishwa kwa kuongeza mamlaka ya urekebu kutojumuisha jedwali lolote la sheria katika toleo la urekebu. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Mwandishi Mkuu wa Sheria kutojumuisha jedwali lolote la kisheria katika toleo la urekebu endapo ataona kuwa kujumuishwa kwa jedwali husika katika toleo la urekebu kutaharibu maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha nane kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) ili kuweka ulinzi kwa suala, kitendo, shauri au sheria ndogo yoyote itakayotengenezwa kabla ya kuchapishwa kwa toleo la urekebu pale ambapo kuna mabadiliko yoyote yamefanywa kama vile mpangilio wa sehemu ya vifungu, mpangilio wa namba, masahihisho ya rejea ya vifungu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Jamii Sura ya 135 ambapo kifungu cha 34 kinarekebishwa ili kuondoa Divisheni ya Hifadhi za Jamii, mamlaka ya kutengeneza kanuni na badala yake kuyaweka mamlaka hayo kwa Waziri mwenye dhamana. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa upungufu uliojitokeza baada ya majukumu na mamlaka iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii kuhamishiwa kwa divisheni hiyo ambayo moja kati ya mamlaka hayo yalikuwa ni kutengeneza kanuni. Hivyo kwa marekebisho yanayopendekezwa, mamlaka

hayo yatatekelezwa na Waziri ambaye ndio mamlaka ya juu katika Wizara na siyo divisheni kama ilivyo katika kifungo hicho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399 ambapo kifungu 5 (7) kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata wa tafsiri ya kifungu hicho ambacho kina lengo la kuainisha namna ya utekelezaji wa vifungu vinavyorejewa katika kifungu hicho na siyo kuanza kutumika kwa masharti yanayorejewa kama inavyoonekana sasa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika sehemu ya fidia kwa wafanyakazi Sura ya 263 ambapo kifungu cha 19 (5) kinarekebishwa kwa kufutwa maneno *"serious disablement"* yanayotafsiriwa katika kifungu kidogo hicho na badala yake kuweka maneno *"permanent total disablement."* Lengo la marekebisho hayo ni kuondoa maneno ambayo hayajatumika na kuweka maeneno sahihi yaliyotumika na yaliyokusudiwa kutafsiriwa katika kifungu hicho kidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mara nyingine tena naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria ya Mwaka 2023 *(The Laws Revision Miscellaneous Amendment Bill, 2023)* na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolea lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa niaba yake Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza. *(Makofi)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA - MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria wa Urekebu wa Sheria Mbalimbali za Mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea, kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni kuhusu Muswada huo kwa njia ya kielektroniki au kufika kwenye Kikao cha Kamati kilichofanyika siku ya Jumamosi tarehe 27 Mei, 2023. Hata hivyo, katika mkutano huo wadau waliojitokeza hawakuwa na maoni kuhusu Muswada huu badala yake wadau hao walikuwa na maoni kwenye Miswada mingine iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati. Kamati ina maoni kuwa, kutokuwepo kwa maoni kuhusu Muswada huu, kunaashiria wadau na jamii kwa ujumla kukubaliana na mapendekezo ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa Sheria ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Nane zinaweka

masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika sheria kuu nane (8). Sheria hizi ni kama ifuatavyo: -

(1) Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119;
(2) Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
(3) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(4) Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya kwanza;
(5) Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4;
(6) Sheria ya Hifadhi za Jamii, Sura ya 135;
(7) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; na
(8) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya uchambuzi na upembuzi wa kina kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya uchambuzi huo, pamoja na majumuisho yaliyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati hii kama ilivyokuwa kwa wadau mbalimbali, inakubaliana kwa sehemu kubwa na mapendekezo ya Muswada huu. Aidha, uchambuzi kuhusu maudhui ya sheria zinazorekebishwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, Marekebisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya pili ya Muswada kuanzia Ibara ya tatu hadi Ibara ya nne. Ibara ya nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119 kwa kukifuta na kukiandika upya ili kuruhusu mashirika yaliyomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kuruhusiwa kukopa fedha Serikalini katika benki mbalimbali za kibiashara. Awali, kifungu hicho kilikuwa kinaruhusu mashirika hayo kukopa Serikalini na katika benki zilizokuwa zikimilikiwa na Serikali ikiwemo Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)* na Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIB)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwa kuwa yakiridhiwa na Bunge yatawezesha Mashirika ya Umma yenye umiliki wa Serikali pekee kupata fedha kwa ajili ya mikopo na hivyo kuwezesha kukuza mitaji, kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili, Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya tatu ya muswada kuanzia Ibara ya tano hadi Ibara ya tisa. Ibara ya sita inapendekeza kurekebishwa kwa kufuta neno *"Excise"* kila linapoonekana katika Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, na badala yake kuweka neno *"Authority"*, likiwa na maana ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha sheria kuendana na uhalisia ulivyo sasa ambapo masuala ya utozaji wa ushuru wa bidhaa yanatekelezwa na kusimamiwa na *TRA*. Aidha, tafsiri ya neno *"Excise"* katika sheria hiyo linapendekezwa kufutwa na badala yake tafsiri ya neno *"Authority"* litumike likiwa na maana ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 100 cha Sheria kwa kufuta maneno *"Excise Revenue"* na badala yake kuweka maneno *"Consolidated Fund"*. Lengo la marekebisho ni kuwezesha fedha zinazopatikana kutokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kushinda mashauri yanayohusu ushuru wa bidhaa kujumuishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya tisa inapendekeza kufuta Kifungu cha 107 cha Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 inayoruhusu Maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kuendesha mashauri ya kijinai kwa makosa yanayotokana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii. Lengo ni kuendana na uhalisia ulivyo sasa ambapo makosa ya jinai yanaendeshwa na kusimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa Mamlaka iliyopewa na Sheria ya Taifa ya Mashtaka Sura ya 420.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa marekebisho haya kwa kuwa yanajibu ushauri wa kamati uliowahi kutolewa katika nyakati mbalimbali. Aidha, kamati inashauri ikiwa kuna sheria nyingine inayoruhusu maafisa wake ambao siyo maafisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuendesha na kusimamia mashauri ya jinai sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ili jukumu hilo libaki likisimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mshtaka kwa kuwa ndiyo yenye jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, tatu; Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Muswada kuanzia Ibara ya 10 hadi Ibara ya 11. Kwa mujibu wa ibara zinazopendekezwa zinakusudia kujumuisha malipo ya mrabaha inayotokana na shughuli za madini katika orodha ya mapato yasiyo ruhusiwa kwa kuongeza aya (b) mara baada ya aya (a) ya kifungu cha 65(E2) kwa Sheria ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuweka uwiano wa masharti ya kifungu hiki cha sheria na masharti ya kifungu cha 65 (E1) kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 2017 ambapo mrabaha ilifutwa kama *allowable deduction.* Kamati ina maoni kuwa; kuondolewa kwa malipo ya mrabaha kama sehemu ya mapato katika shughuli ya madini kutawezesha wadau wa madini kulipa kodi kutokana na faida halisia jambo ambalo litachochea uwekezaji katika shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, namba nne ni marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria sura ya kwanza. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya tano ya muswada kuanzia ibara ya 12 hadi ibara ya 13. Kwa ujumla ibara hizi zinakusudia kuongeza kifungu kipya cha 49(A) mara baada ya kifungu cha 49 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka mipaka ya utekelezaji katika mamlaka ya Waziri katika kurekebisha majedwali ya sheria mbalimbali ili kuhakikisha kwamba masuala ya muundo, uteuzi na muda wa wajumbe wa Bodi ambayo ni masuala ya msingi katika sheria inayoamuliwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile ibara inakusudia kuziba mianya ya matumizi mabaya ya mamlaka katika masuala ya wajumbe wa bodi ikiwa kutakuwa na maslahi binafsi. Aidha, kurekebishwa kwa vifungu hivi katika sheria hakuchukui au kuondoa mamlaka ya Waziri husika kuteua, kubadili au kuondoa Wajumbe wa Bodi kwa mujibu wa sheria bali inamzuia kubadili sheria ili kurekebisha utaratibu wa namna ya kuteua na kuwaondoa wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili sheria hii, kamati ilikuwa na hoja katika kifungu cha 84 kinachoeleza kuwa, Mwanasheria

Mkuu wa Serikali ataweza kutafsiri sheria iliyotungwa katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kingereza au iliyotungwa katika lugha ya Kingereza kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Kamati ilishauri jukumu hilo la kutafsiri sheria lisiwe la hiari bali liwe ni la lazima. Lengo ni kuhakikisha sheria zinakuwa katika lugha zote za Kiswahili na Kingereza ili kurahisisha usomaji na kueleweka baina ya watu wanaotumia lugha hizo, lakini pia zitumike katika kufundisha lugha inayotumika kufundishia wanafunzi wa elimu ya sheria katika vituo mbalimbali. Baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kamati.

Mheshimiwa Spika, namba tano ni Marekebisho ya Sheria ya Urekebu wa Sheria sura ya nne. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya sita ya Muswada, Ibara ya 14 hadi Ibara ya 16. Pamoja na mambo mengine, mapendekezo yanakusudia kurekebisha kifungu cha saba cha Sheria ya Urekebu wa Sheria kwa lengo la kumpa mamlaka Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* kutokujumuisha jedwali la Sheria katika Toleo la Urekebu ikiwa ataona kujumuisha kwa jedwali hilo kutaharibu maana iliyokusudiwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapendekezo ya sehemu hii pia yanakusudia kulinda uhalali wa jambo lolote lililokwisha fanyika kabla ya kuanza kutumia kwa Toleo Jipya la Urekebu wa Sheria mbalimbali. Katika kujadili mapendekezo haya, kamati ilitoa angalizo la kuhakikisha malengo ya sheria yanabaki katika kama yalivyokusudiwa na Bunge ili kubaki na maana iliyokusudiwa. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na ushauri wa kamati na ikakusudia kuboresha ibara husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya sita. Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii sura ya 135. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya saba ya Muswada kuanzia Ibara ya 17 hadi Ibara ya 18. Kwa ujumla marekebisho yanakusudia kufuta neno *division* na badala yake kuweka neno *minister* katika kifungu cha 34(2) cha Sheria ya Hifadhi ya Jamii. Lengo la marekebisho hayo ni kumpa Waziri mwenye dhamana masuala ya hifadhi ya jamii kutengeneza kanuni badala ya kazi hiyo kutekelezwa na *division* ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Sheria namba saba ni marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya nane ya Muswada kuanzia Ibara ya 19 hadi Ibara ya 20. Maudhui ya marekebisho yanakusudia kuweka bayana mamlaka ya Waziri katika kifungu cha 5(7) cha sheria kutangaza katika Gazeti la Serikali tarehe ya kuanza kwa ukadiriaji na mapato. Ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato yatokanayo na sheria zisizokuwa za kodi yaliyoainishwa katika sehemu (b) ya jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Uchambuzi wa kamati umebaini kurekebishwa kwa sheria hii kutaongeza uhiyari katika ulipaji mapato.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya nane ni Marekebisho ya Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi sura ya 263. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya tisa ya Muswada kuanzia Ibara ya 21 hadi Ibara ya 22. Maudhui ya sehemu hii yanakusudia kufuta maneno *serious disablement* na badala yake kuweka maneno *permanent total disablement.* Kamati ilipendekeza maneno husika yabaki kwa kuwa kuna uwezekano wa mtu kuumia kwa kiasi kikubwa ikiwa na maana ya *serious disablement.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kamati ilielezwa kuwa katika suala la fidia kutokana na kuumia kazini utaratibu unaohusika ni ule ule unaohusu *permanent total disablement* na siyo *serious disablement* na hivyo ikakubalika ibara ibaki kama ilivyopendekezwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, kamati inakubaliana kwa ujumla na mapendekezo ya Muswada kama yalivyowasilishwa na Serikali. Kwa sababu hii kamati ina maoni na ushauri kwa ujumla kuhusu Muswada huu. Maoni na ushauri huu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mosi; kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada huu wenye lengo la kurekebisha maudhui ya sheria mbalimbali ili ziendane na lengo lililokusudiwa katika sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inashauri utaratibu huu uendelee ili kuwa na sheria zenye uhalisia na uhai na kukidhi malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mbili; kazi ya kufanya urekebu wa sheria isichukue muda mrefu kama ilivyozoeleka. Kamati ilielezwa kuwa urekebu unaoendelea sasa utawezeshwa kutolewa kwa majukumu ya sheria jambo ambalo mara ya mwisho lilifanyika mwaka 2002 kwa kuwa kupitia urekebu wa sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapata fursa ya kubaini mapungufu mbalimbali katika sheria mbalimbali kama ilivyokuwa sasa. Kamati inashauri kazi hii ifanyike kwa vipindi vifupi zaidi tofauti na sasa ilivyochukua miaka 20.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao katika kutekeleza majukumu yao ya Kikatiba walichambua, kujadili na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa kamati ushirikiano na ushauri wako na kwa maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inashauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2023 pamoja na marekebisho yake kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UREKEBU WA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2023 *(THE LAWS REVISION (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2023)* – KAMA LIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu **Muswada wa Sheria ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 (The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Act, 2023).**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Kikao cha Ishirini na Nane cha Mkutano wa Kumi na Moja, tarehe 18 Mei, 2023 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 96 (1)**. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 136 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Damasi Daniel Ndumbaro (Mb.), siku ya Ijumaa tarehe 26 Mei, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni (Public Hearing) kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielekroniki au kufika kwenye kikao cha kamati kilichofanyika siku ya Jumamosi tarehe 27 Mei, 2023. Hata hivyo, katika Mkutano huo wadau waliojitokeza hawakuwa na maoni kuhusu Muswada huu badala yake wadau hao walikuwa na maoni kwenye miswada mingine iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati. Kamati inamaoni kuwa kutokuwepo kwa maoni kuhusu Muswada huu, kunaashiria wadau na jamii kwa ujumla kukubaliana na mapendekezo ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maelezo ya Serikali, na kufanya uchambuzi wa Muswada huu, siku ya Alhamisi tarehe 01 Juni, 2023 Kamati ilifanya majumuisho na Serikali kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada huu. Majumuisho hayo yalifanyika kwa kumuhusisha Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na watendaji mbalimbali wa taasisi za Serikali zinazohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa.

**SEHEMU YA PILI**

2.0 **UCHAMBUZI WA MUSWADA**

2.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 (The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Act 2023) unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Tisa (9). Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Nane zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika Sheria Kuu Nane (8). Sheria hizo ni: -

a) Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119 (The Corporations Sole (Establishment) Act, (Cap. 119));

b) Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (The Excise (Management and Tariff) Act, (Cap. 147);

c) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (The Income Tax Act, Cap 332);

d) Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1 (The Interpretation of Laws Act, Act, Cap. 1);

e) Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4 (The Laws Revision Act, Cap 4);

f) Sheria ya Hifadhi za Jamii, Sura ya 135 (The Social Security Act, Cap. 135);

g) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 (The Tanzania Revenue Authority Act, Cap. 399) na

h) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 (The Workers' Compensation Act, Cap 263).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba, Muswada huu wa urekebu wa Sheria mbalimbali unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria nilizozitaja kwa lengo la kuondoa mapungufu mbalimbali yaliyobainika wakati wa zoezi la urekebu wa Sheria Kuu unaotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya uchambuzi na upembuzi wa kina kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya uchambuzi huo pamoja na majumuisho yaliyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati hii kama ilivyokuwa kwa wadau mbalimbali, inakubaliana kwa sehemu kubwa na mapendekezo ya Muswada huu. Aidha, uchambuzi kuhusu maudhui ya Sheria zinazorekebishwa ni kama ifuatavyo:-

2.2 **Marekebisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya 119 (The Corporations Sole (Establishment) Act, (Cap. 119)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Pili ya Muswada kuanzia **Ibara ya 3** hadi **Ibara ya 4**. Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha **Kifungu cha 5(2)** cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi, Sura ya

119 kwa kukifuta na kukiandika upya ili kuruhusu mashirika yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja (**corporate sole**) kuruhusiwa kukopa fedha Serikalini na katika benki mbalimbali za kibiashara. Awali, kifungu hicho kilikuwa kinaruhusu mashirika hayo kukopa Serikalini na katika benki zilizokuwa zikimilikiwa na Serikali ikiwemo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB). Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwa kuwa yakiridhiwa na Bunge yatawezesha mashirika ya Umma yenye umiliki wa Serikali pekee kupata fedha kwa njia ya mkopo hivyo kuwezesha kukuza mitaji, kujiendesha kibiashara na kupunguza utegemezi wa fedha za Serikali.

2.3 **Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (The Excise (Management and Tariff) Act, (Cap. 147)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Tatu** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 5** hadi **Ibara ya 9**. **Ibara ya 6** inapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "**Excise**" kila linapoonekana katika Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, na badala yake kuweka neno "**Authority**", likiwa na maana ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA).** Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha sheria kuendana na uhalisia ulivyo sasa ambapo masuala ya utozaji wa ushuru wa bidhaa yanatekelezwa na kusimamiwa na **TRA**. Aidha, tafsiri ya neno "**Excise**" katika sheria hiyo linapendekezwa kufutwa na badala yake tafsiri ya neno "**Authority**" litumike likiwa na maana ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA**).

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 8** ya Muswada inapendekeza kurekebisha **Kifungu cha 100** cha Sheria kwa kufuta maneno "**Excise revenue"** na badala yake kuweka maneno "**Consolidated Fund"**. Lengo la marekebisho ni kuwezesha fedha zinazopatikana kutokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kushinda mashauri yanayohusu ushuru wa bidhaa kujumuishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali yaani "**Consolidated Fund"**.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9** inapendekeza kufuta **Kifungu cha 107** cha Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 inayoruhusu maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA**)

kuendesha mashauri ya kijinai kwa makosa yanayotokana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii. Lengo ni kuendana na uhalisia ulivyo sasa ambapo makosa ya jinai yanaendeshwa na kusimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mamlaka iliyopewa na Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 420. Kamati inaipongeza Serikali kwa marekebisho haya kwa kuwa yanajibu ushauri wa Kamati uliowahi kutolewa katika nyakati mbalimbali. Aidha, kamati inashauri ikiwa kuna sheria nyingine inayoruhusu maafisa wake ambao sio maafisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuendesha na kusimamia mashauri ya jinai, Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ili jukumu hilo libaki likisimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kuwa ndio yenye jukumu hilo.

2.4 **Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (The Income Tax Act, Cap 332)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Nne ya Muswada** kuanzia **Ibara ya 10** hadi **Ibara ya 11**. Kwa ujumla, Ibara zinazopendekezwa zinakusudia kujumuisha malipo ya mrabaha (**royalty**) yanayotokana na shughuli za madini katika orodha ya makato yasiyoruhusiwa **(non-allowable deductions**) kwa kuongeza aya (b) mara baada ya aya (a) ya **kifungu cha 65E (2)** cha sheria ya Mapato. Lengo la marekebisho haya ni kuweka uwiano wa masahrti ya Kifungu hiki cha sheria na masharti ya kifungu cha 65E(1) kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria Na. 7 ya Mwaka 2017 ambapo mrabaha (royalty) ilifutwa kama allowable deduction. Kamati inamaoni kuwa, kuondolewa kwa malipo ya mrabaha kama sehemu ya mapato katika shughuli za madini kutawezesha wadau wa madini kulipa kodi kutokana na faida halisia jambo ambalo litachochea uwekezaji katika shughuli za madini.

2.5 **Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1 (The Interpretation of Laws Act, Act, Cap. 1)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Tano ya Muswada** kuanzia **Ibara ya 12** hadi **Ibara ya 13**. Kwa ujumla Ibara hizi zinakusudia kuongea Kifungu kipya **cha 49A** mara baada ya Kifungu **cha 49** cha Sheria ya Tafsiri za Sheria. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka mipaka

ya utekelezaji wa mamlaka ya Waziri katika kurekebisha majedwali ya sheria mbalimbali ili kuhakikisha kwamba masuala ya muundo, uteuzi na muda wa wajumbe wa Bodi ambayo ni masuala ya msingi katika Sheria yanaamuliwa na Bunge. Vilevile Ibara inakusudia kuziba mianya ya matumizi mabaya ya mamlaka katika masuala ya wajumbe wa Bodi ikiwa kutakuwa na maslahi binafsi. Aidha, kurekebishwa kwa vifungu hivi katika sheria hakuchukui au kuondoa mamlaka ya Waziri husika kuteua, kubadili au kuwaondoa wajumbe wa Bodi kwa mujibu wa sheria bali inamzuia kubadili sheria ili kurekebisha utaratibu wa namna ya kuteua na kuwaondoa wajumbe hao.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujadili Sheria hii, Kamati ilikuwa na hoja katika **Kifungu cha 84** kinachoeleza kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali **anaweza** kutafsiri Sheria iliyotungwa katika lugha ya Kiswahili Kwenda katika lugha ya kingereza, au iliyotungwa katika lugha ya kingereza kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Kamati ilishauri jukumu hilo la kutafsiri sheria lisiwe la hiyari bali liwe la lazima. Lengo ni kuhakikisha sheria zinakuwa katika lugha zote za Kiswahili na kingereza ili kurahisisha usomaji na kueleweka baina ya watu wanaotumia lugha hizo, lakini pia zitumike katika kufundishia katika lugha inayotumika inayotumika kufundishia wanafunzi wa elimu ya sheria katika vyuo mbalimbali. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati.

2.6 **Marekebisho ya Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4 (The Laws Revision Act, Cap 4)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Sita** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 14** hadi **Ibara ya 16**. Pamoja na mambo mengine, mapendekezo yanakusudia kurekebisha **Kifungu cha 7** cha Sheria ya Urekebu wa Sheria kwa lengo la kumpa mamlaka Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (**CPD**) kutojumuisha jedwali la Sheria katika Toleo la Urekebu ikiwa ataona kujumuishwa kwa jedwali hilo kutaharibu maana iliyokusudiwa katika sheria. Aidha, mapendekezo ya sehemu hii pia yanakusudia kulinda uhalali wa jambo lolote lililokwisha fanyika kabla ya kuanza kutumia kwa Toleo jipya la Urekebu wa Sheria mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kujadili mapendekezo haya, kamati ilitoa angalizo la kuhakikisha malengo ya sheria yanabaki kama yalivyokusudiwa na Bunge ili kubaki na maana iliyokusudiwa. Baada ya majadiliano, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na inakusudia kuboresha Ibara husika.

2.7 **Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii Sura ya 135 (The Social Security Act, Cap. 135)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Saba** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 17** hadi **Ibara ya 18**. Kwa ujumla marekebisho yanakusudia kufuta neno "**Division**" na badala yake kuweka neno "**Ministe**r" katika Kifungu cha 34 (2) cha Sheria ya Hifadhi ya Jamii. Lengo la marekebisho haya ni kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Hifadhi za Jamii kutengeneza Kanuni badala ya kazi hiyo kutekelezwa na Divisheni ya Hifadhi ya Jamii.

2.8 **Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 (The Tanzania Revenue Authority Act, Cap. 399)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **Sehemu ya Nane** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 19** hadi **Ibara ya 20**. Maudhui ya marekebisho yanakusudia kuweka bayana mamlaka ya Waziri katika **Kifungu cha 5(7)** cha Sheria kutangaza katika Gazeti la Serikali tarehe ya kuanza kwa ukadiriaji wa mapato, ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato yatokanayo na sheria zisizokuwa za kodi (**non-tax law**) yaliyoainishwa katika Sehemu "B" ya jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Uchambuzi wa Kamati umebaini kurekebishwa kwa Sheria hii kutaongeza uhiyari katika ulipaji wa mapato.

2.9 **Marekebisho ya ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 (The Workers' Compensation Act, Cap 263)**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **Sehemu ya Tisa** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 21** hadi **Ibara ya 22**. Maudhui ya sehemu hii yanakusudia kufuta maneno "**serious disablement**" na badala yake kuweka maneno

“**permanent total disablement**”. Kamati ilipendekeza maneo husika yabaki kwakuwa kuna uwezekana wa mtu kuumia kwa kiasi kikubwa ikiwa na maana ya “**serious disablement**”. Hata hivyo, kamati ilielezwa kuwa katika suala la fidia kutokana na kuumia kazini, utaratibu unaohusika ni ule unaohusu **permanent total disablement** na sio **serious disablement** na hivyo ikakubalika Ibara ibaki kama ilivyopendekezwa katika Muswada.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana kwa ujumla na mapendekezo ya Muswada kama yalivyowasilishwa na Serikali. Kwa sababu hii, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kuhusu Muswada huu. Maoni na ushauri huo ni kama ifutavyo: -

(a) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada huu wenye lengo la kurekebisha maudhui ya Sheria mbalimbali ili ziendane na lengo lililokusudiwa katika sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inashauri utaratibu huu uendelee ili kuwa na sheria zenye uhalisia na uhai na kukidhi malengo yaliyokusudiwa.

(b) Kazi ya kufanya urekebu wa Sheria isichukue muda mrefu kama ilivyo zoeleka. Kamati ilielezwa kuwa, urekebu unaoendelea sasa utawezesha kutolewa kwa majuzuu ya Sheria, jambo ambalo mara ya mwisho lilifanyika mwaka 2002. Kwa kuwa kupitia urekebu wa sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapata fursa ya kubaini mapungufu mbalimbali katika sheria mbalimbali kama ilivyokuwa sasa, Kamati inashauri kazi hiyo ifanyike kwa vipindi vifupi zaidi tofauti na sasa ilivyochukua miaka 20.

(c) Urekebu unaofanyika katika Sheria Kuu ufanyike pia katika Kanuni mbalimbali kwa lengo la kurahisisha kueleweka kwa kwa urahisi na jamii ya Watanzania.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ambao katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama, Mb. | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. | Makamu |
| 3. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo

muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (Mb.), na Naibu Waziri wake Mhe. Pauline Gekul (Mb.) kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (Mb.), akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali **(CPD)** Ndg. Onorius Njole kwa kuandaa Muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika Sheria wakati wa zoezi la urekebu lialoendelea. Aidha, Kamati inawashukuru pia kwa ushirikiano walioipatia kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati inanawashukuru pia watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wote kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, ndc, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, ndc Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio, Ndg. Ganjatuni Kilemile, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Elizabeth Malogo, Ndg. Thomas Shawa, Ndg. Thuwaiba Jumbe, wakisaidiwa na Ndg. Theresia Jacob.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 (The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Act, 2023)** pamoja Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
08 Juni, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge Miswada yote mitatu imeshawasilishwa na hapa nimeletewa orodha ya Wabunge ambao wameomba kuchangia lakini kabla hawajaanza kuchangia niwatangaze wageni ambao wameingia baada ya tangazo la awali la wageni.

Tunao wageni 76 wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao ni Chawa wa Mama Mkoa wa Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 116 na walimu nane kutoka Chama cha Skauti Tawi la Shule ya Awali na Msingi *Green Belt* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa taarifa za ziada kuhusu shule hii, kwanza hii ni shule mojawapo ambayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI wamejenga ile shule ya mfano ya awali. Nadhani mliiona ile shule nzuri sana hawa watoto ndiyo wanatoka kwenye hiyo shule na nimeambiwa hii shule iko Jimbo la Ukonga la Mheshimiwa Jerry William Silaa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeletewa orodha ya wanafunzi 34 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi Ebonite ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 30 wa Shule ya Msingi Betha ya Kibamba Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitaanza kuwaita hawa wanaochangia niwakumbushe tu kwamba uchangiaji ni wa vifungu jamani, vifungu vya sheria, kwa hiyo, kwa sababu hapa tuko kwenye michango kwa ajili ya utungaji wa sheria, kwa hiyo, niwakumbushe michango yetu iwe inajielekeza huko.

Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema leo na pili nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha sheria zetu; tatu nimpongeze Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma wakili msomi Simbachawene, Naibu Waziri Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wakili, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Ndumbaro wakili, Mheshimiwa *Attorney General* Jaji Eliezer Feleshi na watumishi wote ambao wamehusika kuleta maboresho ya Miswada hii mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa Tume ya Mipango na nianze kwa kusoma Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 63(3)(c) inasema hivi na ninaomba ninukuu. "kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo."

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa ni jukumu la msingi la Bunge hili na ndiyo maana Muswada huu ambao unafufua tena Sheria ya Tume ya Mipango ni jukumu zuri sana na tunampongeza Mheshimiwa Rais lakini Wabunge wengi wamezungumza hapa kwenye mjadala huu wa bajeti wakati fulani fulani wakisema wakielezea umuhimu wa kuwa na Tume ya Mipango ya Taifa. Kwa hivyo Muswada huu leo utaleta tena Tume hii ya Mipango ya Taifa kwa hiyo, kwa kweli tunawapongeza Serikali kwa kuleta mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakumubuka Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima alizungumza hapa sana kuhusu uzuri wa Taifa kuwa na mpango wa muda mrefu na wa muda wa kati kwa sababu ndiyo itaongoza Taifa letu. Sasa muswada huu leo utafanya hayo yawezekane lakini mtakumbuka vile vile kwamba Sheria ya Fedha ya 2018 ilifuta iliyokuwa Sheria ya Tume ya Taifa sura ya 314 na kwa hivyo sasa tumerudisha tena lakini imerudi namna gani sasa?

Mheshimiwa Spika, kwanza tunampongeza Mheshimiwa Rais siyo tu kwamba imerudi lakini imerudi kwa sura mpya zaidi. Ukilinganisha sheria iliyofutwa majukumu ya tume yalikuwa ni 13 lakini kwa mujibu wa sheria hii sasa Muswada huu majukumu yameongezeka kutoka 13 hadi majukumu 19 na hii inaonyesha tu dhahiri kwamba kuna imerudi kwa sura na nguvu mpya zaidi na mategemeo yetu kwamba baada ya sheria hii kupitishwa na Bunge hii tume itafanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii vilevile imetengeneza kwa mara ya kwanza na niseme tu kwa historia ya nchi yetu hii Tume ya Mipango imekuwa inapewa majina tofauti tofauti lakini ipo tangu mwaka 1961. Kwa hivyo kila wakati tumekuwa tunabadilisha majina na kubadilisha kwamba safari hii iwe Ofisi ya Makamu wa Rais, iwe chini ya Wizara ya Fedha lakini tafiti zinaonyesha kwamba nchi ambazo zinachukulia kwa usahihi na kwa lugha ambayo ni kubwa zaidi ni kwamba tume hii ikiwa chini ya Mheshimiwa Rais kama Mwenyekiti itafanya itaongezea nguvu na hadhi kubwa tume hii na utafiti duniani inaonyesha nchi zinazofanya vizuri zaidi kwa mfano Ghana, Indonesia, Afrika Kusini na India zote zina tume hii na Mwenyekiti wa tume hii ni Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzuri wa sheria hii safari hii kwa sasa bado ni Muswada kwa mara ya kwanza na haijawahi kutokea hii imeona jukumu la kupanga na jukumu la fedha kwamba ni vitu viwili tofauti. Imeleta wazo la kuwa na Mawaziri wawili ambao ni wajumbe kwenye tume hii ambaye ni Waziri anayeshughulika na masuala ya fedha na Waziri atakayeshughulika na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kwa kweli ni *innovation* mpya sana kwa hiyo kwa mara ya kwanza baada ya Muswada huu kupita kuwa sheria tutategemea hata muundo wa Serikali utabadilika. Tutakuwa na Waziri ambaye ana *deal* na maendeleo ya Taifa peke yake halafu kutakuwa na Waziri wa Fedha ambao wote sasa ni Wajumbe kwenye tume hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma kifungu cha tano utaona Wajumbe wengine ambao wanaongezwa wakiwemo Katibu Mkuu. Kwa hivyo tume hii kwa mara ya kwanza itakuwa na nguvu kubwa zaidi ya kuongoza Taifa kwa mambo yote yanayohusiana na maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, kwa kweli ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sheria ya, kuna utafiti fulani umefanywa 2022 na kuonyesha kwamba Wizara ya Fedha sasa kwa majukumu yake yaliyo mengi na kwa sababu tayari yalikuwa ni mengi tu ukiongezea jukumu la kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa ni kazi kubwa zaidi. Hawataweza kuweka nguvu kubwa zaidi kwenye kutunga au kutengeneza Sera za Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kweli niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwamba kwa mara ya kwanza sasa hii sheria ikipita tutatarajia sasa mipango ya Taifa hili itakuwa ni ya muda mrefu, itaongoza Taifa letu na itaratibu mipango ya Wizara zingine na kutoa dira ya kimaendeleo kwa Taifa letu. Kwa hiyo nawaombeni sana tuunge mkono hii ipite kwa nguvu kubwa kidogo ili tutume ujumbe kwamba kwa kweli yale mawazo yenu kuhusu Tume hii kurudishwa tena na siyo tu kurudi lakini imeboreshwa zaidi kwa mara ya kwanza italeta manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sheria nyingine ni hii ya *TISS (*Tanzania *Intelligence and Security Services bill)* ambayo vilevile kamati yetu iliweza kuchambua na kwa kweli tulikubaliana kwamba kutokana na maendeleo ya intelijensia inavyoenda Duniani yapo maboresho ambayo ni ya lazima kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Muswada huu sasa wa sheria hii inapunguza kazi za Waziri ambaye atakuwa anahusika ili kazi yake iwe ni mambo ya bajeti na mambo ya sera; na tumejaribu kuangalia sera na sheria zingine dunia, ziko hivyo. Kwa hivyo kwa kweli madhumuni ya kubadilisha muundo na kubadilisha kazi za *TISS* ili kazi yao iwe zaidi katika kuangalia mambo ya *intelligence;* na kwa kwakweli badala ya kwenda kwa Waziri waende kwa Mheshimiwa Rais; Kamati yetu iliona kwamba ina tija kubwa sana. Na hata baada ya kuwauliza wale ambao ni Mawaziri, ni Wizara hiyo wakakubali, kwamba kwa kweli *in fact* hata kwa *fact* tu peke yake huwa inafanyika hivyo kwa hiyo hakukuwa na hoja kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nyingine kubwa ambayo ni nzuri kwa sheria hii ni kwamba kwa kuwa *TISS* ni chombo cha Muungano. Sheria kuweka muundo sasa ambao ni wakimuungano ilikuwa ni wazo ambalo ni zuri sana, tuwe na ma-*directors* ambao mmoja anatoka upande mwingine wa muungano na mwingine anatoka upande mwingine wa muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hii tu, ni pamoja na kuwa na sifa za hawa ambao watakuwa wanaongoza vyombo hivi na kwa kweli tuliona kwamba ni *innovation* kubwa nzuri sana kwa kisheria hatuwezi kuwachagua watu ambao sifa zao haziko kisheria. Kwa hiyo hiyo pia inaonyesha kwamba tuko *serious* kuangalia zile *credentials* na kujua kwamba hawa wawe na sifa hizi, na kwa kweli sheria kwa mara ya kwanza imeweka vizuri sana hili jukumu na kwa kweli ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sheria nyingine ni hii ya *revision laws amendment bill,* na yenyewe ukiangalia baadhi ya marekebisho yaliyoletwa kwa mfano Kifungu cha 14. Mtakumbuka mwaka mmoja, miwili iliyopita tulitunga sheria hapa tukasema sheria zetu zibadilishwe ziende kwa lugha ya Kiswahili, na sasa kuna zoezi linaendelea la kufanya sheria zote ambazo ziko kwa kingereza zifanywe kwa kiswahili. Lakini kwa kutambua jukumu vilevile kwamba sheria zetu zinatumika vyuoni na wanakuja Watanzania kutoka kila mahala na wanakuja watu kutoka nje ya Tanzania ni

vyema tuwe na sheria za kiswahili lakini vilevile tuwe na sheria zimeandikwa kwa lugha ya Kingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata Mahakama zetu siyo Watanzania pekee wanaenda wanaoenda huko lakini tulivyobadilisha ile sheria hatukuweka vizuri muda maalumu wa kufanya sheria hizi zote ziwe zinapatikana kwa lugha zote mbili. Kwa hiyo kati ya marekebisho haya ambayo yameletwa sheria hii sasa inaweka vizuri, kwamba sasa Serikali watakuwa na siku 90 baada ya sheria kupitishwa kwa lugha ya Kiswahili halafu na wao baada ya siku 90 wawe wamebadilisha iwe kwa lugha ya kingereza.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia itaondoa ombwe fulani la kuwa na sheria kwa lugha moja halafu kesho wanafunzi, vyuo vikuu ama mtu anakwenda Mahakamani halafu sheria bado haijatafsriwa ipo kwa lugha moja. Kwa hiyo mimi nadhani hii kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria hii kwakweli ni *innovation* kubwa na tumegundua haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo liko jambo lingine hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeishagonga.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ahaa baada ya kusema hayo naomba niwashawishi tuunge mkono, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeishamtaja Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia marekebisho ya sheria hizi muhimu. Mimi nitazungumzia Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, na kama muda utatosha nitazunguzia Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa tuliyonayo ilitungwa mwaka 1996, na leo hii ina miaka 27. Kwa hiyo ni muda mrefu nadhani Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwa kipindi cha miaka 27 kwa vyovyote kumetokea mabadiliko mengi, na hii fursa sasa ya kuweza kufanya marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa tunatakiwa tuione kwamba ni fursa ya kufanya maboresho; kwa hiyo tujadili na kuweza kubadili mambo ambayo yanamanufaa.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ya marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa imefanya maboresho kadhaa kwenye sheria iliyopo *(principal legislation)* na yote yanalengo ya kuendana na hali ya kisasa na kuweka muundo wa kisasa ambao utafanya italeta ufanisi wa Idara ya Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ibara ya pili ya marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa kimsingi inabadilisha muundo wa idara na sasa unapendekeza kwamba jukumu la Usalama wa Taifa liwe chini ya Mheshimiwa Rais moja kwa moja badala ya kupitia kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa ni *issue very sensitive* kwa hiyo badiliko hili la kimuundo la kuhakikisha Idara ya Usalama wa Taifa inasimamiwa moja kwa moja chini ya Mheshimiwa Rais nadhani ni jambo la kuungwa mkono kutokana na u-*sensitive* wa shughuli za Usalama wa Taifa. Lakini vilevile mabadiliko ya muundo huu sasa yatafanya chombo hiki kiwe na hadhi ya chombo cha Usalama wa Taifa ambacho kitakuwa chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Rais moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tukubali marekebisho ya Sheria hii ya Idara ya Usalama wa Taifa, na hasa kifungu hiki ibara ya 2 ambayo kimsingi inakabidhi jukumu hili *very sensitive* sasa lisimamiwe moja kwa moja na Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 15 ya marekebisho ya Sheria hii ya Idara ya Usalama wa Taifa inaongeza majukumu ya Idara hii ya Usalama wa Taifa. Moja ya majukumu ambayo yanaongezwa ni kwamba Idara ya Usalama wa Taifa sasa itakuwa na jukumu la

kukusanya taarifa za ki-*intelligence a* kwa ajili ya kufanya ulinzi kwa maeneo muhimu, tunaita *vital installation* ya kiuchumi. Kuna baadhi ya maeneo ambayo yakiharibiwa au yakifanyiwa hujuma yanasababisha tatizo kubwa sana la kiuchumi

Mheshimiwa Spika, na sasa hivi nchi yetu tunashuhudia uwekezaji mkubwa sana katika maeneo ya kiuchumi, kwa mfano uwekezaji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, uwekezaji kwenye reli ya kisasa, uwekezaji kwa maeneo kama ya Bandari, na uwekezaji kwenye maeneo mengine mengi tu.

Mheshimiwa Spika, na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kwa dhamira hii ya dhati ya kufanya uwekezaji mkubwa sana ambao pengine huko nyuma hatukuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hizi *vital installation* kwa mfano Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR* na mambo mengine, sasa hivi ibara ya 15 ya marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa inaipa idara hii jukumu la kufanya ulinzi wa hizi *vital installation.* Kwa hiyo *vital installation* zote hizi ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi na zinahitaji kulindwa kwa gharama yoyote kwa sababu Serikali imewekeza fedha nyingi na zisipolindwa zikahujumumiwa zitaleta hasara kubwa ya kiuchumi. Sasa jukumu hilo linakuwa la Usalama wa Taifa kuweza kufanya ulinzi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwamba wakubali na kupitisha marekebisho ya Sheria ya Sheria hii ya Idara ya Usalama wa Taifa kwa sababu ina lengo jema la kuhakikisha *vital installation,* uwekezaji katika maeneo muhimu ya kiuchumi unalindwa ili tusipate hasara ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, lakini Idara ya Usalama wa Taifa imekuwa ikifanya baadhi ya kazi ya kazi zingine ambazo sasa zinawekwa rasmi kisheria ili watu wetu wa Idara waweze kufanya hizi *confidently,* kwa kujiamini, kwa sababu sasa baadhi ya majukumu kama ulinzi wa viongozi, ulinzi wa vituo maalum nimezungumza *vital installation*, udhibiti wa matishio ya kiusalama,

upekuzi wa viongozi sasa yanawekwa rasmi kisheria na watu wa idara nina uhakika sasa watafanya kazi hizi *confidentially* kwa sababu sasa mambo haya yako wazi kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini jambao la jumla ni kwamba dunia inabadilika kwa kasi kubwa kiuchumi, kisayansi na kila sekta. Kwa hiyo hata namna ya watu wenye nia ovu ambao wanaweza kuja na kufanya labda mambo ya kigaidi, mambo ya hujuma na wao pia mbinu zao za namna ya kuja zinabadilika kutokana na muda unavyokwenda. Kwa hiyo kuna kila haja Idara yetu ya Usalama wa Taifa nayo ikawa inabadilika kutokana na muda unavyokwenda kwa sababu matishio ya kiugaidi yanaweza kuja kwa namna tofauti tofuati. Kwa hiyo ninaunga mkono mabadiliko haya ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa kwa sababu ni miaka 27 tangu sheria hiyo iliyokuwepo, kwa hiyo muda ni mrefu na unatosha sasa kufanya haya mabadiliko. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge tupitishe marekebisho haya ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa ya mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Uanzishwaji wa Tume ya Mipango. Mheshimiwa Olelekaita amezungumzia na nisingepeda kuzungumzia sana, lakini tulichobaini katika uchambuzi wa Kamati ni kwamba mipango ilikuwa inafanyika lakini kitendo cha kujumuisha Wizara ya Fedha na Mipango, Mipango kuiweka chini ya Wizara ya Wizara ya Fedha tatizo lililokuwa linatokea ni kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ilikuwa ina-*focus*, ina-*concentrate* sana kwenye utafutaji wa fedha kwenye mambo ya fedha na hili eneo la mipango ilikuwa ina muda finyu sana wa kulishulikia kwa hiyo mipango ikakosa *focus,* ikakosa namna ya kulisimamia na kuhakikisha kwamba mipango inaendana na namna ambavyo tumepanga.

Mheshimiwa Spika, mipango iko ya muda mrefu, iko ya muda wa kati na iko ya muda mfupi. Sasa jambo kubwa katika mipango ni ufuatiliaji na tathimini, acha tu kupanga mpango na kuhakikisha mpango upo, lakini ufuatiliaji na tathimini ndilo jambo sana katika eneo hili la mpango. Sasa hili lilikuwa linakosekana na Tume ya Mipango sasa inakuja na jibu na suluhisho katika hili eneo la ufuatiliaji na tathimini.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo bora zaidi ambalo linakuja na sheria hii ya uanzishaji wa Tume ya Mipango ni kwamba Tume hii sasa Mwenyekiti wake anakuwa ni Mheshimiwa Rais. Tume hii imepewa uwezo wa kufuatilia mipango ambayo inafnywa na Wizara zote na Idara zote na maeneo yote. Kwa hiyo kwa nguvu ya kwamba Tume hii itakuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais itafanya sasa Wizara na Idara nyingine zote kuweza kuitikia maelekezo ambayo yatakuwa yanatolewa na hii Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nisingependa kurudia hoja ambazo zimezungumzwa na Mheshimiwa Olelekaita, lakini niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tupitishe sheria hii ya uanzishwaji wa Tume ya Mipango. Sheria hii inakwenda kuiweka Tume ya Mipango kama idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo lile suala sasa la kuwa chini na la kujumuishwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na hatimaye Wizara hii ina-*focus* kwenye kutafuta fedha halafu mipango inakosa mtu wa kuisimamia hilo jambo sasa linakwenda kupata suluhisho. Hii ni kwa sababu hii itakuwa ni idara inayojitegemea na shughuli yake itakuwa ni mipango tu, kutengeneza dira, kuandaa mipango, kufanya tathimini ya rasilimali zote za nchi na kufanya ufuatiliji wa mipango inavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaweza tukawa na mpango wa muda mrefu, kwamba labda mpango wetu tunataka maji ya Ziwa Victoria yafike Dodoma au mpango wetu tunataka ekari za umwagiliaji sasa hivi labda tuna ekari milioni moja baada ya miaka mitano tufikishe ekari milioni saba za umwagiliaji. Kwa hiyo mpango huu ni wa muda mrefu lakini utavunjwa kwenda mipango midogo midogo ya mwaka mmoja mmoja. Kwa hiyo jambo kubwa hapa ni tathimini, ufuatiliaji *(monitoring and evaluation)* ili kuhakikisha hatu-*deviate* kutoka kwenye mpango ule mkubwa. Sasa hili jambo ndiyo sasa itafanywa na hii Tume ya Mipango ambayo itakuwa na jukumu moja tu badala ya kuchanganyika na Wizara ya Fedha ambayo ina jukumu kubwa la kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi kama Kamati tumeridhika kabisa kwamba Uanzishwaji wa Tume ya Mipango unakwenda kuongeza tija katika mapambano yetu ya kuinua uchumi wa nchi hii, kwa maana ya kwamba sasa tutapata idara ambayo ita *concentrate* naku-*focus* na mipango tu peke yake na kufanya ufuatiliaji na kutupa *feedback* ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tupitishe haya Marekebisho ya Sheria hizi kwa ajili ya manufaa ya nchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Na mimi nichangie katika Miswada hii iliyowasilishwa mbele yako na Mawaziri Wizara ya Utumishi pamoja na Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Miswada hii ina maslahi mapana sana ya nchi. Tulishuhudia kule nyuma wakati wa Tume ya Mipango ikiongozwa na Mheshimiwa Profesa Kighoma Ally Malima iliyvofanya kazi nzuri katka nchi hii. Lakini pia tuliona Mheshimiwa Warioba akiongoza Tume hii lakini mwisho kabisa Tume hii ilikuwa chini ya Dkt. Mpango ambayo leo ni Makamu wa Rais wa Nchi hii. Wakati huu wakati wa Dkt. Mpango Tume haikuwa na Wizara, ilikuwa ni Idara ndani ya Wizara ya Fedha tunapokwenda kuanzisha Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais tumeiondoa Wizara ya Fedha, tunampunguzia Waziri wa Fedha majukumu ya kuwaza badala ya kukusanya.

Mheshimiwa Spika, tumeona mambo kadhaa hapa yalipoletwa kwenye Kamati yetu, na sisi tumetaka kujiridhisha ni nchi gani ambazo ziko na mfano wa hii Tume. Mheshimiwa Olelekaita ametaja hapa nchi chache naomba tu niongezee hapa tu Zanzibar iko Tume ya Mipango ambayo Mwenyekiti wake ni Rais, Afrika Kusini pia ipo Tume ya Mipango ambayo Mwenyekiti wake ni Rais; na kama alivyosema India, Ghana na Indonesia.

Mheshimiwa Spika, tunapoiweka Tume ya Mipango kwenye Ofisi ya Rais chini ya Mwenyekiti Rais mwenyewe maana yake ni nini? maana yake sasa Mawaziri ambao kwenye baraza lake watawajibika kufata mipango itakayokuwa imetengenezwa na hii Tume.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hapa kipindi hiki cha Tume ipo na kipindi ambacho Tume haipo, tumeona namna ambapo kumekuwa na mkakanyiko, hatuna sera za kama nchi na tunapokwenda kumaliza dira hii inayoishia mwaka 2025, tumeshuhudia pia, na tumeona kamati pale Jakaya Kikwete ikitambulishwa ya kwenda kuandaa dira ya 2550. Tunapoenda kuunda Tume hii katika Mswada huu wa Tume ya Mipando ile Kamati sasa itakuwa chini ya hii Tume.

Mheshimiwa Spika, natamani na naomba sana Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu waupitishe Muswada huu kwa sababu utakuwa na tija katika nchi yetu hii. Tume hii itakuwa na Waziri wake, itakuwa na Katibu Mkuu, lakini na Mtendaji wa Tume. Hawa wakubwa hawa Waziri na Katibu Mkuu watashughulika tu na mambo ya sera, lakini Mtendaji Mkuu na wale watu wake ambao ni wasaidizi wake ndio watakaokaa na kujadili mara nyingi, lakini wataleta kwenye meza ambayo Wajumbe wa hiyo Tume ni Mawaziri mawili akiwemo Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango mwenyewe. Kwa maana hiyo, hakutakuwa na mkanganyiko wowote hapa na ndio maana sisi tulikataa Waziri wa Fedha tume iwajibike kwake kwa sababu na yeye ni Mjumbe wa Tume. Tume iwajibike moja kwa moja kwa Baraza la Mawaziri na itafanya sasa mlolongo ule uwe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke kwenye eneo hilo, niende katika eneo lingine. Niende kwanza kwenye urekebu kabla sijaja kwenye sheria hii ya *TIS*. Kwenye urekebu kuna maeneo yanakwenda kurekebishwa. Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.

Mheshimiwa Spika, hapa kulikuwa na tozo ambazo zilikuwa baada ya Serikali, baada ya mamlaka ambayo ni *TRA* ikishashinda mashauri ya kikodi, pesa hizi zilikuwa zinaingia tena

katika Mfuko wa Mamlaka. Sasa hivi kwa mabadiliko haya yanaenda kufanya pesa ambazo tutashinda katika mashauri ya kodi, ziende moja kwa moja katika Mfuko wa Serikali. Maana yake ni nini? Zile pesa zinakuwa zina miaka ya nyuma, miaka mitatu, miaka minne na hadi mitano. Sasa zinapoingia kwenye makusanyo ya *TRA,* unajikuta wakati mwingine unasema umevuka lengo kumbe ni makusanyo ambayo yametokana na kushinda katika mashauri ya kikodi. Kwa hiyo tunaenda kufanya sasa mashauri yote ya kikodi mamlaka ikishinda yanakwenda Serikalini, kwa sababu *TRA* anafanya kazi kwa niaba ya Serikali na hapo tunaenda kuisaidia mamlaka, lakini Serikali kuwa na makusanyo ambayo vizuri.

Mheshimiwa Spika, liko jambo ambalo linaenda kurekebishwa hapa katika Muswada huu wa Sheria ya Urekebu kwamba *loyalty* zile ambao zilikuwa zinalipwa na wachimbaji wetu wakubwa au wadogo, zilikuwa haziingii kama sehemu ya gharama kwamba ni sehemu ambazo hela iliyotoka, unatoa *loyalty,* kwa mfano mchimbaji wa *gemstone* akishachimba *gemstone,* anatoa 25% kabla ya kuanza kudadavua madadavuaji ya kodi. Sasa hivi Serikali inaenda kusaidia wachimbaji kupata motisha na uhalisia wa kazi hii. Maana yake miongoni mwa gharama ni ile pesa ambayo ameitoa Serikalini, *loyalty* ya 25% ilikuwa haiingii katika hesabu za kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inaenda kusaidia wananchi, kwamba ukishatoa nayo unaiweka katika hesabu za kodi kwamba ni miongoni mwa matumizi ambayo yametumika wakati unafanya shughuli za uchimbaji wako. Kwa hiyo tunaenda kusaidia wachimbaji wetu lakini tunasaida biashara, lakini pia tutavutia watu ambao wana nia njema ya kuja kuwekeza hapa Tanzania hasa katika eneo kubwa la uchimbaji mkubwa kama wa dhahabu na madini mbalimbali ambayo kila siku nchi hii inaendela kuvumbua.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu wa pili wa Usalama wa Taifa. Muswada huu hasa kipengele cha Msaidizi wa *DJS* wale wa bara, lazima atoke bara na atoke bara kwa uasilia wake na akiwa Mzanzibar basi atoke Zanzibar kwa uasilia wake. Hii inaenda kuondoa ombwe ambapo anaweza akatokea mtu

amezaliwa nchi nyingine ilimradi tu Mzanzibar anaweza akapata fursa hii adhimu, kwa hiyo au ni Mtanzania bara akapata fursa hii adhimu. Kwa hiyo tunaenda kuweka nchi katika usalama mkubwa katika chombo hiki ambacho ni madhubuti na adhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huu mdogo naomba niwashawishi Wabunge wenzangu waunge mkono Miswada hii mitatu ipite na iwe sheria, ikafanye kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Khadija Shaban Taya, ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGEESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Miswada hii, takribani mitatu iliyosomwa na Waheshimiwa Mawaziri hapa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lakini Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, lakini vile vile Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutuletea Miswada mizuri ambayo tunatakiwa kuijadili na hatimaye kuipitisha kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwanza kwenye Muswada wa Sheria huu wa *TISS,* wa Usalama wa Taifa. Inaonesha wazi kwamba Muswada huu ambao tunauzungumzia sasa hivi tunatakiwa tunapokwenda kuuzungumzia tuusome pamoja na sheria mama ukurasa namba 406. Ukisoma hivi vitu viwili bila kukiacha kimoja unaweza kuuelewa Muswada huu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kwa nini tunapendekeza Bunge hili liupitishe ili uanze kufanya kazi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Usalama wa Taifa wanaendelea kufanya kazi yao na kutuweka katika mazingira salama na viongozi wawe salama.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwa sababu katika Muswada huu viko vifungu kadhaa, ibara kadhaa ambazo zimewekwa na zimefanyiwa marekebisho kiasi kwamba sasa badala ya kufanyika

tu bila kuwa na utaratibu vimeingizwa kwenye sheria. Muswada huu umesema wazi kwamba sasa Mheshimiwa Rais ndiye atakuwa kiongozi wa chombo hiki. Mwanzo anaonekana Mheshimiwa Waziri, watu wote walikuwa wanatakiwa waende kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa ndiye mhusika wa Usalama wa Taifa. Kwa Muswada huu inaonekana kwamba sasa hivi kiongozi wa chombo hiki atakuwa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo katika ibara ya 5 tunaona wazi kabisa Muswada huu kwa nini napendekeza kwamba upitishwe, wanawekwa rasmi viongozi ambao wanatakiwa kuendelea kulindwa na Usalama wa Taifa. Mwanzo ukiangalia kwenye sheria zilikuwepo, viongozi hawa walilindwa lakini haikuwa rasmi kwenye maandishi kama inavyoonekana leo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tunaona viongozi mbalimbali hapa wakiwa wameandikwa kutokana na vyeo vyao na kama alivyokuwa anasema Mwenyekiti wa Kamati kwamba hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapa aongezwe ili aweze kupata ulinzi kwa utaratibu huu uliowekwa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ibara ya 6 utaona kuna kifungu namba 5A kimeingizwa pale ambacho kinawekwa masharti yanayoonesha wazi kwamba Waziri mhusika atabaki na sheria ya mambo ya kibajeti na mambo ya kisera. Kwa hiyo utaratibu wa Muswada huu unavyoonesha, unaonesha kabisa *responsibility matrix* yake inatuonesha kwamba Usalama wa Taifa sasa bajeti yao na sera zao zinakuja na Waziri hapa Bungeni. Ukienda kwenye ibara namba 19 ya Muswada huu unaonesha namna ambavyo waajiriwa akiwemo Mkurugenzi Mkuu, wakiwemo waajiriwa wengine wanavyotakiwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hapa ni mahali ambapo panaonesha wazi kwamba viongozi hawa wanatakiwa kuwa na kinga wanapoenda kwenye kazi zao. Hapo kwenye kinga nafikiri kila mmoja anaweza kuwa anafikiria itakuwaje kama hawa watu watakuwa wanakinga wakati wanakwenda kufanya hizi kazi. Nafikiri tumeangalia sheria mbalimbali ndani ya nchi hii, ambazo

sheria hizi zinaonesha kabisa kwamba kunapokuwa na *good faith* lazima kinga iwepo kwa sababu hawa watu wanaenda kufanya kazi ambazo zinawezekana zingine zikawa ni hatarishi, lakini zingine zikawa ni mahali fulani ambapo ni lazima wawe wamekingwa kwa sababu wanaweza kufanya kazi wakapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Sheria ya Dawa na Vitendanishi, Sura 219, kifungu cha 118 kinaonesha namna ambavyo huyu mhusika wa dawa hospitali anavyoweza kuwa amefanya kwa *good faith* hata kama likitokea tatizo asiingizwe kwenye matatizo ya *conviction* kwamba anaweza kufika mahali akashtakiwa mpaka pale itakapothibitika kwamba alifanya kosa yeye bila *good faith*.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sheria Tasnia ya Nyama ukienda kwenye Sura 421, kifungu cha 14, utakuta kitu kama hicho. Pia ukienda kwenye Sheria ya Viwango, Sheria Na.2 ya mwaka 2019, katika kifungu namba 33(1) napo utakuta vitu kama hivyo. Kwa hiyo utagundua kwamba sheria hii inatuonesha kwamba hawa vijana wetu akiwemo mpaka na Mkurugenzi Mkuu wanapokwenda kwenye kazi zao watakuwa *confident,* kwamba wanakwenda kufanya kazi, lakini sheria imewalinda kwamba hata kama wakipata matatizo kama wamefanya hii kwenye *good faith* ikithibitishwa na sheria, hawawezi kuingia kwenye tatizo.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwa haya machache ambayo nimeyaona, yako mengi ambayo tungeweza kuyapitia kuonesha ubora wa hiki ambacho kimefanyika kwenye sheria hii. Niwaombe sana Wabunge wenzangu tupitishe Muswada huu uwe sheria, ili watu wa Usalama wa Taifa wafanye kazi yao na nchi yetu iendelee kuwa salama. Mtakumbuka wazi ni Muswada huu unaoonesha wazi kwamba viongozi pamoja na kulindwa, kuna vituo ambavyo vitakwenda kulindwa, kuna maeneo yetu ambayo ni *very sensitive* yatakwenda kulindwa. Ni sheria hii inataja mambo haya. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tunapokwenda kufanya maamuzi, tufanye maamuzi Muswada huu uwe sheria ili uingie katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, cha pili, nataka kuzungumzia Tume ya Mipango. Tutakumbuka vizuri mwaka jana tulisema sana juu ya Tume ya Mipango kwamba kuna mipango mingine inagongana, kuna mipango mingine inafanyika leo baada ya wiki mbili inavunjwa na tukaomba ingekuja Tume ya Mipango. Ni kweli kwamba mwaka 2018 kulikuwa na uamuzi na ukabadilishwa, hatusemi ilivunjwa, ilibadilishwa na majukumu yake yakaingizwa kwenye Wizara ya Fedha, ikawa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, wenyeji wengi wa Dar es Salaam watakumbuka, inaweza ikajengwa barabara baada ya miezi sita wanasema inataka kuja mwendokasi. Barabara imejengwa miezi mitano nyuma, halafu inakuja mwendokasi wanabomoa tena katikati pale. Hii ni pesa ya Serikali. Sasa pesa ya Serikali ambayo unajenga leo halafu baada ya miezi sita unabomoa unasema tena kuna mwendokasi hapa, hiyo gharama ya kwanza inakwenda wapi? Kwa hiyo niwapongeze sana kwanza kwa kuja na mpango huu wa Tume ya Mipango, ambapo sasa mipango yetu itakuwa inajulikana, haitagongaana huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kwamba, tumesoma kwamba Tume ya Mipango inakwenda kufanya tathmini ya utekelezaji wa kile kilichofanyika kwenye Mpango unaokamilika mwaka 2025. Tutapata taarifa kutoka kwenye Tume ya Mipango hii, nini kimefanyika kwa miaka hii 10 iliyopita, ili tuweze kujizatiti wanapokwenda kutengeneza mpango mpya wa 2025 kwenda mwaka 2050. Vile vile imeonesha kwamba kutakuwa na mambo mahususi yanayoenda kusimamiwa na Tume hii. Tuliona wakati tunajadili Muswada huu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kifungu namba 16(1)*(c)* utaona kabisa Muswada huu ulikuwa umekuja na kwamba hawa watakuwa vilevile wanakwenda kukusanya mapato, lakini Kamati ilisema wazi hawa wajielekeze kwenye kufanya mipango ya Serikali, wasijielekeze kwenda kwenye kukusanya pesa, tutapoteza ile *focus* yetu ambayo tunataka sasa hivi Mipango ya Serikali ya muda mfupi na muda mrefu iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kama tutajikita na Tume ya Mipango itafanya kwa utaratibu wa sheria hii ninayoiona

hapa, Waheshimia Wabunge tuunge mkono Muswada huu wa Tume ya Mipango uweze kupita uwe sheria. Tuwe na Tume ya Mipango inayopanga mipango ya muda mrefu na mipango ya muda mfupi ili yale ambayo tumeyaona yanagongana, yakionekana Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, wanafanya kazi moja hiyo hiyo, wanajenga bwawa moja hayataonekana tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba Wabunge wenzangu waunge mkono, Miswada hii ambayo tumekuja nayo ili iweze kupata kibali cha Wabunge hawa na kuweza kuwa sheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengine. Tunao wanafunzi 85 na walimu 24 kutoka Shule ya Msingi Mikongeni ya Jijini Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge, maelezo niliyotoa kuhusu ile Shule ya Awali ya mfano, inawahusu wanafunzi hawa na siyo wale waliotoka, karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shabaan Taya na Mheshimiwa Omar Issa Kombo ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza sana maamuzi ya Serikali kwa ujumla wake. Mheshimiwa Rais na Serikali nzima na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamewasilisha Miswada. Pongezi vile vile ziende kwa Kamati ya Katiba na Sheria na hususani jinsi walivyojipanga hapa kuwasilisha Wajumbe watatu tofauti tofauti wakiongozwa na Mwenyekiti wametia fora, nawapongeza sana hongereni sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kurejesha upya Tume ya Mipango ni uwamuzi wa busara kubwa sana. Muswada huu wa Tume ya Mipango tukiupitisha, hatimaye ikawa Sheria, ndiyo unaenda kuanzisha Tume ya Mipango ya Tanzania. Ni jambo ambalo ni kubwa, ni la muhimu, ni la muhimu na jambo ambalo kila mtu

katika ukumbi huu na Watanzania kwa ujumla tunahitaji kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia kwa nini napongeza sana uammuzi wa kupeleka Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais na chini ya Uenyekiti wa Rais mwenyewe? Kiuhalisia katika familia zetu za kiafrika hata majumbani kwetu mara nyingi mkuu wa kaya ndio anakuwa Mwenyekiti wa mipango ya nyumbani pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji unaweza ukafanywa na wanafamilia kwa kuelekezwa na usimamizi wa mkuu wa kaya. Kwa hiyo hii Tume ya Mipango kuwa chini ya Ofisi ya Rais na Uenyekiti wa Rais wenyewe ni jambo ambalo ni la muhimu sana. Suala la kutenganisha idara ya, kuna taarifa?

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Prof. Mkumbo.

**TAARIFA**

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba hata mwaka 1962 wakati Mwalimu Nyerere anaanzisha Idara hiyo, alifanya hivyo na naomba nimnukuu; *"Nakusudia kuanzisha idara mpya, Idara ya Mipango ya Maendeleo. Idara hiyo itakuwa chini yangu mwenyewe"*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lile ambalo Muswada umependekeza ni sahihi na ilikuwa hivyo tangu awali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda uinapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na nampongeza sana kwa kunukuu hii aliyonukuu. Nilikuwa nasisitiza kwamba kutofautisha idara ya mipango na idara ya fedha tumefanya hivyo hata kwenye

Wizara. Huwezi kwenda kukuta kuna Wizara ambayo imeunganisha idara ya mipango na idara ya fedha ile ya uhasibu, hamna, ziko tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huku juu ndio kulikuwa na shida kidogo. Mheshimiwa Rais amerekebisha vizuri sana na kwa kweli ningependekeza kwa kweli tuharakishe kupitisha Muswada huu ili twende kurekebisha huko juu sasa mambo yawe mazuri zaidi.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa intokea sehemu gani? Sawa, Mheshimiwa Ally Kassinge.

**TAARIFA**

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji au mchangiaji kwamba hata muundo uliopo katika mikoa yetu kwa maana ya *Regional Secretariat* na Halmashauri zetu kwa maana ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Idara za Mipango na Idara za Fedha ziko tofauti na kwa maana hiyo kama tutakuwa na muundo huo kutoka chini mpaka juu litakuwa ni jambo jema zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napokea taarifa hizi. Hizi taarifa zinakuwa nzuri sana na zinachangia mchango wangu. Nashukuru sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 na ya 5 ndiyo hasa ambayo imejenga msingi wa mchango wangu na naziunga mkono na huu ndiyo msingi wa Tume ya Mipango kwamba Mheshimiwa Rais ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Tume na yeye atateua Wajumbe wengine sita kuingia kwenye Tume ya Mipango na hii itakuwa ndiyo msingi wa mipango yote katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naipongeza sana Kamati imefanya kazi nzuri sana ya kushauriana na Serikali na naipongeza

Serikali kuisikiliza Kamati. Maoni yetu mmeyasikiliza mengi kutoka kwenye Kamati na mengi mmeyazingatia, kwa hiyo kwa kweli nawapongeza sana wote ambao mmeshiriki katika kuujadili Muswada huu na hatimae kuuleta hapa. Kazi yetu sasa Bunge na ningependa nishawishi sana ni kupitisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango ili hatimae tuweze kufanya mapinduzi makubwa kwenye mipango yetu na tuweze kusonga mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, maeneo machache ya ushauri ambayo ningependa haya siyo kwamba yaingizwe kwenye Sheria hapana. Ningependa yazingatiwe wakati watakapokuwa wanaandaa Kanuni. Wazingatie mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza walizingatie baada ya mipango kuandaliwa inatakiwa iandaliwe mifumo ya utekelezaji wa mipango hiyo au *implementation of frameworks* ambayo ndiyo itatumika kurahisisha utekelezaji na kuandaa bajeti kwa uharaka zaidi hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili wazingatie kuweka utaratibu wa kushirikiana na Tume ya Mipango ya Zanzibar kwa sababu hii ni nchi moja. Kule Zanzibar kuna Tume ya Mipango, kwa hiyo Tume ya Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima kuwe na utaratibu wa namna ambavyo watashirikiana na wenzao wa Tume ya Mipango ya Zanzibar ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na mfumo mmoja wa maendeleo ya nchi. Lengo ni kupambana ni umaskini, ujinga na maradhi ambayo ni matatizo tunayopambana nayo tangu uhuru lakini bado yanatusumbua mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependekeza kabisa lizingatiwe ni kuweka utaratibu wa namna ambavyo Tume ya Mipango itashirikiana na Taasisi za Utafiti za Vyuo Vikuu vyetu vya hapa Tanzania na Vyuo Vikuu vya nje katika ku-*share experience* na tafiti mbalimbali. Vilevile namna ambavyo Tume ya Mipango itashirikiana na Taasisi za utafiti za binafsi hapa nchini kama *USRF* au *REPOA*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuweka utaratibu ambavyo Tume ya Mipango itashirikiana na taasisi za utafiti kwenye maeneo ya mitengamano kama Afrika Mashariki, *SADC, AU* na maeneo mengine yenye mitengamano. Nakumbuka mwaka 2004 tulikuwa tumekubaliana na nchi za *SADC* kwamba hapa Tanzania itaanzishwa *Poverty Observatory,* yaani ni mfumo wa kufatilia umaskini na Makao Makuu yalikuwa yawe Tanzania. Kwa hiyo hii ni miongoni mwa mambo ambayo ningependekeza Tume ya Mipango iyaendeleze lakini kupitia Kanuni nadhani mtaweka vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ambalo ningependekeza ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba *linkage* yaani wataalam kuanzia kwenye Halmashauri, Mikoa, Wizara, Mashirika, ni namna gani wataalam wa uchumi na mipango wana-*link* na Tume ya Mipango kama ilivyokuwa zamani. Kama ambavyo Wahandisi na Madaktari wana-*link* na Tume zao za kitaalam zilizoko Makao Makuu kwenye Wizara zao, hawa nao kama wataalam wa mipango na uchumi nao ni namna gani wana-*link* na Tume ya Mipango, ni muhimu sana kuweka utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa kweli nimeisoma Miswada yote mitatu. Nimeridhika sana na Miswada ile miwili, Muswada wa Usalama wa Taifa na Muswada wa Marekebisho Mbalimbali sina tatizo nao. Nilikuwa na maoni kwenye Muswada huu wa Tume ya Mipango na kwa kweli nilikuwa naomba sana, katika Miswada yote mitatu naona kama vile tumechelewa sana kuijadili na kuipitisha ni kama vile tumechelewa sana. Nilikuwa naomba sana nishawishi Wabunge wenzangu tuipitishe hii Miswada yote mitatu ili twende kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaabani Taya atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii ya kuchangia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa viumbe vyote ambaye amenipa uzima leo nasimama hapa mbele kuchangia Miswada muhimu mitatu katika nchi yetu, ambayo hii miswada inaenda kuleta mapinduzi makubwa katika Taifa letu katika nyanja ya maendeleo na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan sana kwa kufikiria kuleta Miswada ya aina hii ambayo sasa ameona ni namna gani inaweza kwenda kuchangia, kuchechemua maendeleo ya nchi yetu, lakini pia naomba nimpongeze kwa namna ambavyo anavyotembea usiku na mchana kwa ajili ya kutetea Taifa letu kuleta maendeleo na kusaidia jamii yake ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nikupongeze wewe kwa kuliongoza Bunge hili vizuri sana na kutupa sifa nzuri sana na keshokutwa hapo unaenda kuwa Rais, tunakuombea Mwenyezi Mungu akujalie uende kuwa Rais wa Bunge la Dunia. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu tunaamini uwezo wako, tunaamini kabisa umaridadi wako, tunaamini kabisa weledi wako, kwa hiyo tunaamini kabisa unaenda kuwa Rais mzuri sana wa Bunge la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia Muswada wa Tume ya Mipango. Katika jambo ambalo Bunge hili tunapaswa ku-*support* leo hii ni hii Tume. Haya yamekuwa malalamiko ya muda mrefu sana kwa Wabunge wengi ambao mimi nimesikia michango yao humu ndani. Wanasema uratibu hakuna kwenye Serikali, wanasema juu ya mipango, leo hii tunaweza tukajenga shule lakini shule haina labda madawati, shule haina walimu, shule haina vitendeakazi vingi tu, Muswada huu unaenda kusaidia tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaenda kusaidia tatizo la kukosa vifaa vya hospitalini. Leo hii tunajenga majengo lakini hatuna vifaa ni kwa sababu tunakosa mipango thabiti katika nchi

yetu. Leo hii Tume hii inaenda kusaidia upatikanaji wa vifaa vya hospitalini na upatikanaji wa vifaa vyote.

Mheshimiwa Spika, wakati mimi nasoma tulikuwa tunaambiwa sehemu ambayo tunataka tupeleke maendeleo, tupate mawasiliano, tupate maji, tupate umeme, tupate barabara nzuri. Nakumbuka tulikuwa tuna *point* zinasema *lack of infrastructure, lack of transportation* vitu vingi sana ambavyo tulikuwa tunajifunza mashuleni. Leo hii Tume hii inaenda kupanga mkakati mzuri sana. Tumeona barabara zetu watu wanajenga barabara baadae wanaenda kubomoa kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji. Tume hii inaenda kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, hii Tume imechelewa kuja kwa sababu tunaamini kabisa chini ya Mheshimiwa Rais hakuna Waziri atashindwa kupanga mpango mzuri wa watu wenye ulemavu. Tume hii inaenda kusaidia masuala yote ya watu wenye ulemavu. Tume hii inaenda kupanga mkakati mzuri wa watu wenye ulemavu wasaidiwe kwa namna gani katika nyanja ya elimu, katika nyanja ya afya, katika nyanja tofauti tofauti ya maendeleo na masuala mengine ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, Tume hii inaenda pia kusaidia kuna Sheria ya *PPRA* ya Manunuzi katika nchi hii, Wabunge wengi hawaifahamu hii sheria na hata watendaji wengine pia hawaifahamu hii sheria. Asilimia 30 ya manunuzi ya taasisi zote inatakiwa iende kwa makundi maalum. Sasa Sheria hii inaenda kusaidia utekelezaji wake wa hii Sheria, pia kusimamia Watendaji waweze kujua hii Sheria inapaswa kutekelezwa kwa namna gani. Kwa hiyo tunaenda kutengeneza mifumo mizuri ya utekelezaji, mifumo mizuri ya utendaji, kwa hiyo hii Sheria nawaomba Wabunge wenzangu leo hii tuipitishe kwa sababu ina umuhimu mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, hii Sheria jamani inaenda kusimamiwa na Mheshimiwa Rais na Mawaziri wawili ambao ni Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Leo hii, hii sheria inaenda kuwa na tija kwa namna moja ama nyingine katika jamii yetu katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie juu ya Sheria ya Usalama wa Taifa. Katika pita pita zetu huko mitandaoni kuna watu wanasema kwamba kwa nini hii Sheria watu wanaenda kulindwa, wale wagombea Urais. Serikali imejipanga vizuri kulinda amani ya Taifa hili. Hii amani tunayojivunia ni kwa sababu Usalama wetu wa Taifa wanatusaidia sana. Sasa leo hii Wagombea wa Urais wanaenda kuomba nafasi ya Urais walindwe na nani? Je, leo hii wakipata shida yoyote huoni kama italeta machafuko katika nchi yetu? Kwa hiyo Sheria hii inaenda kuleta wapate mamlaka ya kwenda kusimamia viongozi wote ambao wanaomba nafasi ya Urais ili waweze kulindwa, kushauriwa namna ya kujilinda na namna ya kulinda na wajumbe wao ambao wanaenda kuwapigia kura.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mtu alikuwa ananiambia kwamba hii Sheria inakwenda kuondoa madaraka ya Mheshimiwa Rais. *Guys* hii sheria inaenda kuongeza madaraka ya Mheshimiwa Rais. Ni nani ambaye anaweza kupinga mamlaka ya Mheshimiwa Rais wakati katika vitabu vyote vya dini vinatambua mamlaka za nchi, sasa ni nani ambaye anaweza kuondoa mamlaka ya Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, hii sheria inaenda kuongeza uwezo wa Mheshimiwa Rais kuchanganua mambo kuweza kulinda nchi yake vizuri, kuwasaidia Usalama wa Taifa vizuri, na Usalama wa Taifa wanaenda kumsaidia Mheshimiwa Rais katika mambo ya usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kusema hayo, naomba Bunge lako hili na Wabunge wako hawa, waweze kupitisha Sheria hizi tatu pamoja na Sheria ya Urekebu ambayo hii sheria ni muda mrefu sana miaka kadhaa haijafanyiwa marekebisho na leo hii tunaenda kufanya marekebisho ya Sheria hii ambayo inaenda kuleta mapinduzi ya kubadilisha Sheria mbalimbali za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kusema hayo machache naomba niunge mkono hoja wa Miswada hii mitatu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Issa Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia Miswada hii ya Sheria ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla tumuombee kwa Mungu Mheshimiwa Spika wetu ili Mwenyezi Mungu amjalie aweze kufanikiwa katika safari yake ya kuwania Urais katika Mabunge ya Dunia. Kwa nini ninasema kwamba tumwombee ni kwa sababu pindi Mwenyezi Mungu atakapomjalia kupata nafasi hii anakwenda kulitangaza Taifa letu na anakwenda kutuheshimisha kama Taifa, kwa hiyo tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu akujalie ili uweze kufanikiwa katika nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Dkt. Samia suluhu Hassan kwa kuleta Muswada huu au kwa kuleta Miswada hii. Miswada hii kwa kweli inakwenda kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mara nyingi tumekuwa tukizililia hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa nini nampongeza Mheshimiwa Rais kwenye Muswada huu wa Tume ya Mipango kwa kweli unadhihirisha ni kwa jinsi gani Mheshimiwa Rais anaonesha dhamira yake ya kuweza kulipeleka mbele Taifa letu, kwa sababu kama Taifa hatuwezi kusonga mbele bila kuwepo na mipango lakini vilevile utekelezaji na kufanya tathmini juu ya utekelezaji wa mipango hii. Kwa kweli Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango. Kama walivyotangulia kuzungumza Wabunge wenzangu hapa kwamba Tume hii ilikuwepo tokea kipindi cha uhuru mwaka 1961 lakini imekuwa ikija katika sura tofauti tofauti. Kwa kweli kuwepo kwa Tume hii ya Mipango au

kitendo cha Mheshimiwa Rais kurejesha tena Tume hii ya Mipango maana yake kwanza inakwenda kuipa zaidi Bunge jukumu lake la kuisimamia Serikali katika mipango ya maendeleo, kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 63(3)(c) ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba Bunge miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia mipango ya maendeleo. Kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba tulikuwa tulikuwa tukilalamikia kwamba kutokuwepo kwa Tume hii ya Mipango vilevile kulikuwa kunapelekea ufanisi mdogo wa usimamizi na utekelezaji. Kama tunavyokumbuka kwamba kwa sasa upangaji wa mipango na utekelezaji uko kwenye Wizara ya Fedha na kama tunavyokumbuka kwamba jukumu la Wizara ya Fedha na kwenda kuongezea tena mzigo wa upangaji wa mipango wa maendeleo na utekelezaji na usimamizi kwa kweli inapelekea ufanisi mdogo sana wa utekelezaji wa mipango yetu ya nchi. Sasa Serikali inapoleta Sheria hii maana yake sasa tunakwenda kutofautisha mipango, usimamizi pamoja na Wizara ya Fedha, maana yake sasa usimamizi wa mipango yetu na utekelezaji itaweza kwenda kusimamiwa kwa ufanisi mkubwa zaidi tofauti na sasa ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna tafiti mbalimbali zilifanyika mwaka 2022 zilionesha kwamba kutokana na wingi au ukubwa na uzito wa majukumu ya Wizara ya Fedha inapelekea usimamizi wa Tume hii ya Mipango na mipango ya nchi kutokuwa na ufanisii wa juu zaidi. Sasa Serikali inapoleta Sheria hii ya Tume ya Mipango maana yake sasa mipango yetu itakwenda kutekelezeka vilevile pia kufanyika kwa tathmini jinsi gani mipango yetu itakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, jirani yangu hapa Mzee wangu Kakunda ameelezea juu ya ushirikishwaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar. Kama tunavyofahamu kwamba Zanzibar kwa upande wetu na sisi iko Tume ya Mipango ambayo mfumo wake ni sawa na huu ambao unataka kuanzishwa ambapo Mwenyekiti wake anakuwa ni Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata ukiangalia baadhi ya majukumu ya Tume ukiangalia kama vile yanashabiana au yanakwenda kugusa vipengele vya Muungano. Kwa mfano, kwenye Ibara ya 6(2)(g) inasema kwamba miongoni mwa majukumu ya Tume kutoa mwongozo kuhusu uchumi kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa. Tunapozungumzia nchi nyingine na mashirika ya kimataifa maana yake tunakwenda kugusa suala la Muungano, kwa hiyo niombe Serikali kwamba iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba inaishirikisha Tume ya Mipango ile ya Zanzibar ili tuende pamoja kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kwamba nchi yetu ilivyoingia katika uchumi wa kati mwaka 2020 ilijumuisha pia Zanzibar, kwa hiyo ili kwenda pamoja ni vyema kuwepo kwa ushirikiano wa mara kwa mara kati ya Tume hii ya Tanzania Bara na Tume ile ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kutoa mchango wangu katika suala la Tume hii ya Mipango. Vilevile niseme kwamba matarajio yetu baada ya kupitishwa kwa Sheria hii nini tunatarajia? Kwanza ni Wizara zote za kisekta kuwa na utaratibu wa kupanga kwa pamoja. Tumeona imekuwa ni kawaida kila Wizara inajipangia mipango yake ya maendeleo na hivyo kupelekea gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Leo Mheshimiwa Kairuki au Profesa Mbarawa anajenga barabara kesho Mheshimiwa Juma Aweso anakwenda kukata barabara anapitisha miradi ya maji. Hii inapelekea matumizi mabaya ya fedha za umma. Kuja kwa chombo hiki cha Tume ya Mipango maana yake sasa tutaweza kutumia vizuri rasilimali zetu za Taifa na hivyo kupelekea kasi ya uchumi katika maendeleo na maendeleo endelevu katika Taifa letu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitishwa au kuundwa kwa Tume hii itakwenda kuongeza ushiriki na ushirikishwaji wa sekta binafsi. Kama tunavyoona kwamba kwa sasa kila sekta inajipangia mipango yake ya maendeleo lakini hata ushiriki na ushirikishwaji wa sekta binafsi unakuwa ni mdogo sana au unakuwa haupo katika hali ya ufanisi zaidi lakini kuwepo kwa Tume ya Mipango

maana yake sasa ushirikishwaji na ushiriki wa sekta binafsi utakwenda kuwa mkubwa zaidi na wa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nigusie katika Sheria hii ya Usalama wa Taifa. Niwaombe Wabunge wenzangu kwamba tuzipitishe sheria hizi na lengo la kuletwa Muswada huu wa Sheria ni kwenda kuongeza hali ya usimamizi wa Usalama wa Taifa letu. Kama tunavyoona kwamba chombo hiki ni chombo muhimu sana kwa maslahi ya usalama wa Taifa letu, hivyo inavyokuja Sheria hizi maana yake tunakwenda kuweka Taifa katika hali nzuri zaidi ya kusimamia usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuzipitishe kwa moyo mmoja Sheria hizi kwani zinakwenda kuleta hali ya mabadiliko makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami napenda kutoa shukurani za dhati kwa kunijalia wasaa kusema machache, kujadili Miswada hii nyeti kabisa ambayo iko hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ikiongozwa na Mawaziri wote watatu ambao wanakwenda kwenye maudhui ya Miswada hii, kwa ushirikiano wao mkubwa sana. Hakika kipindi hiki tulikuwa na kazi nyingi sana, tumepitia sheria nyingi mno, lakini kazi zetu zimekuwa nyepesi kwa sababu ya ushirikiano mkubwa. Nasemea Kamati kwa ujumla kwamba, *responsiveness* ya Serikali na usikivu mkubwa wa Serikali umefanya kazi yetu kuwa nyepesi, tumeimaliza na tumefikia muafaka katika sheria zote ambazo tunazijadili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuweka maoni yangu katika sheria zote, lakini sina hakika kama muda utaniruhusu. Napenda kuanza na Sheria ya *TISS*. Kwa ujumla wake Sheria hii ukiitazama kwa mawanda mapanda, inarasimisha kazi ambazo tayari zilikuwa zinafanyika katika Idara ya *TISS*. Kwa mapana yake, hakuna mambo mapya ambayo yanafanyika katika sheria hii, imerasimisha yale ambayo tayari yamekuwa yakifanyika. Kila jambo likifanyika hivyo, linawekewa *framework* ya jinsi gani utendaji kazi unakwenda.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kuna mambo makuu matano ambayo napenda kuyagusia kwa sababu yamekuwa yakigusa hisia za wadau. Pia, kama mwenzangu alivyosema, ili uifahamu vizuri sheria hii, lazima uzisome sheria mbili; hii ya leo na ile ya mwaka 1996, zina-*inform*. Kuna maeneo ambayo bila kuangalia sehemu zote mbili inaweza ikaja kukuvuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nini ambacho kilikuwa cha msingi na kinazungumzwa sana na watu kuwa na hofu ambapo kwa haki hakuna sababu ya kuwa na hiyo hofu? Kwanza ni kwamba, unyeti wa taasisi hii ni wa msingi mno kwa ajili ya usalama na ustawi wa Taifa letu. Haiwezekani usalama wa Taifa ukawepo bila taasisi hii kuwa na majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza taasisi hii kupitia sheria hii, kwanza imerasimisha kazi zake; pili, iko chini ya Ofisi ya Rais moja kwa moja. Sasa, mambo yapi ambayo ningependa kuyagusia moja baada ya lingine ambayo yamewekwa bayana na yako vizuri katika sheria hii? La kwanza linalozungumzika, kuhusu usimamizi na *oversight* ya taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *TISS* kwa unyeti wake ina *oversight function* ya sehemu mbalimbali. Kwanza ni hii Kamati yetu. Katika masuala ya sera na bajeti ambayo amekabidiwa kwa Mheshimiwa Waziri, yatapita kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Pili, sehemu kubwa ya *oversight* katika sheria hii imeweka bayana, ni Rais mwenyewe na Tassisi ya Urais yenyewe. Tatu, ni Katibu Mkuu Kiongozi, naye sheria hii imeainisha sehemu yake ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, eneo la *oversight* na kwa sababu ya unyeti na mambo mengi yanayoendelea, Waheshimiwa Wabunge lazima tujue kuna siri na kuna mambo nyeti ya Taifa na Mataifa yote ambayo hayawezi yakawa wazi. Hata hivyo, katika *section* ya *oversight* ukiangalia sheria, Rais, Katibu Mkuu Kiongozi, *DGIS* yeye mwenyewe na Kamati hii, *oversight function* ipo.

Mheshimiwa Spika, lingine, kulikuwa na mazungumzo kuhusu *security of tenure* ya *DGIS* kwamba akiingia hatoki. Siyo kweli. Sheria inasema bayana, *DGIS (Director General of Intelligence) ata-serve at the pleasure of the President*. Hiyo iko wazi. Hilo nalo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu. Kuhusu suala la *immunity from Criminal prosecution*. Ukiipitia sheria yote hii hakuna sehemu yoyote ambayo inasema hivyo. Kuna *mistakes done in action and omissions in good faith,* ambayo *professional* yoyote Tanzania, hiyo *omission* anayo. Ukienda kwa Daktari ipo, kwa Mwanasheria ipo, ukienda kwenye taasisi za kawaida *omission* hiyo ipo. Sasa hofu hiyo tusiwe nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ripoti za *CAG,* zimezungumzwa vile vile. *CAG Act* ndiyo ina-*decide* kitu gani kitafanyiwa ukaguzi wa *CAG*. Hakuna sheria yoyote ambayo inasema lazima taasisi hii ikaguliwe na *CAG*. Sheria ya *CAG* iko bayana, anaweza kukagua Serikali nzima na kwa utaratibu gani, itajulikana huku. Tusiwe na wasiwasi, sheria hii imepitiwa, tumeijadili kwa kina, maoni mengi ya wadau ambayo yalikuwa na mashaka yamewekwa wazi na sheria hii iko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaambia ndugu zangu kwamba, kwa mazungumzo ya Kamati na Serikali, tumepata muafaka na sheria hii iko salama.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuzungumzia suala la Tume ya Mipango. Niguse tu kwa muhtasari. Nimekuwa nikimsikiliza ndugu yangu Mheshimiwa Askofu Gwajima akizungumza sana kuhusu mipango iwe endelevu. Sheria hii kwa mawanda yake tena mapana, imefanya mipango yetu kwanza

iwe *specialized* kwamba kuwe na utaalam, na pili, iwe endelevu. Hakuna kitu katika nchi ambacho kinaweza kikafungwa kisibadilike milele. Vilevile sheria hii imefanya mipango isiwe rahisi kubadilishwa kwa wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi hicho ndicho kilikuwa kilio chetu kikubwa sana ndani ya Bunge hili, kwamba mipango inatumia gharama kubwa, inatumia watu wengi na muda mrefu sana, lakini inaweza ikabadilishwa haraka. Sheria hii ndiyo mwarobaini wa hilo tatizo. Inaweza kubadilishwa lakini kwa hatua ambazo zimewekwa bayana kwenye Katiba na Sheria hii kama alivyozungumza Mheshimiwa Kisau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli napenda kutumia fursa hii kuishukuru Serikali kwa maono hayo yaliyotuletea hii Sheria. Napenda kuwaambia Wabunge tuiunge mkono hii sheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, katika Sheria ya Urekebu kulikuwa kuna sheria ambayo tuliipitisha kwenye Bunge hili ambayo ilifanya sheria zetu zisomeke na ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili. Katika mazungumzo yetu huko kwenye Kamati, tulikubaliana kwamba sheria hizi zote zisomeke kwa lugha zote mbili; Kiingereza na Kiswahili. Tanzania ni nchi ya lugha mbili; Kiswahili na Kiingereza. Hapa Bungeni tunaweza ku-*debate* kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili, kanuni ziko wazi. Mashuleni kwetu tunasomeshwa *Primary* Kiswahili, Sekondari na Vyuo Vikuu Kiingereza na mfumo wetun a mitaala yetu yote iko hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nashukuru katika Sheria hiyo ya Urekebu imesahihishwa kwamba sheria zetu zote lazima ziwe *published* kwa lugha mbili (Kiswahili na Kiingereza). Tuipongeze sana Serikali kwa hilo. Sababu kuu ya hilo ni kwamba sisi ni nchi ambayo tuko katika sehemu ya nchi za Jumuiya ya Madola. Nchi za Jumuiya ya Madola tunafuatilia masuala ya kisheria ya *Commonwealth.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, nimekuona na ninakushukuru kwa kunipa wasaa wa ziada. Naunga mkono hii

hoja. Napenda kuwaambia wenzangu wote kwamba sheria zote ziko salama, tumezichambua kwa kina na tuziunge mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda huu wa kuchangia. Kwa makusudi ya kuokoa muda, nataka nikimbie haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassa, nashukuru Kamati zote za Bunge ambazo zimechakata Miswada hii na kutufikisha mahali hapa tulipofika.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana napenda kuchangia Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango 2023. Nimefurahi sana kwamba Muswada huu au sheria hii itakapotungwa itaipa Tume hii majukumu 19, lakini siwezi kuondoka kabisa bila kugusa Muswada wa Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, niseme machache tu kwenye huo Muswada wa Sheria ya Usalama wa Taifa. Nchi imara yoyote duniani inaanza na shirika la kijasusi imara. Mojawapo ya kazi ya idara ya usalama ni kukusanya taarifa, kuchakata taarifa na kuzipeleka kwa walaji ili walaji wa taarifa waamue kwa wakati na waamue kwa usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mlaji mkuu wa taarifa Idara ya Usalama wa Taifa ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tulichelewa sana kuihamisha idara hii na kuileta kwenye Ofisi ya Rais, mahali ambapo mlaji mkuu wa taarifa apate taarifa za moja kwa moja. Kwa hiyo, sheria hii inarahisisha sana kazi ya watu wa Idara ya Usalama wa Taifa kumkabidhi mlaji mkuu wa taarifa hizi kwa haraka na kwa usahihi. Ahsante sana kwa Kamati yako kuleta huo Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jambo la pili, ambalo nafikiri ni la muhimu sana, katika kukusanya taarifa popote pale na kuzichakata kuna hatari. Kuna mtu mmoja alisema, kanuni ya kukusanya taarifa ni kwamba lazima taarifa ipatikane kwa ubaya au uzuri, asubuhi au jioni, mchana au usiku, kwenye harusi au msibani. Katika kukusanya taarifa, wakusanya taarifa hawa wanaweza kukutana na shuruba mbalimbali. Kwa hiyo, vifungu vyote ambavyo Kamati ya Bunge imependekeza katika kujaribu kuwalinda hawa wakusanya taarifa, ninazi-*support* asilimia 100, na zilichelewa tu kuja kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, pia sheria hii imechelewa sana. Nashukuru sana Kamati ya Bunge kwa kufanya haya mapema.

Mheshimiwa Spika, niongee kwa uchache sana kwa habari ya Tume ya Mipango ya Taifa na huu Muswada wa Tume ya Mipango ya Taifa. Tangu niingie kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila nilipopata nafasi ya aina yoyote, nilizungumza kwa habari ya Tume ya Mipango ya Taifa. Nini maana ya mipango ya Taifa? Mipango ya Taifa maana yake ni mwelekeo wa Taifa, ni agenda ya Taifa, ni Dira ya Taifa na ni kesho ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi Mhubiri wa Injili, ninukuu Kitabu cha Hosea Sura 4:6 kinachosema "pasipo maono watu huangamia." Isaya 5:13 inasema, *"My people have gone to captivity because of lack of vision."* Yaani, utumwa unakuja kwa kukosa mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi zote za kiafrika ziko kama zilivyo kwa sababu zilikuwa hazijafika mahali zikaichukua hii agenda ya maono ya muda mrefu kuwa *priority* katika Taifa. Namshukuru Mheshimiwa Rais chini ya Mawaziri wake ambao wameamua kulitengeneza Taifa kwa kuipa agenda ya muda mrefu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni ulinzi wa Mipango ya Tume hii. Tutafanyaje ili tume hii na mipango iliyopangwa iwe *implemented* na kila *regime* itakayoingia madarakani? Hiyo ni changamoto na ni lazima tuiangalie sana. Kwa mfano, chaguzi zinapoanza kila chama kinaandaa ilani ya uchaguzi. Nashauri

ilani ya uchaguzi wa chama chochote ni muhimu *i-comply* na mpango wa Taifa wa muda mrefu. Maana yake, ilani ya uchaguzi kabla haijaanza kunadiwa (Ilani ya Uchaguzi ni Mkataba kati ya wananchi na chama husika). Chama hicho kikichukua madaraka, ilani hiyo ndiyo inakuwa mpango unaotekelezwa ndani ya miaka mitano ya uhai wa Serikali hiyo. Ni muhimu sana kila chama kinapoanza mchakato wake wa kutengeneza ilani, ilani zake zikaguliwe kwanza na Tume ya Mipango ya Taifa ili chama hicho kikiingia madarakani, kiweze kutekeleza Mpango wa Taifa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niongee ni ushauri kwamba tusifanye mipango ya miaka 15 au 20, tufanye mipango ya miaka 50 na kuendelea. Mipango hii inaweza kuwa *reviewed* kulingana na dunia inavyobadilika na uhitaji wa nchi unavyobadilika. Tuwe na mipango ya miaka 50, miaka 100 na kuendelea. Katika kutimiza azma hii ya mipango, tuepuke sana kuwa na msururu wa matukio yanayotokea kwa mwendelezo, tukafikiri hiyo ndiyo mipango.

Mheshimiwa Spika, mipango ni nini? Mipango ni lazima tuwe na kundi la watu wa Tanzania wenye kuiona kesho inapoelekea, wawe na uwezo wa ku-*forecast* miaka 50 ijayo ya dunia na watafute mipango itakayo-*position* nchi yetu mahali salama ili iweze kupanda kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwenye hii Tume ya Mipango kuwe na kitengo cha kufanya *analysis* ya mambo yanayotokea duniani kiuchumi, ki-*medicine,* kijeshi ili hii idara itakayokuwa kama *analysis brain* ya hii mipango iweze ku-*analyze future*. Kwa mfano, tunaona kuna vita kati ya Ukraine na Moscow, Tume hii inatakiwa ku-*foresee,* vita hii itazaa nini baadaye na Taifa letu litakuwa kwenye *position* gani baada ya vita hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuna hzi nchi za *China, Moscow, India, Brazil, South Africa* ambao wanatafuta kutengeneza *currency* yao, na wako mwishoni. Dunia inakokwenda, hatutatumia *swift* kupitia *New York,* inawezekana kuna namna nyingine ya ku-*transfer* fedha duniani, ikabadilika. Tume ya Mipango lazima iwe na *brain* ya ku-*foresee* dunia mpya

itakapozaliwa, mahala ambapo *swift* haiendi *New York* tena, Tanzania itakuwaje? *So,* hii ni *vision* ya nchi, mipango ya nchi na mwelekeo wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunaweza kusema kwa ufupi, ndani ya miaka 30 nchi yetu kila wilaya iwe na hospitali ya rufaa, ndani ya miaka 30 nchi yetu kila wilaya iwe na *university,* ndani ya miaka 30 nchi yetu pasiwe na nyumba ya Mtanzania ya majani au ya matembe kama ndugu zangu Wagogo, ndani ya miaka 30 kila nyumba ya Mtanzania iwe na maji safi na salama. Sasa kila *regime* inapokuja madarakani, inafanya bidii kutimiza mpango huu. *Regime* yoyote itakayoshindwa kutimiza mipango tuliyojiwekea kama Taifa, *regime* hiyo itakuwa imeshindwa kuiendeleza nchi sawa sawa na mipango ya nchi. Kwa muktadha huo, hatuhitaji Rais mwenye maono, tunahitaji nchi yenye maono ili Rais atakayeingia afuate maono yetu tuliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuwa na *worry* sana kwa sababu demokrasia ni namna ya wengi kupata utawala. Kuna wakati demokrasia huwa zina-*manufacture* watu tusiowategemea. Mussolini alishinda kwenye uchaguzi, Hitler alishinda kwenye uchaguzi lakini kulikuwa hakuna *tools* au maono ya kuwaongoza kubaki katika mpango wa Ujerumani, wakaingiza dunia kwenye matatizo. Nasi lazima tuwe na *break,* tuwe na *governing machinery* ya kuiongoza Tanzania kupitia Tume ya Mipango ambayo ni maono ya nchi, uelekeo wa nchi na hapa naiona Tanzania mpya inakuja kama tutaweza kuishika hii mipango na kuifuata. Naam, Tanzania mpya inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nami nichangie Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, lakini mimi nitajikita zaidi kwenye ule Muswada wa Mapendekezo ya Sheria ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana na kukupongeza kwa kusudio la kugombea nafasi ya Rais wa *IPU*. Mimi nafikiri utashinda, nina hakika kwa kaliba yako, taaluma yako na uwezo wako unaojionesha, Mungu atakutangulia na utashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli kwa kuleta Muswada huu ambao utasaidia sana Idara ya Usalama wa Taifa kufanya kazi zake kikamilifu. Muswada huu ukipitishwa na Bunge lako Tukufu utaleta maboresho makubwa ya kiutendaji kwa Idara ya Usalama wa Taifa lakini pia Sheria inayopendekezwa italeta tija kwa wafanyakazi Maafisa wa Idara ua Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa na muhimu ya Idara ya Usalama wa Taifa yameendelea kulifanya Taifa hili liwe na amani na utulivu lakini kukuza uchumi kwa miaka mingi hawa watu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huko nyuma kelele mnazopiga zinafika kiula mahali. Ahsante sana, Mheshimiwa Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, Idara imezuia matukio makubwa ambayo yamezima chini kwa chini kama ilivyo kazi yao ya *secret* na sisi raia hatukujua matukio gani yametokea lakini mengine yalikuwa bayana kama Mapinduzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa itaziba mapungufu hayo yaliyokuwepo katika Sheria ya sasa. Hata hivyo naomba nipendekeze na mimi niweze kuchangia marekebisho ya vifungu vifuatavyo;- kifungu namba 24(1) kinachoweka zuio la watu walistaafu kuongelea mambo ya Idara kutoa taarifa za Idara kifungu hiki kitaimarisha sana usiri wa Idara lakini pia kuficha na kuwazuia watu wanaojifanya watu wa idara walifanya kazi zamani kusema mambo ya Idara na sasa Mkurugenzi Mkuu atakuwa na udhibiti huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maoni mengine pia katika maboresho ya Kifungu cha 25 kinachozuia kuweka zuio la kuingia

katika maeneo ya Idara ya Usalama wa Taifa. Maoni yangu ni kwamba masharti hayo ya kifungu hicho yangeongezwa kujumuisha pia mazuio ya kupiga picha au kuchora maeneo hayo kwa mkono au kwa njia yoyote ile kijiti au kifaa kingine chochote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia malengo ya marekebisho ya Muswada huu kwamba ni kuleta usawa wa mifumo ya kiutendaji sawa na Idara za Kimataifa Duniani lakini kuboresha na kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwepo katika Sheria iliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia Idara hii kuwa chini ya Rais kwa sababu hii itampa nguvu Mheshimiwa Rais kuisimamia vizuri Idara hii lakini Mkurugenzi Mkuu atakuwa na nguvu zaidi kuliko ilivyo sasa kupitia kwa Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia marekekbisho ya kifungu cha 10 ili kumtambua Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa kwamba ndiye mtaalam anayeweza kumshauri Mheshimiwa Rais na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Usalama wa Taifa na huyu *actually* ndiye mtaalamu namba moja wa masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia mapendekezo ya kuwalinda Maafisa wa Idara wanaofanya kazi baada ya kustaafu na wakiwa ndani katika madaraka yao kwa kazi wanaiyoifanya au kwa makosa yatakayotokana na utendaji wao wa kazi. Hii itawapa nguvu Maafisa hawa kufanya kazi kwa nguvu wakiwa na imani kwamba hawatadhurika baada ya matendo yao mazuri yaliyofanywa kwa uaminifu mkubwa kulinda nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana kuniruhusu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae.

**MHE DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia pia ninakuombea kila la kheri katika kupambana kupata nafasi ya Urais wa Bunge la Dunia, Mwenyezi Mungu akutangulie.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuja na Muswada huu muhimu sana wa Sheria ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inaenda kuanzisha Tume ya Mpango ambayo Tume hii itakuwa na mamlaka kubwa ya kusimamia masuala yote yanayohusu Mipango ya Maendeleo ya Taifa letu. Lakini nchi nyingine zote duniani zimekuwa na mifumo mbalimbali ya kisheria, ya kitaasisi ya kusimamia mambo haya ya Mpango wa Maendeleo. Nchi nyingi duniani Amerika ni mojawapo na nyingine nyingi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge jambo hili ni muhimu sana na siyo geni.

Mheshimiwa Spika, Katiba yatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 63, imetoa maelekezo, imeainisha kwamba kuna nia na makusudi ya kuandaa mpango au kuandaa Tume ya kuandaa Mpango wa Maendeleo. Si hivyo tu hata Sheria ya Bajeti Sura namba 439 imeweka mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi na upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Kwa hiyo jambo hili lina baraka zote.

Mheshimiwa Spika, tunajua kabla na baada ya Uhuru kumekuwa kuna chombo cha namna hii cha kusimamia mambo ya Mipango ya Maendeleo. Toka tulipopata Uhuru mwaka 1961 mpaka mwaka huu kumekuwa kumeundwa na vyombo mbalimbali vyenye majina mbalimbali vyombo 11. Vyombo vitano vyote vilivyoundwa toka kupatikana kwa Uhuru vilikuwa chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa ni Mwenyekiti. Kati ya vyombo 15 ambavyo yamesimamia Mipango ya Maendeleo kwa Taifa letu toka tupate Uhuru vitano vyote vilikuwa chini ya usimamizi Rais kama mwenyekiti na kiongozi, vitano vingine vilikuwa chini ya Waziri kwa maana wizara husika ni kimoja tu kilikuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo,

vyombo 11 vimekuwepo toka tupate Uhuru vikisimamia suala zima la kusimamia Mipango ya Maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, chombo cha sasa hivi ambacho sasa hivi inaendakuundwa Tume hii. Tume ya Mpango inaenda kuundwa kisheria tofauti ni tofauti kabisa inaenda kuundwa kisheria japo taasisi zilizopita zilikuwa zina faida kama zilizopita zimetiletea tumekuwa kundi lenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati, cha chini mwaka 2020, kwa hiyo zimekuwepo zikifanya kazi nzuri ila sema zimeelemewa. Kwa hiyo, umuhimu wa kuanzisha Tume kisheria inayofanya kazi peke yake ni muhimu sana si kama zingekuwa hazifanyi kazi ila zimeelemewa kwa hiyo utendaji unakuwa siyo wenye tija sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tume hii inayoenda kuanzishwa au tume pendekezwa inaweza kwenda kutokana na Sheria ya Tume ya Mipango ya 2020/2023 inaenda kuandaa, kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa. Lakini si hivyo tu iko thabiti ina Idara mbalimbali ambazo zitakuwa chini ya Manaibu Katibu Wakuu Watendaji kama ambavyo imeainishwa kwenye Sheria. Kutakuwa na Idara ya Sekta Binafsi ambayo mwanzo haikuwepo, tulikuwa hatuhusishi Sekta Binafsi katika kuandaa mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe *credit* kubwa, lakini si hivyo tu kutakuwa kuna Idara mahususi kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya ubunifu na utafiti kabla ya kupanga mipango. Hii nayo itakuwa chini ya Naibu Katibu Mkuu anayejitegemea. Lakini si hivyo tu kutakuwa na Idara ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji ili kuona mpango una tija? Nilikuwa nauliza wenzangu lazima kuwe kuna Idara mahususi ya ufuatiliaji na tathmini ya je, mipango tunayoifanya inaleta tija? Sasa itakuwepo chini ya Naibu Katibu Mkuu wa Idara hii. Lakini si hivyo tu kutakuwa kuna Idara ya kusimamia maeneo ya vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwenye Muswada, Muswada pendekezwa huu wa Tume ya Mipango kwenye Ibara ya 4 sehemu ambayo inaonyesha kuanzishwa kwa Tume Ibara ndogo ya pili ina sema hivi "Tume itakuwa ni Idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais" imeeleza bayana.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu kama Kamati katika Muswada huu tulishauri mabadiliko kadha wa kadha mabadiliko katika Ibara ya 3, Ibara ya 5, Ibara ya 7, Ibara ya 8, Ibara ya 11, Ibara ya 12, Ibara ya 14, na Ibara ya 21. Kwa kweli Serikali imetupa ushirikiano imeenda kurekebisha imekuja kwenye jedwali la marekebisho ambalo imelisoma pamoja na Muswada kwa mara ya pili. marekebisho yote yamewekwa, imetupa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitasoma marekebisho moja tu ambalo sisi tumeona ni muhimu na hakika hili tumepata kama Kamati ni kwamba katika Ibara ya 6 sehemu ya pili ya Muswada huu ambayo inaeleza majukumu ya Tume ambayo ni *around*19 lakini likuwa na Ibara ndogo tatu tu sisi tukapendekeza kama Kamati kuwe na Ibara ya 4 ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nisome katika Muswada. Ibara ya 7(4) inasema "mpango wowote wa muda mfupi au wa muda mrefu ulioandaliwa kwa mujibu wa Sheria hii au Sheria nyingine iliyotungwa na Bunge au kuidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya Katiba hautabadilishwa au kuacha kutekelezwa katika muda uliopangwa kutekelezwa bila idhini ya Bunge". Tunaipongeza Serikali imekuja na badiliko hilo imeridhia na imeingia kwenye Muswada wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashauri Bunge na Wabunge wenzangu Muswada huu ni mzuri sana, ni Muswada wenye faida wenye *vision* ya Taifa kama walivyotangulia kusema wenzangu. Kwa hivyo kwa Sheria hii mahsusi inayoanzisha Chombo cha Kitaifa cha kusimamia kuratibu uaandaaji, kutekeleza mipango ya Taifa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashauri pia Wabunge wenzangu waunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge tunaongeza nusu saa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie Miswada hii mitatu ambayo imeletwa mbele ya Bunge letu leo tuweze kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada unaohusiana na Tume ya Mipango. Nina mambo mawili ninataka kushauri kuhusiana na Tume ya Mipango pamoja na uzuri wake na Muswada wake kuwa mzuri nina mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kuhusiana na kifungu cha tano cha Muswada ambacho kinasema "Mheshimiwa Rais ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango". Ukisoma kifungu cha tano ambacho kina mruhusu Mheshimiwa Rais kuwa Mwenyekiti ukaenda kusoma kifungu cha saba cha Muswada pamoja na maneno mengine wanasema Tume hii ya Mipango ndio itakuwa chombo cha juu cha ushauri kinacho wajibika kwenye Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ufahamu wangu mdogo Mheshimiwa Rais anaelekeza hawezi kushauri, akisema ni malekezo ni lazima yafanyike. Ukisema kwamba Tume ya Mipango ambayo Mheshimiwa Rais ndio alikuwa Mwenyekiti wakatengeneza mipango ndio inaenda kushauri kwenye Baraza la Mawaziri maana yake kila kitu lazima kifanyike. Kwa mantiki hiyo ni kwamba kama Tume ya Mipango kuna makosa au kuna mambo madogo ambayo yanatakiwa yafanyiwe marekebisho Baraza la Mawaziri litakosa *mandate* ya kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa minajiri hiyo, ninashauri kuweka kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Rais ni jambo jema lakini tungetengeneza mamlaka kamili ambayo inakuwa na Kurugenzi zake ambayo kazi yao ni kutengeneza hiyo mipango watakuwa na wataalam na watamshauri Mheshimiwa Rais na hawa watakuwa kama ni timu ya wataalam ambao pia itakwenda kufanya mawasilisho kwenye Baraza la Mawaziri na kulishauri Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo naungana kabisa na hoja ya Tume ya Mipango lakini kumuweka Mheshimiwa Rais kama Mwenyekiti naona kidogo inaleta ukakasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusiana namna hii Tume ya Mipango ilivyotengenezwa. Nashauri ili mipango iweze kupangwa vizuri kama walivyosema Wabunge wenzangu ni lazima sekta zote na wadau wote waweze kushirikishwa bado sijaona ushiriki wa Sekta Binafsi kwenye Tume hii ya Mipango na wote tunakubaliana kwamba mipango mingi inayotekelezwa mingi inahusisha Sekta Binafsi. Kwa hiyo, hilo ningetamani sana liweze kuzingatiwa katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine niende kwenye Sheria ya Usalama wa Taifa. Sheria ya Usalama wa Taifa imefanyiwa marekebisho lakini niseme tu mambo mengi ambayo yameletwa kwenye Sheria hii yanafanyika tayari huko mtaani. Kwa mfano wameweka kifungu kinachoruhusu wastaafu wa Usalama wa Taifa.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatoka wapi? Anhaa Mheshimiwa Gwajima, kwa sababu mpo Gwajima wawili inabidi nimtaje jina lote Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, naam! Napenda tu kumpa taarifa mchangiaji, pamoja na mchango mzuri anaousema kwamba siyo vizuri Tume ya Mipango kuwa chini ya Uenyekiti wa Rais. Nataka nimjulishe kwamba mipango yote inahitaji *political will* na kwenye nchi zetu mahala ambapo Rais wa nchi pia ni Mwenyekiti wa Chama ni muhimu Mwenyekiti wa Chama na Rais wa nchi awe *chairman* wa hiyo Tume ya Mipango ili a-*push* Serikali na *political will* pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kikanuni ulituelekeza ukishaenda kwenye hoja nyingine mtu hawezi kukupa taarifa kwenye hoja uliyoimaliza lakini taarifa hiyo siipokei kwa mantiki ile niliyoisema Rais hashauri anaelekeza. kwa

hiyo hiyo *issue* ya *political will* vivyo hivyo akiichukulia kwa upande hasi kwa upande chanya atasukuma lakini akiwa kwa upande hasi atazuia kwa hiyo, niseme Tume ya Mipango imshauri na iweze kuwajibishwa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Sheria ya Usalama wa Taifa. Nimesema hapa mambo mengi ambayo yameshauriwa kwenye Muswada huu tayari yanafanyika kwa mfano kuna kifungu cha saba nafikiri kinasema waweze kumiliki silaha, tayari wanamiliki silaha. Kifungu cha tano wanasema kuwalinda watu, sasa hapo ndio nataka niweke mkazo kidogo. Moja kati ya orodha ya watu ambao wanatakiwa kulindwa ni wagombea wa Urais wa vyama vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiisoma kama ilivyo kwenye Sheria unaona nia njema kabisa ya Serikali ukija kwenye utekelezaji huwezi kutofautisha taasisi hii na Serikali iliyoko madarakani, mfungamano wake ni mkubwa sana. Ni kweli kila mgombea Urais ili aweze Kushika dola ni lazima akubalike na vyombo vyote vya dola ili waweze kumpa dhamana ya kuongoza nchi.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai, najua tabia hufa polepole bado tuna changamoto kubwa ya Vyombo vyetu vya Usalama kutofautisha kati ya..

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA;** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Salome Makamba kwamba mgombea Urais yoyote ni *Potential President*, anauwezo wa kuongoza nchi hii kesho na sisi tuna mchukulia sawa, wagombea wote hawa wana haki sawa. Kwa hiyo, ukimuacha pasipokuwa na ulinzi akadhuriwa kuna uwezekano wa kumuua Rais wa kesho. Lazima tumlinde leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ulichokisema ndio nilichokisema kwa hiyo tuliza *ball* tuendelee hapa. Ulichokisema ndio nilichokisema mimi na hoja yangu ni kwamba watu wa vyombo hasa Usalama wa Taifa ni lazima wafahamu kwamba wao wanatakiwa kuwa *impartial* linapofikia kwenye suala la uchaguzi. Kazi yao ni kumlinda Mgombea Urais kwa maslahi ya Usalama wa Taifa na siyo usalama wa chama na hiyo ndiyo hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu ambacho kinasema Usalama wa Taifa hawatashitakiwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome ngoja nielewe jambo moja kutoka upande wa Serikali. Huu Uchaguzi wa 2020 Wagombea Urais wote walipewa walinzi wale walinzi wale waliokuwa nao wanatokea wapi? Annh! Sasa ndio sema kwenye kisemeo maana ukinijibu hivyo kitakuwa hakiingii kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Wale walinzi waliokuwa wamepewa 2020 na miaka mingine kuko nyuma wanatokea wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, walinzi wote walikuwa wanatokea Idara yetu ya Usalama wa Taifa.

**SPIKA:** Kwa hivyo ni sahihi kwamba Sheria hii hakuna jambo jipya inayoleta hicho ndicho kilichopo mpaka sasa hivi? Nitakuwa sahihi nikisema hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nachelea sasa sijui tujibu wakati tunajumuisha

**SPIKA:** Wewe nijibu mimi nataka kuelewa ili nimalizane na hoja ya Mheshimiwa Salome.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Sheria hii imeleta

mambo yote ambayo yanatakiwa kufanyika kwa muktadha wa sasa kwa hiyo hata unavyoona kwa mfano kwenye hiyo orodha ya wale viongozi tunawapa ulinzi pia tumeongeza watu lakini pia tumetengeneza vizuri iweze ku-*fit protocols* kwa hiyo tunakwenda…

**SPIKA:** Nataka kuelewa tu hii ya Urais. Wanalindwa na watu wanotoka Idara ya Usalama wa Taifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ndio wanalindwa na watu wanaotokea Idara ya Usalama wa Taifa.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Salome Makamba, malizia mchango wako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante jambo lingine kwenye Sheria hiyo. Jambo ambalo limeanzishwa ni kwamba hawa Usalama wa Taifa hawatashtakiwa kwenye makosa ya kijinai ambayo watayafanya wakiwa wanatekeleza majukumu yao kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, nia njema sijui tunaipimaje, sijui tunaipimaje wakati huohuo wamepewa ruhusa ya kumiliki silaha, wakati huohuo Sheria hii hii inasema hawa watu hawatakiwi kufichuliwa yaani wakiwa mahali hawatakiwi kufichuliwa hii iko kwenye vifungu vya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni ngumu kuipima nia njema, nashauri Serikali tuliangalie vizuri jambo hili ili tuweze angalau tulinde maslahi ya vijana wetu ambao wanafanya kazi kwenye idara hii, kazi ngumu na ya hatari lakini pia tulinde maslahi ya Watanzania ambao kuna wakati wanashindwa kukwepana na mazingira hayo, tulinde maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nitakwenda kwenye Sheria ya Usimamizi na Tozo za Ushuru wa Bidhaa, Mheshimiwa Waziri amesema wamebadilisha Kifungu cha 100 kwenye sheria hii kwenye Sheria ya Urekebu. Wamebadilisha Kifungu cha 100 kwa kuelekeza fedha zote zinazopatikana kutokana na Serikali

kushinda kesi za za kikodi zipelekwe Hazina. Hizi fedha, sheria iko tangu 2006 ikafanyiwa marekebisho 2008 na fedha hizi zilikua zinatakiwa ziende kwenye mfuko; nataka kuhoji Mheshimiwa Waziri hizi fedha zilikua zinaenda wapi? Ni shilingi ngapi? Tutazipataje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nishauri tu tufanye *special audit* kwenye eneo hili, kwasababu Serikali imeshinda kesi nyingi za kikodi na fedha zile zimerudishwa. Tumeona hapa kuna mambo ya kina *plea bargaining billions money* zilikua zinarudishwa Serikalini, zimekwenda wapi? Zilitakiwa ziende kwenye mfuko *since 2006*, 2008 sasa hivi wanasema ziende Hazina, je, na zile ambazo zimefanyika huko nyuma kabla ya kuwepo kwa sheria hii na zenyewe zitapelekwa Hazina? au … *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Ridhiwani kikwete, ajiandae

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa miswada hii ambayo ni ya muhimu sana kwa nchi yetu. Na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria nikushukuru pia kwa kutuamini sisi wajumbe wa Kamati ambao kwa kweli tumepitia miswada hiyo kwa uweledi mkubwa kwa kujitoa kwa muda na kuweza kufikia hatua hii ambayo tuko siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mimi nimpongeze sana mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utayari wake kuona mahitaji ya Nchi sasa yanahitaji hii miswada iletwe hapa tuijadili na mwisho wa siku tuipitishe kama sheria kwa ajili ya kutoa huduma kwa ajili ya nchi yetu. Niwapongeze wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, Kaka yangu, Mheshimiwa Boniphace Simbachawene, Naibu Waziri Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro na Naibu wake

Mheshimiwa Pauline Gekul na viongozi watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu na watumishi wote wa hizi Wizara zote mbili. Imekuwa ni kujibizana kwa hoja na mwisho wa siku tunaelekea katika eneo zuri la kuhitimisha miswada hii ikiwa na maslahi mapana ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niongelee kwenye Tume ya Mipango. Tunaona utari ya Mheshimiwa Rais kuja na tume ambayo itafanya kazi kwa uweledi wa mipango ya nchi yetu. Tunajua kwamba utaratibu huu umekuja ukiwa umetathimini pia na kuangalia ni sehemu gani ambapo tulikuwa na mapungufu. Tulikuwa na Wizara ya Fedha na Mipango tukaona kweli nchi inafanya kazi nzuri sana kwenye upande wa fedha, lakini ni nchi gani itaendelea kupiga hatua kubwa kukusanya fedha zaidi isipokuwa na mipango ambayo ni mizuri? Sasa ukiangalia muswada huu wa Tume ya Mipango hiyo yote inakuwa *addressed* mule ndani inajibiwa. Kwamba tukienda na utaratibu wa muswada huu ukawa sheria basi hayo mapungufu yote ambayo yalikuwa yako katika maeneo ya mipango yatakuwa yamejibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia muundo kwanza ulivyokuja, tukiangalia muundo, na nilikua namsikilia Mheshimiwa Wakili Msomi hapa Dada yangu na Shemeji yangu Makamba, hivi ni kiongozi ambaye ana utayari kujiweka mstari wa mbele, ili mumtathimi kwa kufanikiwa? Hili sasa amelifanya Mheshimiwa Rais kwa yeye kwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ili tumuone kwamba ana uzalendo na utayari wa kufanya kazi ili aweze kuvusha Taifa letu ambapo yeye ndiye mwenye maono kwa sasa. Kwa hiyo naomba tuondoe shaka kwamba Rais yuko tayari kuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo kwa sababu anajua dhamira ya dhati aliyonayo ni kuongoza nchi yetu na kuhakikisha kwamba Tume ya Mipango sasa imekuwa ya uweledi ni yenye mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Wajumbe na Wabunge wenzangu tuondoe shaka kwa Rais kuwa Mwenyekiti wa Tume hii. Lakini tunaona katika eneo hili weledi wa wajumbe wa kamati hawa ambao Mheshimiwa Rais atakuwa anafanya nao kazi; tunaona kwamba ni wakati gani ambao watatumia watu ambao ni wabobezi, watu ambao ni wazoefu katika

mipango ili sasa mipango hii ikija ina kuja na mipango ambayo kwa kweli inaakisi taswira ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi tumepitia kwa kina kwa niaba yenu kuhakikisha kwamba Tume hii itakapokuja inakuwa ni tume ya weledi. Mheshimiwa Askofu hapa *bishop* na yeye alikuwa na wasi wasi kidogo kwamba mipango hii inawezekana isilindwe vizuri mwisho wa siku ikawa ambayo haijalindwa. Lakini Kamati yako tuliliona na tukakaa na Serikali kwenye uboreshaji wa *amendmet*. Ukiangalia kwamba Ibara 67 (4) kama alivyooma Dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Alice, Mpango wowote wa muda mfupi na muda mrefu ulioandaliwa kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyingine iliyotungwa na Bunge na kuidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara 63 (3) (c) ya Katiba hautabadilishwa na kuachwa kutekelezwa katika muda uliopangwa kutekelezwa bila idhini ya Bunge. Kwa hiyo, tunaona katika kila nyanja kila sehemu mpango huu umelindwa. Kwa hiyo niwaondoe shaka Waheshimiwa Wabunge kwamba tupo katika mikono salama kuhakikisha mpango huu unafanya kazi na kuwa na maono ambayo imepangwa katika utaratibu ulio mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona wajibu ambao umepangiwa katika tume hii lakini sisi wenyewe ni wahanga na ni mashuhuda wa kuona mipango ikipangwa, utekelezaji unapokuja kufanyika ni kama inakinzana. Leo inakuja *TANROADS* au *TARURA* inachimba barabara nzuri kwa rasilimali za nchi, kesho inakuja *RUWASA* inapitisha bomba inachimba Barabara. Kesho inakuja kuziba kwa rasilimali zile zile za nchi. Lakini kama mipango ilikuwa ni madhubuti inajua miaka mitano ijayo hapa itapita barabara, itapita miundombinu ya maji, utapita Mkongo wa Taifa. *Provisons* zote zinakuwa zimewekwa, hautaona kwamba tunarudia kutumia rasilimali ya nchi katika kitu kile kile. Kwa hiyo sasa tunakuja na jibu ambalo litakuwa kwa kweli linasaidia nchi yetu kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona katika eneo hili Serikali imekuja na uwazi na kuonyesha kwamba ilipokuwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kweli kuna mambo makubwa ambayo mengine yaliachwa. Tulijikita katika kukusanya fedha na ndio maana nchi

yetu inaendelea kupata bajeti lakini kwenye suala la mipango halikufanyiwa katika weledi ule ule ambao inatakiwa. Sasa jibu lake ni nini, ni hili ambalo tupo nalo leo mezani. Waheshimwia Wabunge waamini kwamba baada ya hii sheria kupitishwa tunaamini mipango itakuwa mizuri na ni fedha zipi zinazopatikana bila kuwa na mipango mzuri? Tukiwa na mipango mizuri basi tutapata fedha nzuri na inawezekana tukapata na fedha zaidi. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tumepitia kwa umoja na kujibizana kwa hoja na Serikali suala hili liko kwenye mikono ambayo ni salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie kwa uchache katika eneo la Sheria ya Usalama wa Taifa. Tuna maboresho mazuri ambayo yamefanyika na tunaona Rais wetu katika sheria hii ina mtambua kama ni Rais ambaye ni msimamizi wa usalama wa Taifa letu, ambaye yeye amepewa ridhaa na wananchi wote wa Tanzania kuhakikisha kwamba nchi yetu iko salama. Kwa hiyo, jukumu hili anapolibeba yeye linakuwa katika hali ambayo tunaamini kwamba tutakuwa wananchi wote tupo katika mikono salama. Lakini tunaona Mheshimiwa Waziri anabaki pale akiwa anasimamia Sera na Bajeti. Kwa hiyo, mahitaji yote ya nchi yatakayokuja katika eneo hilo Waheshimiwa Wabunge watakuja hapa watapitisha, tutajadiliana vizuri, tutafikia muafaka na taasisi zetu zitaendelea vizuri katika kufanya kazi katika uweledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona hii Sheria ya Usalama wa Taifa imekuja ikiwa na uwiano unaolingana. Imeangalia maafisa wetu wanavyotekeleza kazi katika mazingira yao kwa unyeti wa kazi yao ikawawekea mazingira ya kufanya kazi lakini ikaangalia pia na haki zao za msingi katika kazi zao wanazozitekeleza. Unapokuwa unatekeleza majukumu kwa bahati mbaya ikatokea bahati mbaya hutakiwi kuhukumiwa kwa bahati mbaya iliyotokea. Ndicho tunachokisema kwamba pasiposhaka huyo mtumishi hatahukumiwa kwa kile kitu alichokitekeleza akiwa katika majukumu yake. Kwa hiyo hayo yote tumeangalia kwa upana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba, na sisi Waheshimiwa Wabunge tujiridhishe kwamba wanaosimamia taasisi hii na wenyewe ni Watanzania ni weledi, wamekula viapo

wanapenda nchi yao. Kwa hiyo, hakuna mtumishi anaweza akafanya kitu ambacho ni kinyume na taratibu, ukaona Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa anam-*support* au Mheshimiwa Rais anam-*support*, hapana. Kwa hiyo tuamini kwamba kuna watu ambao wapo pale juu yao ambao na wenyewe wanasimamia chombo hiki ili kiweze kufanya kazi kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yameguswa na sisi kama Kamati tumeangalia pia na misingi ya Katiba inafuatwa katika kutunga hii sheria. Tumeona kuna maeneo mengine ambapo kiongozi mkuu wa taasisi hii baada ya kumaliza muda wake ilikuwa inaonekana kwamba huu mtu sasa asipewe majukumu yoyote, ni kama una mfungia. Kufanya jukumu kama hili si adhabu. Kwa hiyo tuliamini kwamba akifanya kazi yake vizuri basi imefika muda kazi yake imemalizika anaweza akapangiwa majukumu mengine. Kwa hiyo utaratibu wa Nchi ambapo itaona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi bado niendelee kusisitiza mambo mengi mazuri yameongelewa, naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuungane kwa pamoja kupitisha miswada hii yote mitatu kama ilivyowasilishwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani kikwete, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwanza kukushukuru wewe mwenyewe kwa kutupa nafasi ya kuchangia Bungeni. Lakini kipekee sana nikushukuru kwa niaba ya Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kutupa jukumu hili kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge ili tupate nafasi ya kulitazama, kulichambua na kuishauri Serikali, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuishukuru Sekretarieti yako ambayo ulitupa kwa kweli wametupa ushirikiano mkubwa sana na

matokeo ya kazi hii ambayo umeiona mezani kwako ni mapato ya mchango mkubwa wa Sekretarieti yako pia.

Mheshimiwa Spika, nilitamani pia mbele ya Bunge lako hili Tukufu niwashukuru sana sana Waheshimiwa Mawaziri ambao walibeba Miswada hii na kuilete mbele ya Kamati yako. Kwanza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora lakini Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Gekul kwa kweli wametupa ushirikiano mkubwa sana kama Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na fadhila kama sitamshukuru Mwanasheria Mkuu, Dkt. Feleshi ambaye amekuwa na Kamati katika kipindi chote cha kuchambua na kujadili. Tumekuwa tunajibizana mpaka kwa *WhatsApp* kwa hoja mbalimbali. Kwa kweli Serikali ilijipanga vizuri na imetoa ushirikiano mkubwa sana kwa Kamati yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeona kwenye taarifa yetu ya Kamati, takriban asilimia 90 ya maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati, Serikali imechukua. Kwa kweli unaona hii ni Serikali ya aina gani, ni Serikali sikivu, ni Serikali iliyokubali kwamba nje ya Serikali kuna mawazo mazuri na kuna mawazo chanya yanayoweza kulijenga Taiafa letu. Kwa hiyo, nilitamani sana niweke hii kumbukumbu ya kudumu mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu ni Serikali sikivu haiji na mambo yake Bungeni ila inakuja na maoni na inapokea na maoni ya wadau na Wabunge kama ambavyo umeshuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa maeneo mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wamechangia kwa kikamilifu sana; na ninaamini wamelisaidia sana Bunge lako Tukufu kuelewa misingi ya mabadiliko yalioletwa na misingi ya sheria mbalimbali ambazo zimeletwa; lakini kubwa zaidi maeneo ambayo yanenda kuleta tija sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Ninashindwa ku-*comment* vifungu vingi kwa sababu kwa sehemu kubwa Waheshimiwa Wabunge wamevitaja. Lakini kwa sababu tu ya msisitizo nitaje maeneo machache ambayo

nadhani ni muhimu Waheshimiwa Wabunge wakarudia kuyasikiliza.

Mheshimiwa Spika, moja katika changamoto ambazo tulikua nazo ni kuwa na mipango mizuri lakini mipango isiyolindwa na sheria. Kwa hiyo, tumekuwa na mipango, tunapanga kila mwaka, tunarudia kwenye bajeti, Liganga na Mchuchuma inazungumzwa miaka 30 lakini hakuna hatua inayochukuliwa kwenye utekelezaji wake. Liganga na Mchuchuma ni moja katika miradi mikubwa ya kielelezo ya Taifa letu lakini hakukua na namna ya kuilinda kisheria. Sheria hii ya Tume ya Mipango imekuja na Kifungu Ibara ya Sita; na Mheshimiwa Dkt. Alice amesema, Mheshimiwa Mwinyi amesema na Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Florent Kyombo amesema; kwamba imelindwa sasa.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 6 inasema mpango wowote, Ibara ya 6(4) na hii, naomba nirudie, hii imekuja kama *Schudule of Amendment,* imekuja kama jedwali la marekebisho baada ya Kamati kuishauri Serikali ilinde mipango hii ambayo tunaiweka. Serikali niwashukuru sana mlipokea maoni haya ya Kamati mkaenda kutafuta namna gani mipango yetu tuilinde, na hiyo ndiyo namna pekee ambayo tutaisimamia mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imekuja na marekebisho ya jedwali, jedwali la marekebisho *Schedule of Amendment* Ibara ya 6(4), inasomeka kama ifuatavyo: "Mpango wowote wa muda mfupi au wa muda mrefu ulioandaliwa kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyingine iliyotungwa na Bunge na kuidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba hautabadilishwa au kuachwa kutekelezwa katika muda uliopangwa kutekelezwa bila idhini ya Bunge". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni moja katika ibara muhimu sana katika Sheria ya Tume ya Mipango kwa sababu nchi hii mipango tunayo, nchi hii mawazo mazuri tunayo lakini hatuyalindi na hatuyalindi kwa sheria. Kwa hiyo moja katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge walitaja; na nitambue mchango mzuri

wa Askofu Gwajima na Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia eneo hili kwamba tuulinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili kwa maslahi ya muda naona kengele ya kwanza imegonga. Ibara ya 20 inayofanya marekebisho Kifungu cha 19 cha sheria kuhusu suala la *good faith;* na nimuombe Mheshimiwa Makamba. *Good faith* imetafsiriwa kwenye sheria, naomba nimwachie hiyo *assignment* kwenda kutafuta tafsiri hiyo, lakini wanansheria hapa mpo mnajua *good faith* imetafsiriwa na hili ni suala la Kimahakama *upon convinction* kwamba umekutwa na hatia. Kwa hiyo, hili jambo lipo kisheria, niliomba nimuongoze mdau mwenzetu na mdau wetu mzuri sana wa masuala ya sheria, Mheshimiwa Makamba kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilitaka pia kama muda utaruhusu, Ibara ya 5(e) inaongelea ulinzi wa *Presidential Candidate during the general election* ambapo kulikuwa na *intervention* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ambayo ni *very relevant intervention,* inahusu ulinzi wa wagombea nafasi ya Urais. Sasa kwa sehemu Mheshimiwa Waziri amesema lakini kwa sehemu naomba niseme na hii pia naomba nimu-address Mheshimiwa Salome Makamba.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea ulinzi ambao unatolewa na Idara ya Usalama wa Taifa ni tofauti na aina ya ulinzi unaotolewa na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Kazi ya Usalama wa Taifa, Idara ya Usalama wa Taifa imeelezwa kwenye Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, sheria mama, Kifungu 5 (1) (a) mpaka (d) zinaeleza majukumu ya Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa hiyo, aina ya ulinzi tunaouzungumza sio hu ambao wenzetu wa Dar; na nilimsikia Mheshimiwa Zitto Kabwe kwenye mijadala huko nje akizungumza. Naomba arejee kwenye ibara hii inayoweka wigo wa shughuli za Idara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la muhimu zaidi, arejee pia kwenye Muswada uliopendekezwa. Muswada uliopendekezwa ibara hiyo hiyo ya 5A wamefafanua kazi za Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa hiyo tunapoongelea aina ya ulinzi kwa viongozi, haiondoi vyombo vingine vya ulinzi na usalama kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mambo mengi ya kuzungumzia, yamesemwa mengi lakini nitumie nafasi hii kukushukuru sana na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hoja yetu ya Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, niungane na wote waliochangia katika hotuba hii nzuri ya sheria zetu hizi mbili. Pia nitumie nafasi hii kuungana na wenzangu kukutakia kila la kheri katika nafasi unayogombea na sisi tunakuombea sana kheri na Mwenyezi Mungu *Insha Allah* atakusaidia, utafikia yale malengo makubwa ya ndoto zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya, lakini pia kuendelea kumshukuru yeye kutuamini mimi na bosi wangu Mheshimiwa Simbachawene kwa majukumu haya ambayo tunaendelea kuyatekeleza. Pamoja na hilo pia niishukuru Kamati yako nzuri na kwa kweli nataka nikwambie au nikuhakikishie wewe na Bunge lako, sisi kama Serikali kama ambavyo wenyewe wamejielezea hapa na ndiyo ukweli wenyewe kwamba hoja zote zilizotolewa na Kamati yako tumezichukua na tunawashukuru pia kwa yale maeneo machache ambayo na sisi tulitoa hoja zetu nao pia wamezichukua lakini hii ndiyo Serikali ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka kuiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muda mchache nilionao huu, naomba nijielekeze moja kwa moja katika maeneo machache sana na yale makubwa zaidi nimemwachia Mheshimiwa Waziri atakuja kudadavua zaidi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nataka nizungumze katika Tume ya Mipango. Tume yetu ya Mipango mnaweza kuwa mashuhuda kama alivyoeleza Profesa Kitila kwamba imekuwa inabadilika mara kwa mara tokea mwaka 1962 ilipoundwa.

Wameelezea Wajumbe wengine sitaki kurudia, lakini Tme inayoundwa sasa tofauti na Tume iliyokuwepo zamani. Tume ya zamani ilikuwa inaendeshwa kwa matamko yanaitwa Hati Idhini au kwa lugha ya Kiingereza wanaita *instruments* lakini hii ya sasa imekuja na sura ya kisheria na hii kwa kweli inaenda kutoa nguvu zaidi na hasa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwamba hii pia inakwenda kutoa na ulinzi wa mawazo mazuri na jinsi ambavyo Tume itaendeshwa na kwamba hakuna kitakachobadilika isipokuwa kwa idhini yako au ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhakikisha kwamba Nyerere wetu, Mwalimu Julius Nyerere mwanzilishi au *founder* anaendelea kuishi katika mioyo yetu kwa sababu hii yote ilikuwa ni ndoto yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia naendelea kuwashukuru sana wenzetu wote waliochangia katika hotuba ya bajeti kuhusiana na mabadiliko ya Sheria yetu ya Usalama wa Taifa. Nataka kuwatoa wasiwasi baadhi ya Watanzania ambao wana wasiwasi katika hili. Ndugu zangu, sheria hii imekuja kutuhakikishia usalama mkubwa kwetu. Imeongeza majukumu, lakini imeongeza *responsibility* kwa chombo, lakini pia imetoa nguvu kwa chombo na imeenda kutuhakikishia kwamba sasa chombo kinakwenda kupewa majukumu makubwa zaidi ikiwemo kwenda kulinda mpaka rasilimali zile ambazo zimeendelea kuanzishwa na kuendelea kusimamiwa katika maeneo yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pia nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja na pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, aje ahitimishe hoja zake zote mbili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, na mimi kama wenzangu nikutakie kila la kheri kwamba unakwenda kugombea nafasi ya kuwa Spia wa Bunge la Dunia. Nafasi hii ni kubwa na kwa hiyo kwa kweli Watanzania wote tuungane kumwombea Mheshimiwa Spika wetu Dkt. Tulia Ackson ili akaipeperushe bendera ya nchi yetu. Heshima hii kwa kweli siyo yako, wala siyo ya familia yako, ni heshima ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama kiongozi wetu wa Taifa letu la Tanzania, lakini kama ambaye amebeba dhamana ya Watanzania wote katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo na shabaha zake zote na malengo yetu ya kupambana na maadui watatu; ujinga, umaskini na maradhi yanashughulikiwa kikamilifu na katika kufanya hivyo Mheshimiwa Rais ndiyo maana amekuja na azma ya kuhakikisha kwamba tunaanzisha Tume ya Mipango katika kuifanya mipango ya nchi yetu iweze kuratibiwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chimbuko la suala hili, kwanza kabisa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili. Katika bajeti zetu mbili zilizopita Waheshimiwa Wabunge walizungumza sana juu ya umuhimu wa kuwa na Tume ya Mipango na kwa umuhimu huo, Serikali yetu sikivu na Mheshimiwa Rais akaamua kuanzisha mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipoanzisha mchakato huu alitoa maelekezo ya kwamba Tume hii ifanyiwe mchakato wa haraka na Waheshimiwa Wabunge leo hii tukipitisha sheria hii Mheshimiwa Rais ataisaini na itaanza kutumika tarehe 1 Julai kwa sababu anaisubiri kwa hamu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo rasilimali nyingi kama Taifa. Tunao watu, Watanzania ambao wameelimika vizuri sana, lakini tunayo rasilimali ardhi, lakini tunayo amani katika nchi yetu, lakini tunazo rasilimali mbalimbali hata kuzitaja ni nyingi mno. Tuna mito, mabonde, bahari, misitu, wanyama, madini na tuna kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitu hivi bila kufanyiwa utaratibu wa kuhakikisha kwamba vinasimamiwa na kuratibiwa vizuri unaweza ukavikuta badala ya kusaidiana katika kuleta maendeleo vinagombana na ndiyo maana imeelezwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli nataka niwashukuru takribani Wabunge wote 15 wamechangia huku na huku na jumla ya hoja zilizotolewa hapa ni nyingi na naamini hata ambao hawakusema wangeweza kuyasema haya haya juu ya umuhimu wa hii sheria ya kuanzisha rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, Tume ya Mipango kwa ajili ya kutekeleza mipango ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Niwashukuru sana kwa sababu hakuna hata mmoja aliyepinga, lakini niishukuru sana Kamati. Kamati hii ni Kamati yenye watu weledi, ni Kamati yenye watu makini. Kamati hii imekuwa ndiyo chachu ya mafanikio makubwa ya maboresho ya Muswada huu mpaka hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzito wa kazi ya Kamati, lakini usikivu wa Serikali, unauona kwa marekebisho mengi iliyofanya kupitia kwenye majedwali ya marekebisho. Ukiona majedwali ya marekebisho yalivyo marefu ujue Kamati imefanya kazi yake kubwa, lakini majedwali yakiwa marefu maana yake Serikali nayo imekuwa sikivu. Kwa hiyo nataka niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi katika kuhitimisha sijaona ambalo halijasemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge hata ambao walikuwa hawajasoma vizuri na wako nje ya Kamati, Wajumbe wa Kamati wamejitahidi sana kujibu na niwashukuru sana Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kyombo na Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Mhagama, lakini pia na Wajumbe wengine wote ambao wamejitahidi kutoa ufahamu mkubwa walioupata kwa wale ambao walikuwa hawajapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo yamesemwa kwamba Rais anawezaje kuwa yuko kwenye Tume lakini huku ni kwenye kifungu kile cha 7, ni kwamba ile kuwajibika kwenye taarifa kwenye Baraza la Mawaziri tumekifuta, kwa sababu Serikali imekuwa sikivu na Kamati imefanya kazi yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi hakuna *controversy* yoyote katika Miswada yote miwili na kwenye huu wa Usalama wa Taifa, kimsingi Wabunge wote wameunga mkono. Eneo hili ambalo limeleta kidogo mjadala la kinga dhidi ya Maafisa wetu wa Usalama wanapokuwa wakitekeleza kazi zao, ni wakati wakitekeleza kazi zao kwa majukumu yaliyosemwa kwa mujibu wa sheria. Siyo wewe ni Afisa wa Usalama unakwenda kugombana huko mtaani, umeitumia silaha yako vibaya, eti ukasema una kinga, hapana. Sheria itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia kinga katika kulinda usalama wa nchi na pengine tuna *underrate* jukumu la chombo hiki, kwa sababu pengine tunafikiria *domestically,* lakini chombo hiki kinalinda usalama wa nchi dhidi ya maadui wa nje zaidi. Kinalinda usalama wa nchi yetu juu ya mipango yetu ya maendeleo. Vita siku hizi ipo kwenye uchumi zaidi, chombo hiki kinalinda usalama dhidi ya mipango yetu ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kimsingi ni kama tumekubaliana na kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wana wasiwasi lakini pia wananchi walioko huko nje tunaona mijadala mbalimbali hakika ni kwa vile hawajapata fursa ya kupitia yale mambo mazuri ambayo Kamati hii imesimamia lakini Waheshimiwa Wabunge wanayafahamu, taratibu tunaweza tukakuta na wenzetu tuko pamoja kwa sababu hakuna jambo lililofanywa hapa kwa nia yoyote ile mbaya. Msingi mkubwa ni amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu, lakini na kulinda nchi yetu kama jukumu la kila Mtanzania na wenzetu hawa wamepewa jukumu hilo na kwa hivyo lazima tuwakinge dhidi ya mambo fulani fulani ambayo wanaweza wakawa wanatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la kinga limesemwa sana na huko mtaani kwamba wana kinga kwa sababu watafanya jambo fulani. Tunazungumzia kinga dhidi ya magaidi, katika kutekeleza jambo hili anapopambana na magaidi mtu wa Usalama wa Taifa halafu ikatokea silaha yake imefyatuka imemuumiza mtu, wewe unasema achukuliwe hatua lakini umemkinga *nurse* akimchoma sindano mgonjwa akafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinga hizi zimetolewa katika sheria mbalimbali katika nchi yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa Waziri:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** …na Waheshimiwa Wabunge wote wanafahamu. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na kupitia kwao Watanzania wote tuna jukumu sisi kama Watanzania kuhakikisha kwamba tunalinda nchi yetu dhidi ya maadui walio ndani na walio nje ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, naomba niwashukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini Katibu Mkuu wa Uwekezaji Dkt. Tausi Kida; *CPD* Onorius Njole; pia Katibu Mkuu Ikulu, Ndugu Mululi Mahendeka; Katibu Mkuu, Ofisi ya Utumishi kwa ushirikiano pamoja na utaalam wote waliotupatia katika kuhakikisha kwamba jukumu hili tunalitekeleza kuhakikisha kwamba sheria hizi zinatungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kupitia muda huu ulionipa, sasa nichukue nafasi hii kutoa hoja kwa Miswada yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa, tutaendelea na utaratibu wetu.

Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nami nitumie hadhara hii na fursa hii kukupongeza sana wewe na

kukutakia kila la kheri katika mchakato wa kuiwakilisha nchi katika Bunge la Dunia. Sisi tuna imani na wewe, tuna imani na uwezo wako, tunajua utaileteа sifa kubwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kwa dhati kabisa kuishukuru Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Kyombo pamoja na Wajumbe wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada ambao nimewasilisha leo unahusu Urekebu wa Sheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya Nne, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria za Serikali *(CPD)* ndiyo wenye mamlaka ya kufanya urekebu huo wa sheria. Nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na *CPD* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuleta Muswada huu. Umechelewa lakini umekuja na Kamati na Bunge lako limeunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge 15 ambao wamechangia Muswada huu na kwa ufupi wote wameunga mkono, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maelekezo mawili; la kwanza ni kwamba Miswada hii sasa iwe inakuja kwa lugha mbili, lugha yetu pendwa ya Taifa ya Kiswahili, lakini pia na lugha ya Kiingereza. Serikali hii ni Sikivu, tumelipokea hilo na tayari tumeshaweka *schedule of amendment* ili ikipita leo hoja hizo nazo ziwe sehemu ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja kutoka kwa Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, pacha wangu. Amehoji Sheria ya Ushuru wa Forodha yaani *Amendment of the Excise, Management and Tariff Act,* Sura 147 hususan kifungu cha 100. Mheshimiwa Salome hajapinga mabadiliko, ameyaunga mkono, kwenye hilo naomba kumshukuru sana. Hoja yake ni kwamba fedha zile zimekwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilifanya mabadiliko makubwa katika Mfumo wa Ukusanyaji Kodi Tanzania. Ikaunda chombo kipya kinaitwa Mamlaka ya Kodi Tanzania. Mamlaka ya Kodi Tanzania iliunganisha Idara ya *Sales Tax,* Idara ya *Income Tax* na idara ya *Excise Duty*. Idara hizi zilikuwa zinafanya kazi *independently* na kila moja ilikuwa na mfumo wake. Baada ya kuunganisha sasa zote zikaja chini ya Mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika kuunganisha huku kuna vitu vilikuwa havijapitiwa na ndiyo maana ya urekebu wa sheria. Tunaposema urekebu wa sheria au *revision* siyo *amendment* wala siyo kutunga sheria mpya, ni kurekebisha makosa madogo madogo ya kiuandishi ambayo yametokana na mabadiliko ya sheria. Katika hili niseme mamlaka makubwa anayo *CPD* pamoja na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pale mabadiliko yanapokuwa na uzito mkubwa na yakapelekea hata kubadilisha maana, ndipo tunakuja kuomba ridhaa ya Bunge. Kwa hiyo Mheshimiwa Salome kwanza aishukuru Serikali kwa kuleta haya. Serikali hii ingekuwa siyo makini, siyo *transparent* basi jambo hili lisingefika hapa, angemaliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa sababu ya uwazi wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi tumelileta kuiambia Bunge kwamba wakati tunabadilisha sheria mwaka 1995 tulisahau jambo hili, sasa tuliweke sawa, lakini muhimu zaidi ni kwamba ameunga mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa fedha zilikwenda wapi? Ukurasa wa nne wa taarifa niliyoisema, lakini kwenye *paragraph* au ibara ya 8 ya Muswada uliowekwa mezani imesemwa wazi kwamba fedha hii yote kuanzia mwaka 1995 ilikuwa inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na ukitaka kuiona utakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali utaisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mchango ulijaribu kufungamanisha fedha hii na *pre-bargain* hivi ni vitu viwili tofauti,

hii ni kodi ya kawaida siyo suala la *pre-bargain*. Mheshimiwa Salome unajua wewe ni Mwanasheria Msomi unaelewa kabisa, lakini ulitaka tu kutuma ujumbe kwa wananchi na mimi najibu ili kutuma ujumbe kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *good faith* au nia njema amelisema vizuri Mheshimiwa Mheshimiwa Simbachawane…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ahsante. Mheshimiwa Spika, hili suala la kulinda watu au kuwapa kinga halianzi tu na Maafisa Usalama wa Taifa hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani tuna kinga. Ukisoma Ibara ya 100(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Wabunge tuna kinga kwa mambo ambayo tumeyafanya humu ndani, tukitoka nje ya Bunge hili hatuna kinga lakini humu ndani tuna kinga, tumepewa kinga ile ili tusikwaze katika kutekeleza majukumu yetu, lakini kama tunafanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, hata humu ndani ukifanya pasipokuwa na nia njema ndipo utaona Kiti kinasimama na kinasema huyu aende kwenye Kamati ya Maadili, ujue nia yako haikuwa njema. Kwa hiyo, hata hiko kipimo cha nia njema humu ndani napo kipo hatujakianzisha sasa, na wapo watu wengi ambao wana kinga na hiki kipimo cha nia njema kinatumika kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, ninalishukuru Bunge lako tukufu kwa kuunga mkono jambo hili, naomba sasa niseme ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri Ahsante sana. Sasa kwa sababu nilikuwa nimesema naongeza nusu saa, tunaweza kuketi hoja

imeishaungwa mkono. Nilisema naongeza nusu saa naona watu wananitazama na sura fulani hivi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 34 (6) iwapo wakati wa kusitisha shughuli umefika na Spika atakuwa analihoji au yupo karibu kulihoji Bunge basi hatasitisha shughuli mpaka hoja iwe imeamuliwa. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Mtoa Hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2023 napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023 Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofayika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023 kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Baada ya kuungwa mkono sasa nitawahoji halafu tutaendelea na utaratibu wetu. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango kwa lengo la kuweka Mfumo Madhubuti kwa ajili ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Uandaaji, Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Mipango ili Kukuza Uchumi wa Nchi.**

*(Kusomwa Kwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeishasomwa kwa mara ya tatu na sasa tumeishamaliza kwa sehemu yetu kutunga Sheria kuhusu Tume ya Mipango na kwa kuwahoji ninyi baada ya mtoa hoja hapa kusema kwamba Bunge Zima tumemaliza kazi nimeishawahoji na sasa Katibu wetu ametusomea Muswada kwa mara tatu, utaratibu wetu wa kutunga Sheria hii umekamilika na kwa hivyo kwa mujibu wa Katiba yetu tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye aweze kuweka saini kama ataridhia halafu tutawaletea taarifa Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo nitumie fursa hii kuwashukuru sana Serikali kwanza mmesisitiza sana kuhusu usikivu jambo hili limepigiwa kelele sana na Wabunge lakini tumeona ndani ya muda mfupi mmeweza kulifanyia kazi na hii inaonesha nia yenu njema ya kufanyia kazi maoni wanayoyatoa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana Serikali kwa kutuletea Muswada huu ambao umeliwezesha Bunge kutunga Sheria na tunaamini kwamba mambo yote yataenda vizuri na huko baadaye pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwenye hoja hii Bunge limemaliza kazi yake.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

**MWENYEKITI:** Kifungu cha pili kina Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Waziri hapa mmesema kwamba katika Marekebisho mliyoleta kwenye Kifungu hiki, mmesema *deleting* kwenye (d) mnayo hapo Marekebisho? Kwenye (d) mmesema *deleting the word Tanzania when using in a relation to the country wherever it appears in the act and substituting for it the word United Republic*.

Mkiisoma kwenye ile Sheria Mama sehemu ambayo hayo maneno yapo mna uhakika mmeyapitia yote, ili tunavyopitisha yasije yakaenda kuwekwa halafu tukawa na sisi ndiyo tumetoa fursa ya yale marekebisho sasa kuingizwa tena haya maneno mengine. Sijui kama nimeeleweka? Maana mmesema neno Tanzania liondolewe liwekwe neno *United Republic* pale ambapo tunazungumzia Tanzania kama nchi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa marejeo yaliyofanyika wakati wa marekebisho, rejea kwenye Sheria Mama ilifanyika. Kwa hiyo, tunaamini

utoshelevu upo na kama kutatokea na machache sana yataangukia kwenye Mamlaka ya *CPD* chini ya Sheria Na. 4 Sura ya Nne.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Kifungu cha 8 pamoja na Marekebisho mengine yaliyoletwa na Serikali baada ya kushauriana na Kamati ni hii sehemu (c) Sehemu ya 8 (a)(ii)(aa)(c). *In the case of Deputy Director General for Tanzania Mainland is the Tanzanian hailing for Mainland* Tanzania. Siyo jambo ambalo pengine mnaweza kulifanyia hapo, lakini na

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni jambo la kulitazama kwa sababu Nchi yetu watu wanaishi popote wapendapo, kwa hivyo Mzanzibar anaeishi Tanzania Bara na maisha yake yapo Tanzania Bara atastahili kuwa *Deputy Director General for Tanzania Mainland* au hapana? na Mtanzania ambaye kwa sababu nadhani mngeangalia ile lugha iliyo kwenye Katiba ya Zanzibar namna ilivyoweka nani anaweza kuwa Rais wa Zanzibar pengine mngefuata ile lugha ingesaidia kuweka urali mzuri wa kifungu hiki. Kwa sababu nia njema, kwamba huyu Mkurugenzi Msaidizi, anaitwa Mkurugenzi Msaidizi au Makamu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Naibu.

**MWENYEKITI:** Naibu. Haya ili huyu Naibu kwa sababu mnataka kumlinda ambae ni wa Zanzibar awe Mzanzibar na huyu wa Tanzania Bara mnataka awe Mtanzania Bara lazima muweke lugha ambayo haitatokea mahali ambapo Mtanzania Bara anaeishi Zanzibar atajikuta kwamba amepewa hiyo nafasi au Mtanzania Mzanzibar ambaye anaishi Bara akapewa hiyo nafasi.

Kwa hiyo, mtafute lugha nzuri kwa hapo baadae ili hiki Kifungu muwe mmekiweka vizuri kwa namna ambayo nia yenu njema ilikuwa. Kwa sababu la sivyo kama nilivyosema, huku kuna Wapemba, kuna Waunguja, Zanzibar kuna Watanzania Bara wamejaa kule wanakaa muda gani? ndiyo utasema huyo ni wa aina ipi? Kwa hiyo, ni vizuri sana kutazama hilo kwa sababu tunaingiliana sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023)*. Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na Marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Services Amendment Bill, 2023)*.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 (The Tanzania Intelligence and Security Services Amendment Bill, 2023) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa kwa lengo la kufanya Sheria hiyo kuendana na mfumo wa utawala uliopo na taratibu za usimamizi wa Idara za Usalama wa Kimataifa na kuweka masharti ya utekelezaji bora wa majukumu ya Idara hiyo. (A bill of an act to amend The Tanzania Intelligence and Security Services in order to align the provision of the Act with the current Administrative and Global security practices and to put in place effective implementation of function of service)*

*(Kusomwa Kwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa mara ya tatu. Hii inahitimisha utungaji wetu wa sheria. Kwa hiyo, marekebisho haya ambayo yamefanywa katika sheria yetu ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka 2023 yamepitishwa rasmi na Bunge.

Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana upande wa Serikali kwa kuleta marekebisho haya ambayo yanafanya sasa

idara hii iweze kufanya mambo yake yote kisheria. Kwa sababu huko nyuma ilikuwa inafanya mambo ambayo ni ya muhimu sana kuyafanya na kwa kweli tumeona manufaa yake, lakini walikuwa wanafanya kwa utashi badala ya sheria.

Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kuleta Muswada huu na tunawatakia kila la kheri Mheshimiwa Rais atakapoweka saini yake, na tunaamini kwamba ataweka hiyo saini yake tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yale ambayo mmepewa kupitia sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge hilo linahitimisha hatua zote za utungaji wa sheria kwa Muswada huu na kwa hiyo, sheria hii imeshapitishwa rasmi na Bunge.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 *(The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna marekebisho ya Serikali wameongeza kifungu cha14.

Ibara ya 14

*(Ibara mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 15 kina marekebisho ya Serikali.

Ibara ya 15

**MWENYEKITI:** Sawa Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta marekebisho haya ambayo Serikali imeyaleta ya kuongeza hicho kifungu, maana yake mtiririko wa hizi namba utabadilika. Sasa kuliko kusoma 15 sasa ikiwa mpya tutabadilisha yote mwishoni. Kwa hiyo, namna ya kwenda kupanga itaenda kupangika vizuri.

Kwa hiyo, tutasoma 15 kama kinavyosomeka kwenye Muswada, halafu baadaye tutaenda kurekebisha baada ya kukubali hiki kifungu kipya kuingia hapo. Nadhani nimeeleweka Waheshimiwa Wabunge?

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 15 kina marekebisho ya Serikali.

Ibara ya 15

**MWENYEKITI:** Kifungu cha15 kina marekebisho ya Serikali. Mheshimiwa Waziri marekebisho ya Serikali mliyoleta kwenye kifungu hiki kinampa mamlaka *Chief Parliamentary Draftsman* kuondoa *schedule*. Hapa inabidi tu tuongee tu kizungu. *The Chief Parliamentary Draftsman may omit any schedule of an act if in his opinion its inclusion is inconvenient in the preparation and publication of the revised edition. At the same time* inasema, *provided the omitted schedule shall continue to form part of the act. Why would it be an inconvenience for the schedule which is part of the law to have inconvenienced who? The publisher or the CPD?*

Nani anayekuwa *inconvenienced* hapa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, katika kufanya urekebu. *Chief Parliamentary Draftsman* ana mamlaka yake ya kufanya mpaka kipimo fulani, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia ana mamlaka yake. Yanapozidi mamlaka ya *Chief Parliamentary Draftsman* na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni lazima yaje Bungeni. Sasa hapa tunaongelea hizo *limits* za *Chief Parliamentary Draftsman*.

**MWENYEKITI:** Ni nani anayeyapima? Ndiyo nijue kwamba yaani siyo madaraka ya Bunge yanayochukuliwa, nani anayeyapima? Yaani kwamba haya tutapeleka Bungeni, haya tutabaki nayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, anayepima ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hutokea mara nyingi kama usomaji wa kifungu cha sheria au sheria husika kilivyoandikwa kikawa na makosa ya kiufundi. Nyongeza ya swali lako hapa, *inconvenience* wakati wa *publication* ni hasa yale majedwali makubwa ambapo kuna

sheria kama zile za ujenzi ambayo kimsingi ni makubwa sana. Kwa hiyo, hiyo vile vile ilikuwa ni sehemu ya nyongeza ya kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Hiki kidogo kinanipa wasiwasi, yaani wasiwasi kwa maana ya kwamba zile *schedules* ni sehemu ya sheria, sasa kama ni sehemu ya sheria na unafanya urekebu wa ile sheria, unakuwa umeweka kifungu mle ndani kwamba *schedule* atazikuta wapi huyu anayesoma? Nataka tu kuelewa kwa ujumla. Ama unafanyaje? Yaani unaziondoa tu zinakaa huku kwa sababu ni ndefu, wakati kifungu kile kinasema hivi, utalikuta hilo jambo kwenye *schedule*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu elezea.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA – MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikutaarifu kwamba wakati Kamati inajadili, jambo hili ililijadili kwa kina na tulikubaliana na Serikali iweke *cross reference* wakati ambapo itaona kuna haja ya kuyafuata majedwali kwenye sheria mama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Hiyo *cross reference* maana yake ni kifungu ambacho Serikali inakwenda kuweka, ama *CPD* na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanaenda kuweka kwamba watakuwa wanaweka hiyo *cross reference*. Ama ninyi mmeiona tayari imo kwenye haya marekebisho!

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema kwamba inafanya marekebisho.

**MWENYEKITI:** Serikali kuna marekebisho hayo yanayoonesha kwamba mtaondoa hizi *schedule,* halafu mtaweka mahali kwamba *cross reference* tutaiweka mahali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinaongelea mamlaka ya *CPD,* siyo kwamba tunafanya hayo mabadiliko kwenye Muswada huu. Kimewekwa ili katika siku zijazo endapo *CPD* atakuwa anataka kucheza na haya au kugusa haya majedwali, afuate utaratibu huu. Kwa hiyo,

katika Muswada husika ambao uko Mezani leo, hakuna jedwali ambalo tunaligusa.

**MWENYEKITI:** Wakati anapewa hayo madaraka, si ndiyo inabidi awekewe hilo takwa la kwamba ikitokea amefanya haya tunayompa, lazima aoneshe kile ambacho Kamati inasema, ama hicho ataenda kusemea wapi? Sijui kama nimeeleweka!

Mwenyekiti wa Kamati anasema, wao wamekubaliana na ninyi kwamba yale ma-*schedule* yanakuwa marefu, makubwa, kwa hiyo, maana yake yatachukua kitabu kizima. Sawa yale mnayaondoa, lakini mmekubaliana kwamba wakati anaandika, kwa sababu sasa hayatakuwa tena pale, afanye *cross referencing.* Hayo mamlaka ya kupewa *cross referencing,* amepewa na Kamati kama mawazo ya mdomo. Hapa wakati huyu anapewa haya madaraka, si ndiyo hapa palitakiwa kusema! Kama ambavyo mmeandika, mmesema, "*provided that the omit schedule shall continue to form part of the Act, it was supposed to be part of this* kwamba ita-*form part of the Act* na atafanya hiyo *cross referencing.* Naamini Kamati ndicho inachojaribu kusema? Sijui kama naeleweka.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANSHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeeleweka. Nafikiri moja ni kwenda na hilo wazo, lakini lingine ilikuwa tuangalie kama kutakuwa na umuhimu wa kufanya marekebisho kwenye sheria ile ya sura ya nne yenyewe kwa kuongeza kwenye kipengele kinachompa mamlaka *CPD.*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa hapa kwa sababu haya mamlaka tunayompa ni ya muhimu katika hili zoezi la kufanya huu urekebu wa sheria, na pia kwa sababu sheria ile ilivyotungwa na Bunge imetungwa pamoja na hayo yanayosemwa, siyo yeye anayetunga. Kama hivyo ndivyo, tukimpa haya madaraka bila hicho kifungu, pengine sasa ndiyo ninyi Serikali, kwa sababu ndiyo tupo Bungeni hapa kutunga sheria. Kuna namna mbili. Moja, ni kuondoa hiki kifungu ili tuje tushughulike nacho mtakapoleta hayo marekebisho ili tuwe tumerekebisha sheria vizuri. Hiyo ni njia moja wapo.

Njia ya pili ni kukipitisha hiki kifungu kwamba mnaleta marekebisho. Siyo mnaleta hapa ndani, yaani mnaleta kwa utaratibu ule wa kawaida kabisa. Kwa hiyo, mimi nawapa nafasi mchague kati ya hizo mbili, kwa sababu sioni namna ambayo tutaweka kifungu hiki kikae kwa sura hii, halafu *CPD* tumempa mamlaka ya hiki kukiweka pembeni kikiwa na hizo changamoto. Tunaamini katika ile ile nia njema, sasa yeye akiondoa yale, tumempa mamlaka halafu atamwelekezaje mwingine huko mbele?

Kwa hiyo, chagua kati ya hizo mbili.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachagua njia ya pili.

**MWENYEKITI:** Njia ya pili.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** *Yes.*

**MWENYEKITI:** Marekebisho mnaleta lini ili hizi nguvu zisikae zina-*hang* huko? Tunaweza kufanya hivyo mwezi wa tisa, mtakuwa tayari mmelimaliza jambo hili?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada utakaofuata tutaleta hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, naona ulisimama.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimekusikia unasema kwamba yale majedwali. Wenyewe wanasema atafanya *cross reference* kama majedwali ni makubwa hayawezi kuingia kwenye hii sheria inayofanyiwa urekebu. Kwa uelewa wangu ni kwamba, yale majedwali, hiyo *cross referencing* hayatakuwa mahali, yaani wakiwa wanayasoma, wanasoma hii sheria mpya ambayo imefanyiwa urekebu, wanafanya rejea ya majedwali ambayo yapo kwenye sheria ambayo imefutwa ile ya 2002. Siyo kwamba yatakuwa mahali kwamba kuna kitabu maalum cha majedwali. Ile *cross reference* ni kwamba watasoma, lakini watawaambia *refer* jewali

ambalo liko kwenye sheria ile ambayo imefutwa. Kwa hiyo, lile jedwali halitafutwa, yaani litakuwa halijafanyiwa *revision*.

**MWENYEKITI:** Haya. Wewe umemwita huyu ni wakili msomi sijui, haya Mwanasheria hebu nieleweshe. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuseme kwamba hapa hakuna sheria tunayofuta. Mheshimiwa Salome anapo-*refer* sheria ya mwaka 2002, zile nazo hazifutwi. Maana ya urekebu ni kwamba, masahihisho madogo madogo, tutakuwa tuna-*refer* sheria zetu kama ambavyo zimerekebishwa mwaka 2022. Hili likipita leo, tuta- *refer* kama zilivyorekebishwa mwaka 2023. Kwa hiyo, hatufuti sheria yoyote, *it is just a way of referring them* na hakuna jedwali ambalo liko kule, tunalisubiri hapa. Hapana. Tunachoongelea ni mamlaka ya *CPD* endapo itahitajika kugusa majedwali fulani na mengine ni makubwa, ndicho tulicho-*discuss* hapa.

**MWENYEKITI:** Hapo umeweka hoja vizuri. Lile neno "endapo" ndiyo linatakiwa liweke sasa yale tunayosema lazima iwepo huku ili sisi tuwe tumetunga sheria ambayo iko kamili. Kwa hiyo, hayo "endapo" ndiyo ataongezewa hapo. Uzuri umeshasema kwamba umechagua njia ya pili. Kwa hiyo, sisi tutakuwa tunasubiri hicho kifungu ili mamlaka ya *CPD* yakamilike kwenye eneo hili. Hilo eneo mlifanyie hayo marekebisho ili tusije tukajikuta…

Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba zile sheria za zamani zinafutwa. Hoja yangu ni kwamba, wenyewe hawataki kurudia ku-*print,* urekebu unaofanyika 2023, hawataki kurudia ku-*print* yale majedwali makubwa. Kwa hiyo, ili kupunguza hiyo gharama ya ku-*print* majedwali makubwa, kifungu kitasomeka kwamba utafanya rejea ya yale majedwali ambayo yako kwenye *revised edition* ya 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tutapitishaje kifungu ambacho kina *discrepancy?* Yaani hoja hapa ni kwamba hicho kifungu kinatakiwa kiondolewe wakilete kwenye marekebisho ya

sheria zinazofuata mbeleni, lakini tukisema tukipitishe na upungufu, wasipoleta!

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa sababu mimi ndiyo mtoa hoja kwenye hoja hii, Waheshimiwa Wabunge lazima tuelewane vizuri. Tukikipitisha hiki kifungu namna kilivyo maana yake ni kwamba Serikali inaweza kuendelea na ule mchakato, lakini sasa inaweza ikaendelea na mchakato ukiwa hauna yale majedwali. Mpaka pale ninaposema mchakato, inamaanisha hawatatoa mpaka kile kimeletwa hapa, ndiyo majedwali yasiwe sehemu. Sijui kama tumeelewana! Yaani ndiyo hoja yenyewe hapo ilipo.

Waheshimiwa Wabunge, ina maana ya kwamba, tukiipitisha tunampa *CPD* mamlaka ya kuendelea kwa hapa tulipoishia. Yale majedwali yatakayokuwa wameyaweka huko yalipoenda, maana anasema watakuwa wameyaweka. Kwa sababu sheria yetu tunavyotunga inakuwa imekamilika. Sasa tunampa mamlaka kwamba hii sheria ni kubwa sana, ishia hapa. Ndiyo tunachofanya hapa. Tunampa mamlaka kwamba *CPD* unaweza kuishia hapa. Sasa ili tumwelekeze *CPD* kwamba sisi bwana tulipotunga sheria ilikuwa kubwa, hapa padogo, weka hayo maneno "endapo," ndiyo Mheshimiwa Waziri watayaleta hayo maneno ya "endapo" ili sasa ule mchakato uliofanywa kule mbele uende vizuri. Nadhani tumeelewana vizuri.

Mheshimiwa AG niko sahihi, ama?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona ni vizuri labda tufanye vilevile kuangalia kifungu cha 8 kifungu kidogo cha (2).

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 8 cha nini?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sheria ya *Law Revision* ya 2015, ambapo mamlaka ya *CPD* ni pamoja na ku-*collect references* na *cross references.* Sasa tukafikiri hoja yetu iwe kwamba…

**MWENYEKITI:** Sasa kwa sababu hiyo sina hapa, ehe, malizia hoja yako, halafu nipate na mimi kilichoandikwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ni kwamba sheria ipite, halafu basi endapo kutajitokeza changamoto inayobadili maana ya kifungu, tutakuja sasa na ile *option* ya pili ambayo ulikuwa umeelekeza.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa sababu hatuwezi kuwa tunarudia kukirekebisha kila wakati, ndiyo maana tukiweka endapo, maana yake kama haihitajiki, haihitajiki. Kama ipo maana yake ipo. Si ndiyo? Si ndiyo hata ninyi hapa mmetumia haya maneno, sijui wapi mmesema? Ngoja, Hapa mmesema: "*If in his opinion its inclusion is inconvenient.*" Kwa hiyo, kama mmempa hiyo *leeway* na huku chini mnampa hiyo hiyo leeway. Si ndio? Haya hebu leta hicho kifungu unachosema.

Mheshimiwa *AG*, ngapi ngapi? *Subject 2 (8) in the preparation of the revised edition, The Chief Parliamentary Draftsman and has and may exercise the following powers. (i) correct references and cross references*. Ulikuwa na hoja yako hapa sasa nimesoma naweza kukuelewa sasa. Hoja yako ilikuwa ni nini Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa ni kwamba tukiangalia kifungu hiki inaendana sasa na yale maelezo ya kamati na kama yalivyokubaliwa na kuja kwenye jedwali la marekebisho ya kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Ni sawa lakini nafikiri kwa ajili ya *neatness* ya sheria wewe kilete kikae hapo kwa sababu ile imetoa mamlaka yote kwa ujumla hapa umekuja na mahsusi unataka kuhusu yeye kupunguza hicho anachokipunguza. *Cross referencing* nadhani wote tunajua maana yake ni ile ya jumla lakini hapa unaongelea *schedules* sasa hizi *schedules* zipate neno lake mahsusi. Nadhani tukubaliane kwenda kwa sura hiyo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama naweza kusaidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tulijadili hii pia kwenye kamati hata ukisoma sheria aliyosoma *AG* bado neno *convenient* lipo linatumika linampa *CPD* mamlaka. Inasema hivi kifungu cha 5(2) *notwithstanding sub section one, The Chief Parliamentary Draftsman may cause subsidiary registration to be published in an appropriate form separately from the acts under which the subsidiary registration is made, in any case where it appears to him to be convenient or appropriate do so.*

.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa huku kwenye neno *convenient* tulishatoka. Tunataka ku-*safe guard* mamlaka ya Bunge, si ndio? *AG* si tumeelewana kwenye hoja hii na Mheshimiwa Waziri tumeelewana, nadhani twende kwa sura hiyo ili hapa maneno iki kifungu chetu kiwe na ukamilifu mtaleta yale marekebisho, Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hicho ni kifungu cha kumi na tano, si ndio Katibu?

**NDG. ZAINABU ISSA- KATIBU MEZANI:** Ndio.

*(Vifungu tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Vifungu tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Kifungu tajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Vifungu tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarudia.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria ya Mwaka 2023 yaani *(The Laws Revision, Miscellaneous Amendments Act 2023)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na mrekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali yatokanayo na urekebu wa Sheria ya mwaka 2023 *(The Laws Revision, Miscellaneous Amendments Act 2023)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINABU ISSA- KATIBU MEZANI:**

*Muswada wa Sheria ya yatokanayo na Urekebu wa Sheria mbalimbali zipatazo nane kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi la urekebu katika Sheria hizo (A Bill of an act to amends certain laws in order to address various shortcomings realised in those laws in course of Laws Revision Exercise)*

*(Kusomwa Kwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na kwa katibu kusoma Muswada huo mara ya tatu unaashiria kumalizika kwa hatua zote za utungaji wa Sheria na hivyo nitumie fursa hii kutangaza kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali yatokanayo na Urekebu wa Sheria ya Mwaka 2023 *(The Laws Revision, Miscellaneous Amendments Act 2023)* umepitishwa rasmi na Bunge na tutampelekea Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuweka Saini yake ili sasa iwe Sheria tayari kwa ajili ya kutekelezwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuishukuru Serikali pia kwa kutuletea Muswada huo ambao umeliwezesha Bunge kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ambazo ilisha zitunga huko nyuma na tunawatakia kila la kheri katika yale ambayo mmekusudia kuyafanya pale ambapo Mheshimiwa Rais atakuwa ameridhia Muswada huu kuwa Sheria.

Waheshimiwa Wabunge na ninyi nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa ushiriki wetu, tukiongozwa na Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria wamefanya kazi nzuri, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote na Waheshimiwa Wabunge wote mliopitia Muswada huu na kutoa michango yenu na wengine mmetoa michango yenu kulingana na taarifa ya Kamati. Kwa hiyo, tumemaliza kazi hii kwa ushirikiano wetu sote pamoja. Kwa hiyo, nawashukuru sana na kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru tena kwa uvumilivu kwa muda wetu umekwenda sana lakini sote tuko hapa ndani, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo linalo wahusu Wabunge wanawake wa Chama cha Mapinduzi mnakumbushwa kuhudhuria kikao muhimu cha Umoja wa Wanawake Tanzania katika ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuhairishwa shughuli za Bunge leo. Kwa hiyo, mkitoka hapa Wabunge wanawake wa Chama cha Mapinduzi mnatakiwa kuelekea Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nahairisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 8.57 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*